# Nipashe

Jumatano Oktoba 5, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581089

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ

MWANGA WA JAMII

0745 700710

LIKE & FOLLOW



SUPA JACKPOT

TZS.1,037,361,877

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Polisi** yataja walichobaini kujinyonga Katibu Kanisa la Masanja

UKURASA 25



**HARMONIZE AWAKATAA 'MACHAWA'**

UKURASA 27

# TAMISEMI mfupa mgumu mawaziri

• **Miaka** 7 mawaziri 5, mtihani wa Kairuki huu hapa... *Endelea ukurasa 2*



Simbachawene
**(2015 - 2017)**



Selemani Jafo
**(2017- 2021)**



Ummy Mwalimu
**(2021 Machi – Jan. 2022)**



Innocent Bashungwa
**(Jan. 2022 - Sept. 2022)**



Angellah Kairuki
**(Sept.3, 2022 mpaka sasa)**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**PM AAGIZA MKAKATI WA NGO UTAFSIRIWE KISWAHILI**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezindua Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa...

## Rais ataka ufumbuzi vikwazo ubunifu katika afya

UKURASA 2




Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Kiongozi wa Taifa la Qatar, Sheikh Tamim bin Hamad Al Thani (wa pili kulia), baada ya kuwasili kwenye ofisi za kiongozi huyo, Doha nchini humo jana. **PICHA: IKULU**

## Utata kifo aliyekutwa na kanga shingoni

UK.25

**MICHEZO** **NABI ATETEA MAYELE KUTOTETEMA** UK.32

**KABWELA** UK.7




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza wakati akifungua mkutano wa wadau wa demokrasia kujadili masuala mahususi ya Zanzibar yanayohusu demokrasia ya vyama vingi vya siasa, Unguja jana. **PICHA: IKULU**

# TAMISEMI sasa mfupa mgumu kwa mawaziri

**Na Mwandishi Wetu**

NI mfupa mgumu. Hivyo ndivyo inavyoonekana hali halisi ndani ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kutokana na mabadiliko makubwa kwa mawaziri wanaoteuliwa kuiongoza.

Hiyo inatokana na mawaziri walioteuliwa katika kipindi kisichozidi miaka saba ya serikali ya awamu ya tano na ya sita kudumu kwa muda mfupi kisha kuondolewa au kuhamishiwa wizara zingine.

Awali, kutokana na unyeti wa wizara hiyo, ilionekana kama neema kwa mtu kuteuliwa kuwa waziri. Lakini sasa imekuwa mwiba mchungu au shubiri kwa wanaopewa nafasi hiyo.

Kwa ujumla, TAMISEMI ni taasisi nyeti kwa kuwa inasimamia mambo mengi yanayohusu mambo muhimu yanayohusu wananchi kama vile afya, elimu, maji na miundombuni hasa ya barabara na madaraja. Sehemu kubwa ya fedha zinazotokana na bajeti ya serikali, hupelekwa kwenye halmashauri za mitaa kwa ajili ya utekelezaji wa hiyo.

Pamoja na kuwa ni eneo nyeti katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika utekelezaji wa miradi mbalimbali, hali imekuwa tofauti kutokana na miradi mingi kutekelezwa kwa kiwango duni.

**MIAKA 7 MAWAZIRI 5**

Kuwapo kwa madudu ndani ya halmashauri, kumekuwa kama mfupa mgumu au kaa la moto kwa mawaziri wanaoteuliwa kuongoza TAMISEMI. Kila mara Rais anapofanya uteuzi, amekuwa akikemea ugoigoi katika ukusanyaji mapato pamoja na udokozi.

Wakati akitangaza mabadiliko ya Baraza la Mawaziri muda mfupi baada ya kuchukua nafasi ya Rais (marehemu) John Magufuli, Rais Samia Suluhu Hassan alimwagiza aliyekuwa Waziri wa TAMISEMI, Selemani Jafo, akasimamie ipasavyo mapato ya halmashauri na kubana mianya ya uvujaji wa mapato.

Kwa kauli hiyo inaonyesha kwamba katika halmashauri nyingi kuna upigaji mkubwa wa fedha zinazotolewa na serikali kuu pamoja na zile za mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Tangu kuingia kwa serikali ya awamu ya tano chini ya Magufuli, Novemba 2015 hadi sasa, takriban miaka saba, mawaziri watano wameiongoza TAMISEMI baadhi wakiwa hawajamaliza hata mwaka na kuondolewa.

Desemba, 2015 Dk. Magufuli alipotangaza Baraza lake la kwanza la Mawaziri, alimteua George Simbachawene kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ambaye alikaa hadi Septemba 17, 2017 alipojiuzulu. Baada ya Simbachawene, Selemani Jafo aliteuliwa kuongoza wizara hiyo hadi Machi, 2021 kisha akaingia Ummy Mwalimu aliyeongoza hadi Januari, mwaka huu.

Ummy ambaye kwa sasa ni Waziri wa Afya, alimpisha Innocent Bashungwa ambaye naye amekaa takriban miezi tisa na kuhamishiwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Angellah Kairuki aliteuliwa Jumapili iliyopita kushika usukani wa kuongoza wizara hiyo.

**MAMBO MAZITO**

TAMISEMI ambayo kwa kiasi kikubwa inaonekana ndiyo roho ya serikali katika maendeleo kwa ajili ya wananchi na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM, inakabiliwa na mambo mazito ambayo kwa namna mbalimbali ni dhahiri mfupa mgumu kwa mawaziri wanaoteuliwa hata kuondolewa ndani ya muda mfupi.

Mambo hayo ni kuwapo kwa madudu mbalimbali yakiwapo ya upigaji wa fedha za maendeleo zinazotoka serikali kuu na mapato yanayotokana na makusanyo ya ndani katika halmashauri. Matokeo yake, miradi mbalimbali imekuwa ikifanyika chini ya kiwango.

Sababu kubwa ni kuwapo kwa usimamizi hafifu wa viongozi waliopewa dhamana. Mfano wakati Mwenge wa Uhuru ukiwa mkoani Pwani, Kiongozi wa Kitaifa wa Mbio za Mwenge mwaka huu, Sahili Geraruma, amekemea tabia ya miradi ya maendeleo kutokamilika kwa wakati kunakosababishwa na usimamizi hafifu wa viongozi

Kuwapo kwa tabia hiyo, Rais Samia wakati akiwaapisha wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa hivi karibuni, aliwataka viongozi katika halmashauri zote kuhakikisha fedha zinazotolewa na Serikali zinahudumia wananchi kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo.

Alisisitiza kuwa fedha hizo zimekuwa zikitolewa kwa ajili ya maendeleo ya sekta mbalimbali zikiwamo maji, afya na elimu, hivyo zitumike ipasavyo katika kusukuma miradi ya maendeleo ya wananchi na wahusika wasibadili matumizi.

Mikataba yenye kutia shaka katika baadhi ya halmashauri na taasisi za fedha ni moja ya madoa yanayoifanya TAMISEMI kuonekana kuwa na matatizo. Mfano wa mikataba hiyo ni wa Sh. bilioni 20 kati ya Manispaa ya Benki ya TIB.

Pia kumekuwa na matatizo katika masoko yaliyoko kwenye halmashauri ikiwamo miundombinu duni na ufujaji wa mapato. Sheria za utekelezaji wa mapato ya masoko ikiwamo ya kutaka asilimia 15 ya mapato hayo kuhudumia masoko ikiwamo ukarabati wa miundombinu haitekelezwi ipasavyo.

Aidha, katika vituo vya mabasi vikiwamo katika miji mikubwa, makusanyo yake yamekuwa hayajulikani yanakwenda wapi hivyo kutokuwapo kwa tija katika miundombinu hiyo. Kwa maneno mengine, vituo vya mabasi vimekuwa vichaka vya upigaji wa mapato ya serikali yatokanayo na chanzo hicho.

Tatizo lingine lililoko katika TAMISEMI ni ukusanyaji duni wa mapato ya ndani ikiwamo kukadiria kiwango cha chini tofauti na vyanzo vya mapato. Rais pia alionya hilo na kuzitaka halmashauri kupitia viwango vya ukusanyaji wa mapato na kuziba mianya ya upotevu wa mapato ili zijihudumie na kujikimu kwa mahitaji ya kiofisi.

Sambamba na hilo, kumekuwa na tatizo katika mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani kwenye halmashauri kwa vijana, wanawake na wenye ulemavu. Katika mikopo hiyo, mabilioni yamekuwa yakitolewa bila kuwapo kwa marejesho, hivyo kupotea bila taarifa.

Makusanyo ya mapato yamekuwa duni katika baadhi ya halmashauri hivyo kupewa hati chafu mara kwa mara huku baadhi ya fedha zinazokusanywa katika vyombo mbalimbali baadhi zikiishia katika mikono isiyo salama.

# Rais Samia ataka ufumbuzi vikwazo ubunifu katika afya

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameiomba jumuiya ya kimataifa kujadili na kuvipatia ufumbuzi vikwazo vitatu vinavyotajwa kurudisha nyuma juhudi za kufanya ubunifu kwenye sekta ya afya nchini na dunia kwa ujumla.

Samia alitoa wito huo jana mjini Doha nchini Qatar alipokuwa akishiriki kwenye ufunguzi wa Mkutano wa Dunia wa Ubunifu wa Masuala ya Afya.

Alisema vikwazo vinavyorudisha nyuma juhudi za ubunifu kwenye sekta ya afya nchini ni pamoja na ukosefu wa wafanyakazi wenye ujuzi. Rais Samia alivitaja vikwazo vinne kuwa ni uhaba wa miundombinu na kukosekana kwa fedha za kufadhili ubunifu.

"Niwaombe wote kuchukua fursa hii kutafuta mawazo ya pamoja kujadili njia bora tunazoweza kutumia kukabiliana na changamoto hizi na kuzipatia ufumbuzi," alisema Rais Samia.

Aliongeza kuwa Tanzania haijabaki nyuma kama zilivyo nchi zingine kwa kuwa imekuwa ikitumia kasi ya mabadiliko ya teknolojia kufanya ubunifu ambao umekuwa na tija kwenye sekta ya afya na taifa kwa ujumla.

Pia alibainisha kuwa teknolojia hizo zimekuwa na manufaa katika kupunguza vifo vya wajawazito na watoto na kwamba hatua ambazo serikali inaendelea nazo kwa sasa ni kuhakikisha teknolojia hizo zinasambaa Tanzania Bara na Zanzibar.

"Baadhi ya uvumbuzi ambao umekuwa na tija nchini ni mfumo wa simu wenye kumwezesha mjamzito kuita usafiri kwa dharura na kupelekwa hospitali M-Mama pamoja na teknolojia inayotembea ya kulea watoto wenaozaliwa kabla ya wakati," alisema Rais Samia.



## HABARI KITAIFA

# PM aagiza mkakati wa NGO utafsiriwe Kiswahili

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezindua Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (National Strategy for NGOs Sustainability) na kuagiza utafsiriwe kwa Kiswahili.

"Katika kuhakikisha uratibu wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Serikali unatekelezwa kwa ufanisi, ninaielekeza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kukamilisha tafsiri ya Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kutoa fursa kwa wadau mbalimbali kuuelewa sambamba na kuunga mkono jitihada za kukiendeleza Kiswahili."

Alitoa wito huo jana wakati akizindua Mkakati huo pamoja na Madawati ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Kisekta katika ukumbi wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.

Waziri Mkuu ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, aliitaka wizara hiyo ihakikishe Mkakati huo unazingatia maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa Septemba 30, 2021 kuhusu kufungamanisha mipango ya NGOs na ya serikali ili kuhakikisha shughuli zao zinakuwa endelevu.

Alisema serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa kutoka kwa mashirika yasiyo ya kiserikali katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Pia maboresho kwa sheria, kanuni na miongozo inayosimamia mashirika yasiyo ya kiserikali.

Aliyataka mashirika yote yasiyo ya kiserikali yaboreshe mawasiliano na mamlaka za serikali katika maeneo yaliyopo na kutoa taarifa sahihi kuhusiana na shughuli zinazofanywa ili kuimarisha dhana ya uwazi na uwajibikaji.

Pia, alizitaka wizara na mamlaka za mikoa na wilaya zihakikishe mashirika yote yasiyo ya kiserikali yanatekeleza shughuli zao kulingana na usajili, malengo na vipaumbele vya taifa. Aidha, aliyataka mashirika yasiyo ya kiserikali yajielekeze kufanya kazi maeneo yenye uhitaji ikiwemo vijijini badala ya kujikita katika maeneo ya mijini pekee.

Kuhusu madawati yaliyozinduliwa jana, Waziri Mkuu alisema amepewa taarifa kuwa wizara 19 tayari zinayo madawati hayo na kuziagiza wizara nyingine ambazo bado hazijaanzisha madawati hayo, zihakikishe zinateua maofisa dawati ili kurahisisha uratibu wa mashirika hayo katika sekta zao.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu amewataka viongozi wa mashirika hayo yenye makao makuu nchini waweke fedha kwenye benki za ndani ili fedha zinazoletwa nchini ziwe na thamani zaidi.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
04.10.2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Alhamisi tarehe **06-10-2022** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Rufiji,** gari hizo zina namba za usajili: **T 499 BKC / T 837 CHK, T 419 DFC / T 325 BYR, T 897 BNS / T 385 DHQ, T 195 BTE / T 153 CHN**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 18**
**Upana - mita 4.20**
**Kimo - mita 4.60**

2. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji** kupitia Kibiti, gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

XXXXXX

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***



DRC DANISH REFUGEE COUNCIL

**TANGAZO LA ZABUNI**

**SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUNUNUA MAJIKO YANAYOTUMIA NISHATI YA JUA**

**KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAARIKA WAZABUNI KULETA BEI ZAO.**

**NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA TAREHE 05.10.2022 HADI TAREHE 18.10.2022 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.**

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA +255625482649 au barua pepe sadock.kabuko@drc.ngo**

**ZABUNI ZITAFUNGULIWA HADHARANI TAREHE 20.10.2022 SAA 4:00 ASUBUHI OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI YA DANISHI.**

217076902

**UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA RFQ.TZA@drc.ngo AU KULETA MOJA KWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI.**



halopesa *150*88#

# Ada za wateja

217077501


| Kiwango (TSH) | | Customer fee (TSH) | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kwenda HaloPesa | | | Kwenda mitandao mingine | | | Tuma kwa namba isiyosajiliwa | | | Kutoa pesa | | |
| Kutoka | Mpaka | Makato ya HaloPesa | Tozo ya Seri kali | Jumla ya makato | Makato ya HaloPesa | Tozo ya Seri kali | Jumla ya makato | Makato ya HaloPesa | Tozo ya Seri kali | Jumla ya makato | Makato ya HaloPesa | Tozo ya Seri kali | Jumla ya makato |
| 100 | 999 | 10 | 10 | **20** | 10 | 10 | **20** | - | 10 | **10** | - | 10 | **10** |
| 1,000 | 1,999 | 20 | 10 | **30** | 32 | 10 | **42** | 350 | 10 | **360** | 300 | 10 | **310** |
| 2,000 | 2,999 | 20 | 10 | **30** | 32 | 10 | **42** | 380 | 10 | **390** | 300 | 10 | **310** |
| 3,000 | 3,999 | 50 | 14 | **64** | 63 | 14 | **77** | 475 | 14 | **489** | 400 | 14 | **414** |
| 4,000 | 4,999 | 55 | 27 | **82** | 77 | 27 | **104** | 530 | 27 | **557** | 500 | 27 | **527** |
| 5,000 | 6,999 | 130 | 54 | **184** | 162 | 54 | **216** | 710 | 54 | **764** | 780 | 54 | **834** |
| 7,000 | 9,999 | 130 | 56 | **186** | 162 | 56 | **218** | 790 | 56 | **846** | 780 | 56 | **836** |
| 10,000 | 14,999 | 320 | 102 | **422** | 450 | 102 | **552** | 1,250 | 102 | **1,352** | 1,200 | 102 | **1,302** |
| 15,000 | 19,999 | 320 | 195 | **515** | 450 | 195 | **645** | 1,250 | 195 | **1,445** | 1,200 | 195 | **1,395** |
| 20,000 | 29,999 | 360 | 306 | **666** | 495 | 306 | **801** | 1,550 | 306 | **1,856** | 1,500 | 306 | **1,806** |
| 30,000 | 39,999 | 370 | 351 | **721** | 558 | 351 | **909** | 1,620 | 351 | **1,971** | 1,600 | 351 | **1,951** |
| 40,000 | 49,999 | 380 | 419 | **799** | 648 | 419 | **1,067** | 1,800 | 419 | **2,219** | 2,100 | 419 | **2,519** |
| 50,000 | 99,999 | 580 | 573 | **1,153** | 900 | 573 | **1,473** | 2,350 | 573 | **2,923** | 2,500 | 573 | **3,073** |
| 100,000 | 199,999 | 700 | 707 | **1,407** | 1,350 | 707 | **2,057** | 2,750 | 707 | **3,457** | 3,300 | 707 | **4,007** |
| 200,000 | 299,999 | 750 | 821 | **1,571** | 1,620 | 821 | **2,441** | 4,200 | 821 | **5,021** | 4,500 | 821 | **5,321** |
| 300,000 | 399,999 | 950 | 838 | **1,788** | 1,800 | 838 | **2,638** | 5,600 | 838 | **6,438** | 5,500 | 838 | **6,338** |
| 400,000 | 499,999 | 1,200 | 982 | **2,182** | 1,980 | 982 | **2,962** | 6,600 | 982 | **7,582** | 6,000 | 982 | **6,982** |
| 500,000 | 599,999 | 1,300 | 1,245 | **2,545** | 2,520 | 1,245 | **3,765** | 7,500 | 1,245 | **8,745** | 6,400 | 1,245 | **7,645** |
| 600,000 | 699,999 | 1,400 | 1,532 | **2,932** | 2,880 | 1,532 | **4,412** | 7,600 | 1,532 | **9,132** | 7,000 | 1,532 | **8,532** |
| 700,000 | 799,999 | 1,400 | 1,700 | **3,100** | 2,880 | 1,700 | **4,580** | 7,650 | 1,700 | **9,350** | 7,000 | 1,700 | **8,700** |
| 800,000 | 899,999 | 1,750 | 1,500 | **3,250** | 3,150 | 1,500 | **4,650** | 8,100 | 1,500 | **9,600** | 7,500 | 1,500 | **9,000** |
| 900,000 | 1,000,000 | 1,750 | 1,776 | **3,526** | 3,150 | 1,776 | **4,926** | 8,300 | 1,776 | **10,076** | 7,500 | 1,776 | **9,276** |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 3,000 | 1,875 | **4,875** | 3,600 | 1,875 | **5,475** | 8,300 | 1,875 | **10,175** | 7,500 | 1,875 | **9,375** |
| Above 3,000,000 | | 3,000 | 2,000 | **5,000** | 4,500 | 2,000 | **6,500** | 8,300 | 2,000 | **10,300** | 7,500 | 2,000 | **9,500** |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kuongezwa mabasi ya DART kulete ufanisi wa usafiri

**MAHITAJI** ya usafiri wa umma katika miji yoyote hasa ya kibiashara lazima yatakuwa makubwa kutokana na shughuli zinazofanyika kila siku, iwe kibiashara, kiofisi na kijamii.

Kutokana na mahitaji hayo, ndiyo maana wadau wa sekta ya usafiri nchini wakaona fursa ya kuwapo kwa mabasi ya jumuiya ambayo yatasaidia abiria ambao hawana magari binafsi kurahisishiwa usafiri.

Na katika hali hiyo, serikali iliona umuhimu wa kuanzisha mabasi yaendayo kwa haraka ili kuepuka msongamano wa magari na kuwarahisishia abiria kufika sehemu zao za kufanyia shughuli kwa haraka.

Ili kuwezesha sekta hiyo inakuwa endelevu, Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka (DART), imesema imejipanga kuongeza mengine 177 ili kuboresha huduma hiyo.

Ahadi hiyo ilitolewa jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa DART, Dk. Edwin Mhede, wakati wa kikao cha pamoja baina ya viongozi wa taasisi hiyo, wakuu wa wilaya na wakuu wa polisi wa Wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa wakala huo wakati wowote DART itasaini mkataba na mzabuni na baada ya kusaini mabasi hayo yatawasili nchini ndani ya kipindi cha miezi sita ijayo na kuanza kutoa huduma kwenye sehemu zitakazoainishwa.

Kwetu tunasema hatua hiyo ni nzuri na itarahisisha huduma ya usafiri kwa wananchi wengi.

Pia kutokana na hatari ya kupata magonjwa ya mlipuko, mabasi hayo yatakapoongezwa yatasaidia idadi ya watu wanaosongamana katika magari hayo kupungua.

Kadhalika tuna imani kuwa njia zilizopangiwa magari hayo kupita zikiwamo zinazoelekea kwenye hospitali kubwa kama kutoka Muhimbili kwenda Mlonganzila zitarahisisha wanaougua au kuuguza waende kwenye hospitali hizo kwa urahisi.

DART iliamua kuitisha mkutano wa wadau kuweka mikakati ya pamoja kuhakikisha kunakuwa na ulinzi na usalama wa kutosha kwenye matumizi ya miundombinu ya magari hayo.

Usafiri huo utapelekwa Kibaha Mkoa wa Pwani na kwa sasa wanahudumia makundi maalum kama ya wazee na wenye changamoto za maumbile.

Kwa sasa mabasi yao yanawahudumia watu 180,000 kwa siku na yatakapowasili mabasi mengine idadi hiyo itaongezeka mara dufu na kupunguza muda wa msafiri kukaa muda mrefu kusubiri basi.


Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Heri James naye alisema wamekubaliana kusimamia miundombinu ya DART na mabasi yake ili watumiaji wa usafiri huo wasipate shida.

Katika kudhibiti matumizi yasiyotakiwa katika barabara zinazopita magari hayo, Mkuu huyo alisema serikali haitawavumilia watu wanaojaribu kuhujumu miundombinu ya DART kwa kuwa serikali imewekeza fedha nyingi kwa lengo la kuwapunguzia adha ya usafiri wananchi wake.

Serikali haitakubali kuona hasara ya mara kwa mara inayosababishwa na watu kupita kwenye miundombinu ya DART wakati hawatakiwi kufanya hivyo na wakuu wa wilaya wamekubaliana kwa pamoja na polisi kusimamia suala hilo kwa nguvu zote.

Ujio wa magari hayo unasubiriwa kwa hamu ili sekta ya usafiri nchini iendelee kuimarika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Makada waepuke rushwa kulinda hadhi ya CCM

Na Sabato Kasika

**CCM** inaendelea na uchaguzi wa viongozi ambao sasa umeingia ngazi ya wilaya huku baadhi ya vigogo waliokuwa wenyeviti wa chama wa wilaya wakiangushwa.

Wakati chama kikiendelea na mchakato huo, tayari kimefuta baadhi ya matokeo ya uchaguzi ukiwamo wa Umoja wa Vijana UVCCM, na kusimamisha mwingine wa Umoja wa Wanawake-UWT kutokana na sababu mbalimbali.

Kwa mujibu wa Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, miongoni mwa sababu za kufutwa kwa uchaguzi ni ukiukwaji wa maadili, rushwa na upangaji wa safu za uongozi.

Si mara ya kwanza chama hicho kufuta uchaguzi kutokana na sababu hizo, kwani kimewahi kufanya hivyo wakati wa serikali ya awamu ya tano, kitendo ambacho kilitosha makada kuzingatia taratibu za chama na kujifunza.

Wakati wa awamu ya tano CCM, ilifuta matokeo katika kata 41 zilizofanya uchaguzi ngazi mbalimbali, kutokana na kukiuka taratibu za uchaguzi ikiwa ni ishara ya kuelekea kuwa na chama na Tanzania mpya.

Kufutwa kwa uchaguzi huo kulielezwa kuwa ni matokeo ya ukiukwaji wa kanuni na katiba ya CCM, kuendeleza makundi baada ya uchaguzi, kupanga safu za uongozi kwa maamuzi ya nani awe kiongozi, huku ikielezwa jambo hilo ni kinyume na utaratibu na sheria.

Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi wa wakati huo Humphrey Polepole, alisema wote waliosababisha kadhia hiyo wangechukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu za CCM, wengi walidhani kwamba kufutwa kwa uchaguzi huo kungetosha kuwafunza makada wa chama hicho, kuachana na mtindo huo wa kutofuata taratibu, lakini umejirudia tena mwaka huu.

Ingekuwa ni vyema kama makada hao wangekuwa wanaingia katika uchaguzi kwa kuzingatia taratibu zote za chama na jumuiya zake ili wapigakura wachague viongozi wenye nia ya kukitumikia chama na wale wananchi wanaowakubali.

Imewahi kutokea kwenye uchaguzi ndani ya CCM wakati wa awamu ya tano, baadhi ya maeneo wajumbe wa vikao wa chama hicho kutopewa taarifa sahihi za wagombea na kusababisha kuchagua viongozi wasiokuwa na sifa.

Kwa kuwa chama kinaongozwa kwa mujibu wa katiba na kanuni, makada wazingatie hilo ili kuondoa sintofahamu kama hizo za kufutwa kwa matokeo kutokana na ukiukwaji taratibu na maadili ya chama.

CCM, ni chama kikongwe na tawala, hivyo si vyema baadhi ya wanachama wake wakiharibie sifa mbele ya umma kwa kuingiza mambo ambayo ni kinyume katika uchaguzi wa viongozi, ni wakati wa kukifanya kiwe kioo kwa vyama vingine vya siasa, kwa kufanya mambo kwa utaratibu bila kuingiza 'figisu', ili kuwahamasisha wanaotamani kujiunga wawe na imani nacho.

Ninatambua kwamba CCM ni chama kikubwa, 'figisu' haziwezi kukosekana, lakini pamoja na hayo, jambo la muhimu ni kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na haki, ili wanachama wapate viongozi wanaowataka.

Rushwa na ukiukwaji wa taratibu na kanuni za chama visingepewa nafasi badala yake kiendelee kuwa kioo cha vyama vya upinzani, ili viweze kupata mambo muhimu ya kujifunza.

Wakati huo akiwa Mwenyekiti wa CCM, Jakaya Kikwete, aliwahi kuonya rushwa ndani ya chama hicho na kusema itakiua na kuwataka wanachama kujiepusha nayo, lakini imeendelea kuwa mwiba hadi leo.

Kufutwa kwa uchaguzi katika maeneo kadhaa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ukiukwaji wa maadili, rushwa na upangaji wa safu za uongozi, ni wazi kwamba vitendo hivyo bado vinaishi ndani ya chama hicho.

Hivyo, hata hatua zilizochukuliwa na chama hivi karibuni za kufuta baadhi ya uchaguzi, zingekuwa fundisho la kuwafanya wagombea kurudi kwenye mstari, watafute uongozi kwa kutafuta yaliyomo kwenye katiba ya chama.

Vilevile, ni vyema wale wanaotarajia kuingia kwenye kinyang'anyiro katika ngazi ya mkoa, wajifunze kwa yaliyowakuta wale waliofutiwa uchaguzi, ili katiba ichukue nafasi yake katika kupata viongozi wa chama.

## HABARI KITAIFA




Msajili wa Hazina, Benedicto Mgonya (katikati) akiwa ameshika bango la Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), uliozinduliwa mkoani Dar es Salaam jana, katika maadhimisho ya wiki ya huduma kwa mteja. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), Dk. Elirehema Doriye na (kulia) ni Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL Mhandisi Ladislaus Matindi. **PICHA: FRANK MONYO**

# Wadau walia na zabuni jengo uwanja wa ndege

**Na Gwamaka Alipipi**

CHAMA cha Waendesha Shughuli za Anga Tanzania (TAOA) kimeiomba Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) kuingilia kati mchakato wa zabuni wa usimamizi wa kuendesha jengo jipya la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume Zanzibar.

Hivi karibuni Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) ilitoa agizo ambalo lililipa kampuni binafsi ya Dubai (DNATA) mkataba wa usimamizi pekee wa kuendesha jengo hilo.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na Menejimenti ya TAOA, chama hicho kinauona uamuzi huo ni ukiukwaji wa kanuni na taratibu za ununuzi wa zabuni na kanuni za usafiri wa anga.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa miongoni mwa kanuni zilizovunjwa, ni kanuni ya 20 ya usafiri wa anga kwa wapakia na washusha mizigo kwenye ndege za mwaka 2012.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa kanuni hiyo inaelekeza taratibu za kumchagua mtoa huduma kuwa za uwazi bila upendeleo na zenye kuendana na viwango vya ushindani vya kimataifa na zenye kufuata kanuni na sheria za zabuni za umma.

Kwa mujibu wa agizo la ZAA, kuanzia Desemba Mosi mwaka huu huduma katika uwanja huo wa ndege zitatolewa na kampuni ya DNATA kutoka Dubai na mashirika ya ndege yatalazimika kutumia mtoa huduma mmoja.

"Hii ni kinyume cha uamuzi wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania Na. 1 wa Mwaka 2022 unaokataza ukiritimba na mgawanyo wa vituo vya viwanja vya ndege.

"Agizo hilo litafifisha ushindani wa kibiashara na hivyo kutowalinda watumiaji wa huduma ambao sheria inakusudia kuwalinda," chama hicho kililalamika kupitia taarifa yake hiyo.

Chama hicho pia kilidai kuwapo kandarasi kampuni hiyo ya Dubai bila kuwapo mchakato wa zabuni ZAA kumeweka mfano mbaya kwa sekta ya usafiri wa anga na kutia doa jitihada za kuvutia wawekezaji wa kimataifa.

Taarifa hiyo pia ilibainisha uamuzi huo unakwenda kinyume cha mienendo bora ya biashara ya kimataifa katika huduma za anga.

"Hivyo basi jumuiya inaiomba TCAA kuingilia kati suala hili na kuimuru ZAA kufikiria tena agizo lake kutokana na athari kubwa itakayojitokeza kwa waendeshaji wa mashirika ya ndege ya nje ya nchi, watoa huduma wa viwanja vya ndege na watumiaji wa viwanja vya ndege kwa ujumla," chama hicho kilisisitiza.

Nipashe ilimtafuta Mkurugenzi wa ZAA, Juma Juma, kuzungumzia suala hilo, akiwa na mrejesho kwamba wakati wa mchakato wa kumpata msimamizi, wadau walikuwapo.

Alikiri wadau hao walishapeleka malalamiko yao katika Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) na kwa sasa suala hilo linashughulikiwa.

Hivyo, aliwataka wadau hao kuwa na subira wakati suala hilo linafanyiwa kazi na mamlaka husika.

# Waonywa kubadili matumizi ya ardhi

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula amezionya halmashauri nchini kuacha utaratibu wa kubadilisha matumizi ya ardhi bila sababu za msingi.

Dk. Mabula, alitoa onyo hilo juzi jijini Dodoma wakati wa kuhitimisha kikao kazi kilichowaunganisha wakurugenzi wa halmashauri na wataalamu wa sekta ya ardhi.

"Sasa hivi kila mmoja anaondoa open spaces (maeneo ya wazi), anataka kupima viwanja, anafuta mashamba anataka kupima viwanja hata kama bado yako katika sura ya kijijini ya kimashamba na anataka kila sehemu kuwe fremu," alisema.

Alitolea mfano Jiji la Dodoma, akisema limeanza kusheheni fremu wakati ni makao makuu ya nchi na kusema haiwezekani kuwa na miji ya aina hiyo ambayo haipangwi kwenye sura ya makao makuu kwa kujaza fremu na vituo vya mafuta na kusisitiza kuwa hiyo si sahihi kitaaluma.

Kwa mujibu wa Waziri wa Ardhi, wapo wataalamu wengi katika sekta ya mipango miji na mabadiliko ya matumizi yasiyo na sababu za msingi hayakubaliki kwa kuwa yanawakosesha hata watoto maeneo ya kucheza na miji kupumua.

"Mipango iliyopangwa awali inatakiwa kubaki siyo kuendekeza mabadiliko ya matumizi kwa kujaza fremu au vituo vya mafuta na kuharibu miji, tunahitaji maeneo ya matumizi ya umma," aliagiza.

Kupitia kikao hicho kilichohudhuriwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Laurean Ndumbaro, Dk. Mabula aliwataka wakurugenzi ambao halmashauri zao tayari zina mipango kabambe, kutoruhusu ujenzi kuendelea kwenye maeneo yao bila kuzingatia mipango hiyo na kusisitiza umuhimu wa maeneo kutunzwa kwa kuzingatia mipango kabambe badala ya kufuata mkumbo wa kutaka kubadili matumizi ya ardhi na kuharibu sura ya miji.

Kikaokazi kati ya wakurugenzi wa halmashauri na wataalamu wa sekta ya ardhi kimefanyika kwa lengo la kupata maoni kuhusu muundo mpya wa utendaji kazi wa wataalamu wa ardhi katika ngazi ya Halmashauri.

## KABWELA



# SMZ yaitaka NMB iongeze ATM za kubadilisha fedha za kigeni

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BENKI ya NMB inaendelea kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja na shughuli za maadhimisho hayo zilizoanza kufanyika kitaifa Jumatatu huko Zanzibar huku Serikali ya Mapinduzi ya Znzibar (SMZ) ikiitaka iongeze kasi ya kuzisambaza mashine za kubadilisha fedha za kigeni (FX-ATMs).

Uzinduzi wa ATM ya kwanza ya aina hiyo visiwani hapa ambayo ni ya tatu nchini ulikuwa moja ya matukio matatu katika siku hiyo ya ufunguzi wa maadhimisho hayo ambayo NMB iliyatumia kuonyesha thamani aliyonayo mteja na inavyochangia ustawi wa jamii na kushiriki kwenye maendeleo ya kibiashara nchini.

Viongozi waliokuwapo walisema mashine hizo zinahitajika kwa wingi na kwa haraka ili taifa liwahi kunufaika na huduma hiyo mtambuka yenye tija kubwa kibiashara na ufanisi kimaendeleo kwenye uchumi wa kidijitali.

Walisisitiza umuhimu wa NMB ambayo mpaka sasa ndiyo pekee iliyo na ATM hizo kuhakikisha inaziweka sehemu zote zinapohitajika kwa wakati mwafaka.

Mashine ya kwanza ilizinduliwa mwaka 2020 kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) na ya pili ilisimikwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanaro (KIA) hivi karibuni.

Tukio la pili lilihusu uwajibikaji wa benki hiyo kwa jamii kupitia michango mitatu ya uwekezaji wa kizalendo wa zaidi ya Sh. milioni 20 kwenye sekta ya elimu na msaada kwa watu wenye ulemavu.

Akizungumza kabla ya kuzinduliwa kwa mashine ya FX-ATM kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Amani Abedi Karume, Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa NMB, Benedicto Baragomwa, alisema shughuli zote hizo tatu ni muhimu kwa benki hiyo na maendeleo ya Tanzania kwa ujumla hasa kufanikiwa kwa ajenda ya uchumi wa buluu.

Juzi benki ilianza kusherekea wiki hii ya huduma kwa wateja katika Kanda ya Dar es Salaam kwenye tawi la Mlimani City ambapo Mkuu wa Idara ya Huduma kwa Wateja wa NMB, Abella Tarimo alisema uzinduzi wa mashine ya kubadili fedha umekuja katika muda mwafaka kwa kuwa ndicho kipindi ambacho taifa linapokea wageni wengi.

Pia kwa Kanda ya Magharibi, Benki ya NMB ilitumia tawi la Kigoma kuendeleza sherehe za huduma kwa wateja kwa kukutana na wateja, pia kutoa misaada mbalimbali kwa shule kadhaa za msingi mkoani hapo. Jana sherehe hizo kwa Kanda ya Ziwa zilisherehekewa katika Tawi la Kaitaba mjini Bukoba.

Baragomwa alisema: "Katika kusherehekea Wiki ya Huduma kwa Wateja, tunazindua huduma muhimu sana ya ATM ya kubadirishia fedha za kigeni hapa kwenye Uwanja wa Kimataifa Amani Abeid Karume ambao ni lango kuu la watalii wengi wanaokuja katika visiwa hivi na Tanzania yote."

Aliongeza kuwa NMB pia inaitumia wiki hii kuadhimisha mwaka mmoja wa kuanza kutumika kwa Hati ya Huduma kwa Mteja ambayo ilianzishwa katika maadhimisho ya mwaka jana kuonyesha kwa vitendo nguvu ya huduma kwa wateja wa benki hiyo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango wa Zanzibar, Dk. Saada Salum Mkuya, aliyewakilishwa kama mgeni rasmi na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Miundombinu na Uchukuzi, Shomar Omar Shomar, aliipongeza NMB kwa uimara na umahiri wake kiutendaji na kiuendeshaji.

Alisema kuiweka ATM ya fedha za kigeni itakayoanza na kuzibadilisha dola, pound na euro kwenye uwanja wa ndege ni fursa kubwa kiutalii na mtaji mzuri kwa uchumi wa taifa.

"Tunaambiwa kuwa mashine hii ni mojawapo ya mashine nyingine ambazo zitawekwa kwenye viwanja vya ndege vyote vya kimataifa nchini. Ni jambo jema na litasaidia sana huduma hii ya kubadilishaji fedha. Rai yangu jambo hili lifanyike kwa haraka na maeneo yote lengwa yawe na mashine hizi," aliagiza.

Baada ya kupokea mchango wa NMB wa madawati 100 kwa ajili ya skuli za Regeza Mwendo na Chunga pamoja na mabati ya Skuli ya Fuoni na vifaa vya kuwasaidia wenye ulemavu, Shomar alisema kwa sasa umuhimu wa uwajibikaji wa kampuni kwa jamii (CSR) hauna mbadala.




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Miundombinu na Uchukuzi Zanzibar, Shomari Omari Shomari (wa tatu kushoto), akikata utepe kuzindua ATM ya NMB, kwa ajili ya kubadilisha fedha za kigeni kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume Terminal 3, jijini Zanzibar jana. Wa (pili kushoto) ni Ofisa Mkuu wa Ukaguzi wa Ndani Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa, Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Rashid Simai Msaraka (wa pili kulia), Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard (wa tatu kulia) na Kaimu Mkuu wa Biashara Zanzibar, Naima Shaame (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT na polisi wavutana zuio la mikutano kisiasa

**Na Mwandishi Wetu,** TUNDURU

KATIBU Mkuu wa ACT Wazalendo, Ado Shaibu amesema ataendelea na ziara yake wilayani Tunduru, licha ya zuio la Jeshi la Polisi kwa madai ya kuwapo kwa tishio la ugaidi.

Ado, alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na wanachama na viongozi wa ACT Wazalendo katika Kata ya Namwinyu, Jimbo la Tunduru Kaskazini.

"Nimemwelekeza Katibu wa Mkoa, Ndugu Mtutura awajulishe polisi kwa maandishi kuwa ninaendelea na ziara yangu kwa sababu sijaona msingi wa kisheria wala wa kimantiki kwenye katazo la polisi.

"Polisi wajue kuwa neno ugaidi siyo la kufanyia mzaha. Lina madhara makubwa kitaifa na kimataifa. Unaposema kuna tishio la ugaidi, unaleta taharuki isiyo lazima. Rais Samia, ametumia nguvu kubwa kuhamasisha watalii na wawekezaji. Yote hayo unayahujumu kwa sababu za kisiasa kwa kuzusha kuwapo kitisho cha ugaidi.

"Ninaendelea na ziara ili kuitangazia dunia kuwa Tunduru na Tanzania ni shwari na salama na wapuuze habari za kuwapo kwa kitisho cha ugaidi," alisema.

Ado aliongeza kuwa hatua hiyo ya Jeshi la Polisi kumzuia inazidisha ari ya ACT Wazalendo, na wapenda haki nchini kupigania mageuzi ya kimuundo, kisheria na kiutamaduni katika Jeshi la Polisi ili lijiendeshe kwa haki, weledi na kwa kutanguliza mbele maslahi ya Taifa.

Mwishoni mwa wiki Jeshi la Polisi wilayani hapa liliuandikia barua uongozi wa ACT Wazalendo, ukizuia kufanyika kwa mikutano ya kisiasa iliyoombwa na Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado.

# Simbachawene ataja sababu mbili mauaji ya wazee

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, amesema mauaji ya wazee yaliyotokea mwaka huu yamesababishwa na tamaa ya mali na imani za kishirikina na kuvitaka vyombo vya ulinzi na usalama kushirikiana na jamii kukomesha vitendo hivyo.

Pia ameagiza Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaotekelezwa kupitia Mpango wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kufanya tathmini kubaini wazee wanaopaswa kupewa huduma stahiki ili kuwatoa katika umaskini.

Simbachawene aliagiza hayo juzi jijini hapa alipozungumza kwa niaba ya Waziri Mkuu kwenye kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani yaliyoandaliwa na Wizara kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali la HelpAge International Tanzania.

Alisema kwa mujibu wa takwimu kuhusu hali ya mauaji ya wazee nchini, mwaka 2021 nchi ilikuwa shwari na halikutokea tukio lolote. Hata hivyo, kwa mwaka huu 2022 mwanzoni nchi iliingia kwenye doa kubwa.

Simbachawene alisema mikoa ambayo matukio hayo yalitokea ni Singida (Iramba) ambapo wazee watatu waliuawa kwa kuchomwa moto wakiwa ni wanawake na Mkoa wa Ruvuma mzee mmoja alizikwa akiwa hai huku Mbeya mzee aliuliwa na mwanawe.

"Jamii yote tunahusika, viongozi wa dini, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ni bora kushiriki na kuhusika katika kukinga matukio haya, maana hayajianziagi mara moja, ni dhahiri yanakuwa na dalili zake, hivyo sote tushikiane," aliagiza.

Waziri huyo alihimiza jamii kuwafichua wahalifu ili vyombo vya dola vidhibiti viashiria vya uhalifu mapema.

Pamoja na hayo, Simbachawene aliagiza kuharakishwa kwa mchakato wa maboresho ya Sera ya Wazee ya Mwaka 2003.

Alibainisha kuwa jumla ya mabaraza 20,749 yameanzishwa nchini kote ili kuwapa fursa wazee kukutana na kujadili mambo yao, pia kutumika kama chombo cha ushauri katika jamii.

Katika hatua nyingine, Waziri Simbachawene alisema nchi inakopa kwa sababu ina heshima ya kukopeshwa na kuonyesha kushangazwa na wanaohoji sababu za 'serikali kukopakopa'.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alikemea tabia ya watu kuwahusisha na ushirikiana mzee ambao macho yamekuwa mekundu na yanatoa machozi na wengine wamezeeka na migongo kupinda.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Taifa, Lameck Sendo alishauri hatua zichukuliwe kwa wanaoua na kuwafanyia ukatili wazee.

HABARI KITAIFA

# Sababu kufutwa uchaguzi UVCCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) umetaja sababu za kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi kwenye wilaya tatu kuwa ni kutokana na washindi kudanganya umri.

Pamoja na hilo, umoja huo umetangaza kuanza mchujo wa wagombea walioomba nafasi mbalimbali ikiwamo Mwenyekiti wa UVCCM Taifa huku ukisisitiza kuwa uteuzi wa wagombea utazingatia umri.

Katibu Mkuu wa UVCCM, Kenani Kihongosi, akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo, alizitaja wilaya zilizofutiwa uchaguzi ni Mwanga, Mvomero na Singida Mjini kutokana na sababu mbalimbali, kubwa ikiwa ni wagombea kuzidi umri.

"Uchaguzi kwenye hizi wilaya utafanyika baadaye ili kupata viongozi wanaokidhi sifa. Kati ya vitu tutakavyokwenda kusimamia kikamilifu ni suala la umri kwa wagombea.

"Kanuni inasema wazi ya Umoja wa Vijana mgombea anapaswa kuwa na umri usiozidi miaka 30. Kwa hiyo, kupitia kanuni hii wanajua nini wanapaswa kufanya, niombe vielelezo wanavyotakiwa kufika navyo waje navyo," alisema.

Kihongisi alisema wagombea watakaovunja kanuni za maadili watatolewa na kuondolewa sifa ya kuteuliwa na kuwataka wawe na utulivu hasa wakati wa usaili na vikao vinavyokuja vya ngazi ya juu.

"Mtu atakayekwenda kinyume cha kanuni, tamaduni na taratibu za chama watapoteza sifa, hawa waliotia nia wajue hakuna mtu mwenye mamlaka ya kuteua isipokuwa vikao vya chama na jumuiya zake.

"Asitokee mtu au kikundi cha watu kikajipa mamlaka ya kufanya kazi ya vikao nje ya utaratibu, watakuwa wamepoteza sifa ya kuteuliwa na vikao, Niwaombe wagombea wazingatie kanuni, miongozo na taratibu za chama, wasije kufanya vitu vinavyokiuka utaratibu," aliagiza.

Pia aliwataka wapambe wa wagombea wawe watulivu wakati wanasubiri vikao vya uteuzi wa majina.

"Kwa sasa tunapanga safu za uongozi kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu. Tunataka safu zitakazozivusha chama kwenye uchaguzi huo unaokuja ili CCM iendelee kuongoza serikali," alisema.

Kuhusu vikao vya mchujo, Kihongosi alisema wanachama wa UVCCM ambao wamechukua fomu nchi nzima ni 556,381 kuwania nafasi mbalimbali huku wanaowania nafasi za ngazi ya kitaifa ni wanachama 1,253.

"Vikao vya uchujaji vitaanza Oktoba 8 hadi 16 mwaka huu na vitafanyika Dodoma kuanzia saa mbili asubuhi, tutoe wito kwa wagombea mbalimbali ambao wamewania nafasi ngazi ya taifa, kipindi hicho ni cha usaili.

"Tutakwenda kufanya usaili kwa wanaowania nafasi ya Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, wajumbe wa Baraza Kuu, wajumbe wawakilishi wa jumuiya za chama, wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC)," alisema.

Kihongosi aliwataka kufika na cheti cha kuzaliwa, kadi ya uanachama, vyeti vya masomo na mafunzo na kadi ya kitambulisho cha taifa au namba ili kufanya uhakiki kwa wagombea hao.

Alionya watendaji wa UVCCM watakaobainika kupanga safu watachukuliwa hatua za kinidhamu kwa kuwa kanuni na miongozo ya chama inafahamika.

"Wajikite kusimamia kanuni, wasijikite kuwanadi au kuwabeba wagombea. Atakayebainika atachukuliwa hatua," Kihongosi alionya.

## Kizimbani kwa mashtaka kusafirisha dawa kulevya

**Na Grace Gurisha**

ALLY Mkwawa (33) amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya aina ya Heroine gramu 231.06.

Akisoma hati ya mashtaka mahakamani huko juzi, Wakili wa Serikali, Silvia Mitanto alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Yusto Ruboroga kuwa mshtakiwa anakabiliwa na shtaka moja la kusafirisha dawa za kulevya.

Alidai kuwa Juni Mosi, 2022 mshtakiwa alikutwa eneo la Ubungo Mawasiliano akisafirisha dawa za kulevya aina ya Heroine gramu 231.06 huku akijua ni kosa kisheria.

Mshtakiwa huyo hakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo ambapo upande wa mashtaka ulidai upelelezi haujakamilika.

Awali, mshtakiwa huyo alidai mahakamani kuwa shauri hilo siyo jipya na pia tayari alishaandika barua ya kumaliza kesi hiyo lakini haijajibiwa.

Baada ya Kwawa kudai hayo, Wakili Mitanto alidai tarehe ijayo watakuja na majibu kuhusiana na barua aliyoiandika, lakini pia alimweleza kuwa inawezekana hajajibiwa kwa sababu kiwango cha dawa ni kikubwa.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Oktoba 11, 2022 kwa ajili ya kutajwa na mshtakiwa alirudishwa rumande kwa kuwa shtaka hilo halina dhamana.

**Alidai kuwa Juni Mosi, 2022 mshtakiwa alikutwa eneo la Ubungo Mawasiliano akisafirisha dawa za kulevya aina ya Heroine gramu 231.06 huku akijua ni kosa kisheria.**



Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (EWURA), Prof. Mark Mwandosya (wa pili kushoto), akiangalia namna mradi wa uongezaji mfumo wa gesi asili kwenye magari unavyofanyika, alipotembelea taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Prof. Preksedis Marco Ndomba. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## TCU: Nafasi 62,000 zipo wazi vyuo vikuu

**Romana Mallya**

TUME ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) imetangaza kuongeza muda wa udahili kwa kufungua awamu ya nne huku ikiwataka waombaji kutumia fursa hiyo ili kujaza nafasi 62,150 zilizobaki kati ya 172,868 za wadahiliwa wa mwaka huu wa masomo.

Mkurugenzi wa Uratibu wa Udahili na Menejimenti ya Data TCU, Dk. Kokuberwa Katunzi-Mollel aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa Tume, Prof. Charles Kihampa.

Alisema kati ya nafasi za udahili 172,868 za mwaka huu, mpaka sasa kupitia madirisha matatu ya udahili yaliyofanyika, waliodahiliwa ni 110,608 na nafasi zilizobaki ni 62,150.

"Udahili katika awamu zote tatu kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo 2022/23, umekamilika kwa mujibu wa ratiba ya udahili, majina ya waliodahiliwa katika awamu ya tatu unatangazwa na vyuo husika," alisema.

Alisema waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja katika awamu ya tatu na wale ambao hawakuthibitisha udahili katika awamu zilizopita, wanahimizwa kuthibitisha udahili wao katika chuo kimojawapo kuanzia jana hadi Oktoba 24 mwaka huu.

Pia alisema kuwa baada ya kukamilika awamu zote tatu za udahili, wamepokea maombi ya kuongezwa muda wa kutuma maombi kutoka kwa baadhi ya waombaji ambao hawakufanikiwa kupata udahili katika awamu zote zilizopita na vyuo vyenye nafasi navyo vimeomba hilo.

"Tume imeongeza muda wa udahili kwa kufungua dirisha la nne na la mwisho linaloanza Oktoba 4 hadi Oktoba 7 mwaka huu, waombaji ambao hawakutuma maombi ya udahili au hawakufanikiwa kudahiliwa katika awamu zilizopita, watumie fursa hii kwa kutuma kwa usahilhi maombi yao kwenye vyuo wanavyovipenda, taasisi za elimu ya juu zinazofanya udahili zitangaze programu zake ambazo zipo wazi," alisema.

Aliongeza kuwa kwa siku mbili kuanzia Oktoba 11 mwaka huu, vyuo vitawasilisha TCU majina ya waliodahiliwa na siku tatu baadaye vyuo vitatangaza majina ya waliodahiliwa awamu ya nne.

Alisema kuwa Oktoba 15 mwaka huu hadi Oktoba 24 mwaka huu, itakuwa ni nafasi ya kuthibitisha udahili kwa waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja kwa awamu ya nne na walioshindwa kuthibitisha awamu zilizopita.

# Mahakama Kuu yabariki kifungo miaka 30 gerezani

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Mtwara imembariki mrufani Musa Omary, kutumikia adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela kwa kubaka na kumpa ujauzito mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kitandi wilayani Ruangwa.

Uamuzi wa mahakama hiyo ulitolewa jana mbele ya Jaji Dk. Eliamani Laltaika, baada ya kusikiliza hoja nne za rufani zilizowasilishwa kupinga kutiwa hatiani na adhabu aliyopewa.

Mrufani alishtakiwa na kutiwa hatiani katika Mahakama ya Wilaya ya Ruangwa kwa mashtaka mawili ya kubaka na kumpa ujauzito mwanafunzi.

Ilidaiwa Julai 3, 2021 katika Kijiji cha Kitandi, Ruangwa mkoani Lindi, mrufani alimnajisi mwanafunzi wa miaka 14 wa Shule ya Msingi Kitandi na kumpa ujauzito.

Omary, alikana mashtaka huku upande wa mashtaka ukipeleka mashahidi sita na vielelezo mbalimbali na baada ya usikilizwaji, mrufani alitiwa hatiani na kuhukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 jela.

Baada ya kutiwa hatiani, alipinga adhabu na kuwasilisha rufani akiwa na sababu nne ikiwamo mahakama kukosea kumtia hatiani na kumpa adhabu kwa kuegemea ushahidi wa upande wa mashtaka ambao una shaka nyingi.

Sababu nyingine alidai mahakama ilikosea kumtia hatiani kwa ushahidi wa kwanza kwa kuwa eneo linalodaiwa kutokea tukio halikuwa na viashiria vya utendekaji wa kosa hilo la kunajisi.

Mrufani alijiwakilisha mwenyewe mahakamani wakati Jamhuri iliwakilishwa na Wakili Enoshi Kigoria.

Wakili Kigori, akiwasilisha hoja, alidai mrufani analalamika kwamba daktari aliyefanya uchunguzi alishindwa kutaja jina la mwathirika mahakamani.

Akijibu hoja hiyo, alidai hoja haina msingi na kwamba daktari wakati akiwasilisha mahakamani PF3, alisoma kwa sauti kielelezo hicho mahakamani na kilikuwa na jina la mwathirika.

Wakili alidai mrufani alishtakiwa kwa kumnajisi mtoto, kitu kinachotakiwa kuthibitishwa ni umri wa mtoto, ushahidi wa shahidi wa nne, umethibitisha umri wa mtoto na hata mwathirika alitaja umri wake.

Alidai, hoja kuhusu umri wa mtoto haina mashiko kwa kuwa haubishaniwi na aliomba hoja ya rufani itupwe kwa kuwa haina mashiko.

Mrufani, akijibu hoja hizo, alidai hakutenda hilo kosa Julai 3, 2021 saa saba kwa kuwa muda huo alikuwa anampeleka mama yake mwenye ulemavu katika sherehe za unyago wa jamii ya Wamwera.

Alidai kuwa, muda huo alikuwa na mama yake na mtoto wa marehemu dada yake, akidai mama yake alishapooza na alikuwa akihitaji msaada, hivyo alimpeleka kupata msaada kwa watu waliokuwa kwenye unyago.

Alidai kuna chuki kijijini dhidi ya familia yake na kwamba mama wa mwathirika alikwenda kununua eneo lakini familia yao ilikataa, hivyo kukawa na chuki.

Alidai mama huyo alifanya njama ili aende jela na kuchukua ardhi kwa urahisi, hivyo akaomba aachiwe huru arejee nyumbani kumsaidia mama yake.

Jaji katika uamuzi wake, alisema sababu zote za rufani hazina mashiko na hivyo zinatupwa.

"Rufani imekosa mashiko, mrufani ataendelea na hatia pamoja na adhabu aliyopewa na mahakama ya chini," alisema Jaji.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NCBA, Julius Konyani (katikati), akimlisha keki mmoja wa wateja wa benki hiyo, Seraphin Lusala, wakati wa sherehe ya wiki ya huduma kwa wateja, jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni mfanyakazi wa benki hiyo, Anna Shirima. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mabasi 170 kuongezwa mradi wa mwendokasi

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) umesema mabasi yaliyoko kwa sasa hayatoshelezi mahitaji ya usafiri huo wa umma na imejipanga kuongeza mengine 177 ili kuboresha huduma hiyo.

Ahadi hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa DART, Dk. Edwin Mhede, wakati wa kikao cha pamoja baina ya viongozi wa taasisi hiyo, wakuu wa wilaya na wakuu wa polisi katika wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam.

Alisema wakati wowote DART itatia saini mkataba na mzabuni na baada ya kutia saini, mabasi hayo yatawasili nchini ndani ya kipindi cha miezi sita ijayo na kuanza kutoa huduma kwenye sehemu zitakazobainishwa.

"Usanifu wa mradi wa mwendokasi wakati unaanza makadirio yalikuwa mabasi 305 na sasa tunayo mabasi 210. Yaliyopo hayatoshelezi mahitaji, ndiyo sababu tunatarajia kuongeza mengine 177 hivi karibuni," alisema

Dk. Mhede alisema kutokana na mahitaji ya watu, DART iliamua kupeleka huduma hiyo kutoka Muhimbili hadi Mloganzila ili watu wanaougua au kuuguza wafike kwenye hospitali hizo kwa urahisi.

Alisema DART iliamua kuitisha mkutano huo ili kuweka mikakati ya pamoja kuhakikisha kunakuwa na ulinzi na usalama wa kutosha kwenye matumizi ya miundombinu ya DART.

Alisema mahitaji ya usafiri huo yaliwalazimisha kupeleka usafiri huo Kibaha mkoani Pwani na kwa sasa wanatoa huduma kwa makundi maalum ya wazee na watu wenye ulemavu.

Alisema kwa sasa mabasi yao yanatoa huduma kwa watu 180,000 kwa siku lakini baada ya kuwasili kwa mabasi mengine idadi hiyo itaongezeka mara dufu na hivyo kupunguza muda wa msafiri kukaa kusubiri basi.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Heri James, alisema wamekubaliana kusimamia miundombinu ya DART na mabasi yake ili watumiaji wa usafiri huo wasipate shida.

# Wanaharakati wakutana kujadili usawa wa kijinsia

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

ZAIDI ya watu 600 wanatarajiwa kushiriki Tamasha la Jinsia Kanda ya Kaskazini lililoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kusherehekea mafanikio na kujadili namna bora ya kutumia fursa zilizoko na zinazoibuka za kiuchumi ili kuongeza ajira zenye staha na kuleta maisha endelevu.

Vilevile, TGNP imesema inaridhishwa na utendaji wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyotoa nafasi kwa wanawake kwenye uongozi, zikiwamo ambazo hazikuwahi kushikiliwa na kundi hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini Same, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, alisema tamasha hilo ni la 14 tangu lilipoanza mwaka 1996 kwa lengo la kuwaleta pamoja zaidi ya washiriki 25,000, asilimia 70 wakiwa ni wanawake.

Alisema TGNP kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wanaotetea haki za wanawake na usawa wa jinsia, wanaharakati binafsi na kwa ufadhili wa Ubalozi wa Watu wa Canada, Sweden, Coady Institute Canada na Seedchange, wameandaa tukio hilo muhimu ambalo pia litaonyesha fursa za kiuchumi kwa wanawake na jamii kwa ujumla.

"Tamasha la siku tatu litatoa fursa ya kutafakari na kutathmini changamoto zilizopo na namna ya kuweka mikakati ya kukabiliana nazo. Mgeni rasmi ni Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema jukwaa hilo ni la wazi kwa ajili ya wanawake na wadau wa haki za binadamu ambao hukutana pamoja kila baada ya mwaka mmoja kubadilishana uzoefu, kusherehekea, kutathmini na kupanga mipango ya kukabiliana na kero zinazowakabili.

Liundi alisema mada ndogo zitakazojadiliwa ni pamoja na haki za uchumi na kuwezesha fursa za kilimo kuwanufaisha makundi yaliyo pembezoni kwa maisha endelevu.

Nyingine ni uongozi shirikishi, chachu ya haki za kiuchumi na maendeleo endelevu, na mila kandamizi - kikwazo cha haki za uchumi kwa maendeleo endelevu.

"Tamasha hili litahusisha mawasilisho, mijadala ya pamoja, maonesho na warsha, mijadala ya pamoja kujenga dhana halisi kuhusu mada ndogo katika siku husika.

"Siku ya mwisho itahusisha kufunga kwa kuyaweka pamoja masuala yaliyoibuka katika mijadala mbalimbali siku zote tatu za tamasha," alisema.

Liundi alisema yatafanyika maonyesho kutoa nafasi kwa washirika na mitandao inayoshiriki kuonyesha kazi zao kupitia njia mbalimbali kama vile video, mabango, picha, wachapishaji, AZAKI na wanawake binafsi wanakaribishwa kuonyesha na kuuza bidhaa zao.

Kuhusu usawa kwenye ngazi za uamuzi, alisema Rais Samia ametengua utamaduni uliojengeka miaka mingi kwenye baadhi ya nafasi za uongozi akawaweka wanawake ambao wamefanya vizuri na tangu aingie madarakani suala la jinsia imekuwa kipaumbele chake.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Edward Mpogolo, akiwakaribisha TGNP, alisema wilaya hiyo ina watu zaidi ya 325,000 na kati yao, asilimia 52 ni wanawake wanaojishughulisha na kilimo na shughuli zingine za uzalishaji.

# Taasisi yajitosa kuokoa vijana ukatili kijinsia

**Na Allan Isack,** ARUMERU

BAADA ya kundi kubwa la wavulana kuingia katika mfululizo wa matishio ya matukio ya ukatili wa kijinsia, asasi moja ya kiraia katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, imelazimika kuanzisha Mradi wa Boy's Vac Lab unaolenga kuwatetea watoto hao.

Mradi huo unaofadhiliwa na Shirika la The Foundation for Civil Society (FCS), unatekelezwa na Shirika lisilo la kiserikali la CWCD katika shule sita zilizoko halmashauri hiyo.

Akizungumza jana, wakati wa kutambulisha mradi huo, Mkurugenzi wa CWDC, Hindu Mbwego, alisema wameanzisha mradi huo baada ya kusikia matukio mengi ya ulawiti kwa watoto wa kiume katika jamii.

"Utafiti unaonyesha kuwa matukio ya ulawiti kwa watoto wa kiume yameongezeka kwa kasi, hivyo tumeona kuna haja ya kuanza kuelekeza nguvu za kuwalinda watoto wa kiume, kama ilivyokuwa kwa watoto wa kike.

"Kwa kuwa wote wanahitaji ulinzi, naomba madiwani tuungane kupaza sauti, na niwatake wazazi na walezi kuwekeza nguvu kuwalinda watoto wa kiume."

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo ya Arusha, ambaye pia ni Diwani wa Laroi, Ojung'u Salekwa, alisema kumekuwapo na ongezeko la ulawiti kwa watoto wa kiume nchini, ulawiti ambao unafanywa na watu wa karibu nao hasa ndugu.

"Inasikitisha sana kuona matukio mengi yanayoripotiwa kwa sasa ni ya watoto wa kiume kulawitiwa na kulawitiana wenyewe kwa wenyewe, sisi kama viongozi kupitia mradi huu, tumejipanga kutumia majukwaa mbalimbali kuelimisha jamii dhidi ya madhara ya vitendo vya ulawiti kwa watoto wa kiume,"alisema Mwenyekiti Ojung'u.

Naye, Diwani wa Kata ya Kiranyi, John Seneu, aliwasihi wananchi katika eneo hilo kufungua macho ili kupambana na matukio hayo na kuungana kwa pamoja kupambana nayo, kwa kuwa yanaanzia nyumbani, shuleni, kanisani na sokoni.

**Kwa kuwa wote wanahitaji ulinzi, naomba madiwani tuungane kupaza sauti, na niwatake wazazi na walezi kuwekeza nguvu kuwalinda watoto wa kiume.**

# Wazee wadai kukosa fursa kujikimu kimaisha

**Novatus Makunga,** ARUSHA

CHAMA wa Wazee Wanaume Tanzania (CCWWT), kimeeleza kuwa kundi hilo kwa sasa, linakabiliwa na tatizo kubwa la kukosa fursa za kiuchumi, ambazo kama zingeelekezwa kwao, zingewawezesha kujikimu kimaisha na kutokuwa tegemezi kwenye familia.

Kutokana na kushindwa kufikia fursa hizo, wazee hao wanadai hiyo ni moja ya sababu kuu ya wengi wao kufariki dunia kabla ya wake zao.

Akizungumzia tatizo hilo jana, Kiongozi Mkuu wa CCWWT, Tade Mcheni alisema: "Kwa mfano katika sera ya mikopo ya uwezeshaji kiuchumi makundi maalum inayotolewa na Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, wazee hawana nafasi.

"Sasa utaona namna kundi hilo limekuwa likikosa fursa ya mikopo isiyokuwa na riba inayotolewa na serikali, ikiwa inawalenga pekee wanawake, vijana na jamii ya watu wenye ulemavu."

Mcheni, alieleza masikitiko yao jana, baada ya viongozi wakuu wa chama hicho chenye matawi katika mikoa 20 ya Tanzania Bara, waliokutana na Wanahabari kueleza mwelekeo wa chama hicho katika kipindi cha mwaka mmoja tangu kisajiliwe rasmi.

Chama hicho ambacho kinawajumuisha wanaume wenye umri wa kuanzia miaka 50 kilisajiliwa rasmi mwezi Novemba, mwaka jana.

"Kiujumla ukifuatilia kwa kina utabaini kuwa sehemu kubwa la kundi hili ndilo linalohudumia familia,lakini cha ajabu limekuwa likiwekwa kando katika kujumuishwa kwenye fursa za kiuchumi ambazo zinanafasi kubwa za kuwakwamua kimaisha,"alisisitiza.

Alisema, kuwa idadi kubwa ya wanaume wenye umri wa kuanzia miaka hamsini na kuendelea walikuwa wanajishughulisha katika kilimo,ufugaji na uvuvi huku idadi ndogo tu ndiyo walikuwa katika ajira rasmi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CCWWT, Joseph Laizer, alisema chama hicho kimejipanga pia kulipigania kundi hilo kupata huduma zikiwamo za matibabu.

"Tunakwenda zahanati, vituo vya afya au hospitalini, lakini mara nyingi tunakosa faragha kwa kuhudumiwa na mabinti zetu na hivyo wengi hurejea nyumbani na matatizo yao kwa kushindwa kuyaeleza ama kuhudumiwa," alisema.

Laizer, pia alieleza kuwa malengo mengine ya chama hicho ni pamoja na kuendesha kampeni ya kurejesha maadili katika jamii kwa kupambana na vitendo vya ubakaji na mauaji pamoja na kuibuka kwa makundi hatarishi ya kihalifu aliyoyataja kuwa ni Panyaroad kwa mkoa wa Dar es Salaam na Tatu Mzuka kwa Mkoa wa Arusha.

"Suala la maadili haliishii kwa vijana tu hata baadhi ya wazee wenzetu wamekuwa wakishiriki yakiwamo matukio ya kuwabaka wajukuu na katika hili tutahakikisha tunafanya udhibiti na kukemea vikali," alisema.

Katika hatua nyingine, Katibu Mwenezi wa Chama hicho, Claude Bernadict, alisema kuwa wamewaengua viongozi watatu katika uongozi kwa kushindwa kuwajibika akiwamo aliyekuwa Makamu Mwenyekiti, Gray Misolo, Katibu Mkuu, Cozy Zan na Ofisa Miradi Mkoa wa Arusha, Haruna Iddi

**Suala la maadili haliishii kwa vijana tu hata baadhi ya wazee wenzetu wamekuwa wakishiriki yakiwamo matukio ya kuwabaka wajukuu na katika hili tutahakikisha tunafanya udhibiti na kukemea vikali.**



Baadhi ya wanawake wa jamii za wafugaji wa kata ya Makuyuni, wilayani Monduli, mkoa wa Arusha, wakichangamkia fursa kwa kuwauzia watalii bidhaa wanazotengeneza yakiwemo mapambo, katika njia panda ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Manyara, hivi karibuni. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# Mdogo wa bilionea madini achaguliwa M/kiti CCM

**Na Jaliwason Jasson,** SIMANJIRO

KIRIA Laizer, mdogo wake na bilionea wa madini ya tanzanite, Saniniu Laizer, amechaguliwa kuwa Mwenyekiti mpya wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara.

Akitangaza matokeo hayo jana, Msimamizi wa uchaguzi huo ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Sezaria Makota, alisema Kiria aliibuka kidedea kwa kupata kura 315.

Mwenyekiti huyo, alimshinda mpinzani wake wa karibu, Anna Shinini, aliyepata kura 205 na Haiyo Mamasita aliyeambulia kura 34. Kwa mujibu wa Makota, kura zilizopigwa katika mkutano huo wa uchaguzi ni 560 na zilizoharibika ni sita, wakati halali ni 554.

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi, Kiria, alisema atahakikisha Simanjiro inakuwa moja na kazi yake ya kwanza anayoanza nayo ni kuvunja makundi.

"Kipaumbele changu itakuwa siasa ya uchumi na kuhakikisha tunapiga hatua wote kwa pamoja," alisema Laizer.

Baada ya uchaguzi huo, Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alisema ana imani kubwa na Mwenyekiti huyo, kwa kuwa ni muumini wa haki na hapendi kuyumbishwa na wala sio mtu wa makundi.

Vilevile, mkutano huo ulimchagua, Mosses Makeseni kuwa Katibu mpya wa Siasa na Uenezi Wilayani humo, baada ya kushinda nafasi hiyo kwa kura 61, dhidi ya mpinzani wake, Papai Njiday, aliyepata kura 25.

# Serikali kufuatilia mfumo utoaji mikopo wanafunzi

Na Godfrey Mushi, ROMBO

SERIKALI inaendelea kufanya uchunguzi kuhusu mfumo wa utoaji mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu nchini, kwa kipindi cha miaka mitano ili kubaini kama kulikuwa na udanganyifu kwa kuwapa wasiokuwa na sifa na vigezo vilivyowekwa.

**Lengo la serikali ni kuimarisha utoaji wa mikopo na kuwanufaisha wanafunzi wengi wenye sifa za kupewa mikopo.**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alidokeza hilo juzi, alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Maki kilichoko Wilaya ya Rombo, mkoani Kilimanjaro.

Prof. Mkenda, ambaye pia ni Mbunge wa Rombo (CCM), alizungumzia uchunguzi huo alipohudhuria mahafali ya Shule ya Sekondari ya Maki ikiwa ni sehemu ya ziara yake ya siku tatu katika wilaya hiyo.

"Serikali inaendelea kupitia (kufanya uchunguzi) mfumo wa utoaji mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kwa kipindi cha miaka mitano ili kubaini kama kulikuwa na udanganyifu au utoaji mikopo kwa wanafunzi wasiokuwa na sifa na vigezo vilivyowekwa," alisema.

Kwa mujibu wa Prof. Mkenda, lengo la serikali ni kuimarisha utoaji wa mikopo na kuwanufaisha wanafunzi wengi wenye sifa za kupewa mikopo.

Katika hatua nyingine, alisema wizara yake inatambua muktadha wa Rais, Samia Suluhu Hassan, katika kuendeleza sekta ya elimu na lengo la kuja na Samia Scholarship ni kutokana na uamuzi wake wa dhati wa kukubali kutoa ufadhili kwa wanafunzi 640 nchini.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ilianzisha programu ya ufadhili wa masomo iitwayo Samia Scholarship, kwa masomo ya shahada ya kwanza kwa wanafunzi waliopata ufaulu wa juu katika mitihani ya kidato cha sita mwaka 2022.

Mitihani hiyo iliyoendeshwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) katika tahasusi za Sayansi za PCB, PCM, PGM, CBG, CBA, PMC na CBN).

Kwa mujibu wa Waziri Mkenda, Samia Scholarship itagharamia kwa asilimia 100, masomo ya Chuo Kikuu kwa wanafunzi hao, ambao wamepata udahili katika fani za teknolojia, uhandisi, hisabati na tiba.



Meneja mradi wa kituo cha kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu CCBRT Moshi, Lucy Kavishe (wa tatu kulia), akisalimiana na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alipofika ofisini kwa mkuu huyo jana, akiwa na timu ya wazalishaji wa kipindi cha afya ya Jamii – ITV, katika maandalizi ya kuelekea kuadhimisha miaka 25 ya utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu, mkoani humo na maeneo ya jirani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NSSF kulipa stahiki wanachama saa 24

Na Oscar Assenga, TANGA

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii nchini (NSSF), umeahidi kulipa madai yote ambayo ni stahiki za wanachama wake katika muda usiozidi saa 24.

Jana, Meneja wa NSSF, Mkoa wa Tanga, Audrey Claudius, aliahidi hayo wakati wa ufunguzi wa wiki ya huduma kwa wateja.

"Katika wiki hii ya wateja, tutahakikisha wanachama wote wanaowadai watawalipwa ndani ya siku moja. Rai yangu kwa waajiri, watusaidie kulipa michango kwa kufuata mifumo na walipe kila mwezi.

"Lakini niwatake waajiri, kuacha kulimbikiza michango, kwa kuwa kufanya hivyo kunasababisha usumbufu kwa wanachama wanapokuja kwetu kufungua madai. Hivyo tuhakikishe tunalipa kwa wakati.

"Katika kuhakikisha kila Mtanzania ananufaika na hifadhi ya jamii, tumejipanga kuyafikia makundi mbalimbali katika Mkoa wa Tanga ili kuwapa elimu ya hifadhi ya jamii ili waweze kujiandikisha na kujenga utaratibu wa kujichangia kwa manufaa yao ya baadaye."

Awali, Ofisa Mkuu wa NSSF Tanga, Abubakari Mshangama, akizungumzia huduma hiyo, alisema katika wiki ya huduma kwa wateja, watatoa huduma mbalimbali ikiwamo ya mtandao, ambao utawawezesha wanachama kupata taarifa zao.

Mshangama alisema, kwa waajiri wanaweza kutumia member portal (mfumo wa kielektroniki) kuwasajili wanachama na kulipa michango yao.

Wiki ya wateja ya NSSF ni maalumu kwa ajili ya kutoa elimu zaidi kuhusu huduma hizo za kimtandao.

# Wakazi waituhumu serikali ya kijiji kuuza maeneo

Na Mwandishi Wetu, MOSHI

WAKAZI wa Kijiji cha Uchira, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, wameituhumu serikali ya kijiji hicho, kuuza maeneo ya hifadhi ya barabara kinyume cha sheria, huku wakijua wanasababisha bugudha kwa kaya ambazo hazina barabara za kuingia majumbani mwao.

Walitoa tuhuma hizo jana baada ya kukusanyika wakilalamikia moja ya sehemu ya barabara iliyouzwa bila kushirikishwa.

Baadhi ya wananchi hao, akiwamo Onesmo Mkojera na Victor Mlay, kwa nyakati tofauti walieleza kuwa kuuzwa kwa maeneo hayo ya hifadhi ya barabara kumewasababishia kukosa njia za kupitisha mazao yao, kuzifikia huduma za jamii kama masoko, zanahati na vituo vya afya.

Mlay alisema: "Viongozi wetu wa kijiji wanapaswa kujiweka kando na jambo hili kwa sasa. Kwanza ni lazima wayaepuke malalamiko na hasara itakayojitokeza.

Pia, wananchi wanaonunua maeneo haya hawanabudi kuheshimu sheria, ikiwamo kutojenga ndani ya hifadhi za barabara kama sheria inavyotaka."

Mkonjera alisema, kama serikali ya wilaya haitachukua hatua dhidi ya tuhuma hizo, wananchi watawawajibisha viongozi wao.

Alipotafutwa kujibu malalamiko hayo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kijiji hicho, Sadick Mdee, alikanusha juu ya kuuzwa kwa maeneo hayo, akisema yanayozungumzwa hayana ukweli, kwa kuwa maeneo yaliyouzwa hayakuwa barabarani.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Abbas Kayanda, alipoulizwa kuhusu malalamiko hayo, alisema hana taarifa hiyo, lakini atakwenda katika kijiji husika kujua ukweli wa jambo hilo na kulitafutia ufumbuzi wa kudumu.

**Pia, wananchi wanaonunua maeneo haya hawanabudi kuheshimu sheria, ikiwamo kutojenga ndani ya hifadhi za barabara kama sheria inavyotaka.**




Ukurasa 15

**DOROTHY SEMU Makamu Mwenyekiti ACT Wazalendo anayelenga demokrasia imara vyama vingi**



Ukurasa 18

Unaibu,kurithi urais Afrika: Ni zama Wakenya kujifunza kilichotokea Afrika Kusini




**Burkina Faso hakukaliki mapinduzi kila kukicha**


# siasa

JUMATANO OKTOBA 5, 2022

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


MWALIMU JULIUS NYERERE 1922-1999

# Yafanyike mambo makubwa, tofauti kumuenzi

**Na Gaudensia Mngumi**

NI wakati wa kufanya mambo makubwa zaidi kuijenga Butiama kumuenzi Mwalimu Nyerere ambaye Oktoba 14 mwaka huu, taifa litakumbuka maisha na kifo cha muasisi wa Tanzania, ambaye licha ya kuondoka duniani, ameacha mafanikio kisiasa, kiuchumi , kijamii nje na ndani ya Tanzania.

Kijijini Butiama mkoani Mara ndipo alipozaliwa Aprili 1922, kadhalika eneo la Mwitongo kijijini hapo ni eneo lilipo kaburi lake, gwiji huyo na mwana mapinduzi wa Afrika aliyefariki Oktoba 14,1999 jijini London, anaheshimika kwa mengi zikiwamo fikra tunduizi -critically thinking alizoacha.

Marejeo na tafakari za maisha yake zinafanyika kila wakati akiwa ndiye aliyebuni na kutekeleza mikakati ya kuijenga Tanzania na kuipa taswira iliyonayo leo, kuanzia viwanda, mabwawa makubwa ya maji kama Mtera , Kidatu, Hale ili kuzalisha umeme, lakini pia kuweka vyuo vikuu - Dar es Salaam, Sokoine na kuanzisha vituo mbalimbali vya huduma zikiwamo kampuni za simu, mashirika kama la Ndege ATC au Air Tanzania Corporation.

Ndiyo maana wakati umefika Watanzania kuiweka Butiama kwenye ramani ya dunia, kama yeye alivyoliweka taifa hili likajulikana duniani kote, pengine kwa kuanzisha mkakati wa kitaifa wa kuijenga Butiama ya Nyerere.

Mwalimu Nyerere ndiye aliyebuni na kuuweka mweleko wa Tanzania lakini, kama ambavyo wengi wangedhani hakuijenga Butiama alipozaliwa na kupaandaa kwa kuweka barabara za kisasa, vivutio kama hoteli, viwanja vya ndege au mambo mengine makubwa ambayo baadhi ya viongozi wa Afrika wanafanya katika miji walikozaliwa.

Katika moja ya mahojiano yaliyofanywa na wakazi wa Mara, wanadokeza kuwa kuna wakati Baba Taifa aliulizwa na watu wa mkoa huo kuwa amekuwa Rais wa Tanzania kwa miaka mingi na kutakiwa aeleze watu wake amewafanyia nini?

Inasemekana jibu lake likawa "mimi si rais wa mkoa wa Mara, bali nchi yote inanitegemea na inanitazama." Ikaelezwa kuwa na huo ukawa mwisho wa kudai upendeleo.

Kwa kuwa Nyerere alijijenga Tanzania ni zamu ya Watanzania kuijenga Butiama kwa kuipa sura na hadhi ya kumuenzi Nyerere na jamii iliyomuandaa hadi akawa kiongozi bora.

Kazi ianze kwa kuanzisha mfuko wa kuijenga Butiama ili hata miaka 1,000 ijayo vizazi vyake vione na kufahamu kazi za mwasisi wa taifa lao kwa kutembelea makazi yake, maktaba zake, kaburi na makumbusho yake lakini pamoja na kuweka vitega uchumi vitakavyoivutia



dunia kumtafuta, kumjua na kumfurahia zaidi.

Ni wakati wa kuhimiza wawekezaji wa nje na ndani kuwekeza katika wilaya Butiama, kuing'arisha zaidi na kuweka vitu ambavyo havipatikani popote duniani.

Pengine mojawapo ni kuwa na bustani , majumba na maeneo yenye vitu vinavyopatikana Tanzania pekee , kwa mfano 'tanzanite' ambayo duniani kote iko Mererani pekee mkoani Manyara.

Ripoti ya utafiti ya 'Gem Wealth of Tanzania' iliyochapishwa na wanajilojia kadhaa akiwamo Dona Dirlarn na Elise Misiorowski, inaitaja Tanzania kuwa na hazina ya vito vya thamani ambavyo havipatikani sehemu nyingi duniani kwa mfano 'kito spinel' ambayo kwa Afrika inapatikana Tanzania, liko 'jiwe zircon ruby' tena ikitajwa kuwa ni jamii ya rubi ya kipekee na nyororo na inayong'aa sana.



Tanzania itumie vivutio vya kipekee kama wanyama, madini na mimea kuvutia watu wengi duniani kama njia ya kumtangaza Mwalimu Nyerere. **PICHA: MTANDAO**

Kwa Afrika nzima ni Tanzania yenye vito mujarabu vya ' fancycolored sapphire', mataifa vinakopatikana ni Sir Lanka, Burma na Madagascar lakini kwa kumuenzi Mwalimu mtalii au mwanafunzi wa jiolojia kutoka ughaibuni anaweza kusafiri hadi kijijini Butiama kuiona 'green grossular garnet' au ' tsavorite kwa vile iligundulika eneo la Tsavo.

Vyote hivyo vijengewe maeneo maalumu ya namna ya miamba na majabali vinakochimbo huko Butiama kumuenzi Nyerere.

Inawezekana pia kuweka bustani za maua yanayopatikana nchini tu na si kwingineko duniani kwa mfano ua 'Saintpaulia' lenye gharama kubwa zaidi duniani na uzuri wa kipekee linaloota


**INAENDELEA UK. 20**

# Wachambuzi watafuta vyanzo mabadiliko ya baraza mawaziri

• Maelezo ya Rais yatumiwa kukoleza vianzio



Waziri Dk. Stergomena Tax, akila kiapo Jumatatu Ikulu. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

**Na Ani Jozeni**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amefanya mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri na kikubwa ni kuondolewa Balozi Liberata Mulamula Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Kazi yake ikachukuliwa na Dk. Stergomena Tax, aliyehama kutoka Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, na huko akaenda Innocent Bashungwa, aliyekuwa Ofisi ya Rais TAMISEMI. Ofisi hiyo inayoshughulika na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, akapelekwa, Angella Kairuki.

Ni mabadiliko ambayo Rais aliyaelezea kwa kirefu na kwa maana hiyo yako makosa yaliyofikia kuondolewa katika nafasi hiyo Balozi Mulamula, ila labda si jambo la kushangaza kwani ni mjuzi wa diplomasia katika ngazi ya uwakilishi wa nchi na kutetea maslahi yake, si kudhihirisha au kusadikisha mwelekeo na sura ya serikali siku hadi siku.

Kuna mitego mingi kama alivyosema Rais, kwa mfano jinsi waziri anavyohitaji kujua kuwa ziko pande mbili za Muungano katika kufanya kazi yake. Ila kwa vile hakufafanua, si ajabu suala siyo hilo.

Anataja pia kutunza siri za serikali tena kwa pande zote mbili, suala ambalo linaleta mtego wa aina nyingine, kuondoka katika utetezi wa maamuzi ya serikali kama mshiriki wa kuyafikia na kutoa siri za upande huu au ule wa Muungano. Kimsingi maelezo ya Rais Samia kuhusu mapungufu kiutendaji yaliyoleta mabadiliko barazani hayatoi picha halisi ya jambo lenyewe, katika kugusia mipaka ya kazi za mawaziri, ambayo pia ni mapana ya uwajibikaji.

Ni hoja ya kuangalia nini kilitokea tangu Machi 2021 Balozi Mulamula alipoteuliwa katika nafasi hiyo na kilichojiri.

> Yako maeneo mengine ambako ipo mijadala na hayana majawabu sahihi, kwa mfano suala la uraia wa nchi mbili kwa Watanzania ambao tayari wamepata uraia wa nchi nyingine.



Balozi Liberata MulaMula; ameondoka kwenye uwaziri.

Kuna kanuni ya kisaikolojia kuwa kumwelewa mtu alivyo, sikiliza kile anachoongea na kukitazama kwa karibu, usingoje kuambiwa siri hii au ile inayomhusu.

Kutosikiliza siri katika masuala kama haya ni muhimu kwa sababu ni suala lisilo na athari zozote kwa umma au vyombo vya dola nje ya kundi la watu wachache, na hivyo si lazima kubadili serikali kwa ajili ya suala kama hilo. Isitoshe, kila siku kuna hiki au kile kinavujа katika idara tofauti za serikali au mamlaka za uendeshaji uchumi.

Ina maana kuwa kuelewa kilichotokea inatosha tu kuangalia mwenendo wa jumla wa mawaziri hao ukilinganisha na mwelekeo kimawazo au kisera wa Rais Samia, halafu kwa kuchora 'grafu' au jedwali ' hiyo inafika mahali watofautiane waziwazi.

Isitoshe, tofauti hizo si za watu binafsi ila ni mielekeo ya kitaasisi ambako wahusika wana makundi makubwa ya watu nyuma yao, ambao wanafuatilia wanachotenda, si kwa kufahamishwa ila kwa kuendana kihisia. Ukienda kwa mtazamo huo wa mwelekeo wa kisera au kimawazo ambao una idadi kubwa ya wafuasi kitaasisi na kwa maana hiyo kisiasa, unaanza kupata picha nini kinahusika, na mabadiliko hayo hasa yanalenga nini.

Inasaidia zaidi pale unapolinganisha mtazamo wa wazi wa aliyeondoka na anayechukua nafasi yake, kuwa ni taswira gani kisiasa au kijamii ambayo huyu au yule anawakilisha. Bila shaka, kwa mtazamo wa awali wa kihisia, utakuwa katika nafasi nzuri ya kuelewa tofauti hizo, kwani kinachojiri ni kuwa kwa watu waliochukua nafasi zao wakati mmoja, mwelekeo wa mmoja wao ulikuwa unaendana kukinzana na ule wa Rais.

Mwelekeo wa huyu wa pili unaendana kabisa na ule wa Rais, hivyo anapewa kazi ya kumwakilisha kwa karibu zaidi, halafu kwa vigezo tofauti vya kitaasisi, mwingine anapewe nafasi iliyoachwa na huyu wa pili, na hapa wa ziada ni Waziri Bashungwa.

Kwa kifupi ndicho inachoelekea kimetokea, kuwa kuna maeneo ya ukakasi kihisia kati ya Balozi Mulamula na Rais Samia ambayo yalikuwa wazi tangu mwanzo, na msingi wake ni wa kitaasisi, siyo mgongano tu kwa hisia binafsi.

Rais Samia anawakilisha mtazamo wa utandawazi na uboreshaji wa kuhusika kwa Tanzania katika masuala nyeti ya ukanda huu, kwa mfano hatari ya ugaidi iliyoinuka Msumbiji, askari watoke nchi ndogo ya Rwanda iliyo mbali na Msumbiji, halafu Tanzania imekaa pembeni. Hakuna habari kuwa kutojihusisha kunatoa mwanya mpana kwa kundi hilo au lile la magaidi kujipanga, hata kisaikolojia ni kuwaunga mkono.

Mwelekeo huo wa kutojihusisha umeenea katika ngazi tofauti za kitaaluma na unaendana na kutotaka kusikia tena masuala ya 'kusaidia ukombozi Kusini mwa Afrika.

Ni kutoa sifa kwa ndimi za nje bila kuwa na suala hilo moyoni, kwani siyo kupambana na ukoloni mkongwe au ubaguzi wa rangi ambavyo peke yake ni sahihi kwa Tanzania kuhusika. Suala hilo ni kati ya uhafidhina wa kutotaka kuhusika na umaendeleo, ubinifu wa kusikiliza na kuchukua hatua kitaasisi, kuhusika kimataifa, kwa masuala hayo.

Kwa maana hiyo Waziri Stagomena ni muumini halisi wa sera za kusaidia kwa dhati haya mapambano dhidi ya ugaidi kama sehemu ya majukumu ya kitaifa. Siyo kungoja litengwe fungu la kulinda amani halafu ndipo watu waanze kwenda.

Yako maeneo mengine ambako ipo mijadala na hayana majawabu sahihi, kwa mfano suala la uraia wa nchi mbili kwa Watanzania ambao tayari wamepata uraia wa nchi nyingine.

Hapa kuna hoja ya uwakilishi wa kile ambacho serikali inasimamia kwa sasa, na inawezekana kukawa na tofauti za hapa na pale, zinazoweza kuchangia kwa mfano hatua za kinidhamu, kujitenga na uamuzi huu au ule badala ya kuutetea. Yapo vile vile masuala ya jinsi ya kuendesha mambo ya nje ndani ya mfumo wa Muungano, kuna mitego huko.

Ni katika eneo hilo la mambo ya nje, sera za kupambana na ugaidi halafu uraia wa nchi mbili, au lugha inayowakilisha Muungano ambako inawezekana mitego ilizidi uwazi wa nini kinahusika. Ni sehemu ya kujifunza serikalini kuhusu suala hilo, kwani sasa itaeleweka kwa watendaji wizarani nini lugha sahihi katika suala hili au lile, halafu nini mwelekeo wa serikali kwa jambo hilo. Mijadala ya kihisia ni kama inafunikwa, suala hilo limalizike kwa utawala uliopo ujifafanue kwa hilo.

DOROTHY SEMU

# Makamu Mwenyekiti ACT-Wazalendo aanika amelenga demokrasia imara ya vyama vingi

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha ACT--Wazalendo kinaendesha operesheni ya 'Tume Huru ya Uchaguzi Kuelekea Katiba Mpya', inayolenga Tanzania kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi inayofanyakazi mwaka 2024 kwenye kuchagua viongozi wa serikali za mitaa na ule mkuu wa 2025.

Wanachofanya ni kuona kila mwanachama, kiongozi na wananchi wanaelimishwa kwamba mazingira ya kisiasa na ya sasa yanapaswa kuipata tume huru ya uchaguzi wanapoelekea kupata katiba mpya yenye maoni ya wananchi.

Dorothy Semu Makamu Mwenyekiti ACT-Wazalendo Bara, anazungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, akifafanua mikakati mbalimbali ya chama na yenye lengo la kujiimarisha

"Chama chetu kinapendekeza kuwa na tume ya uchaguzi, mageuzi ya jeshi la polisi, katiba mpya na kuandikwa upya kwa sheria ya vyama vya siasa ni masuala makubwa ya kufanyiwa kazi, ili kutekeleza azma ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kufungua ukurasa mpya wa kisiasa nchini," anasema Semu.

Mwanasiasa huyo anasema ACT Wazalendo inaendelea kusimamia hoja hizo nne, ili kuhakikisha kwamba zinatekelezwa na kwamba ndio maana imekuja na operesheni hiyo kwa kuwa ina mambo ya msingi.

Anasema hatua hiyo pia itasaidia kuandaa na kusimamia uchaguzi mkuu 2025 iwapo utafanyika kabla ya kupatikana kwa katiba mpya, kusimamia kura ya maoni ya katiba mpya ambayo ACT Wazalendo hawaafiki kusimamiwa na tume ya uchaguzi iliopo. ambapo pia anajibu maswali yafuatayo:

**SWALI:** Ukiondoa malalamiko ya kudai kàtiba na tume huru ya uchaguzi, hali ya siasa ikoje nchini na ndani ya chama chenu inaendeleaje?

**JIBU:** Suala la tume huru ya uchaguzi, maboresho ya sheria za uchaguzi, vyama vya siasa, sheria ya jeshi la polisi tunalipa umuhimu wa kipekee kwa vile ni sehemu ya ujenzi wa demokrasia ya vyama vingi tulioichagua kuiendea kama taifa. Demokrasia inahitaji misingi, kukuzwa na kuendelezwa na hivyo kuwekewa sheria wezeshi ambazo zitaboresha katika kuweka uwanja sawa wa kutekeleza siasa za vyama vingi nchini. Tunaona utashi wa kuyaendea maboresho haya, lakini tunashauku ya kuona utashi huu ukitimilika kwa kuuwekea misingi ya kikatiba, sheria na kanuni ambayo sote kama nchi tutaifuata. Kama chama Tunaendelea na majukumu yetu ya msingi kama cha siasa makini, na pia na kujipanga na kutekeleza ujenzi wa chama cha kisasa cha siasa kilichojikita kwenye mioyo ya Watanzania kwa kuja na sera bora zitakazowezesha kuendeleza ujenzi wa taifa bora. Pia kuendelea na kazi ya kuisimamia serikali ya iliopo na kutoa suluhisho kwa masuala yanayosibu wananchi wetu.




Makamu Mwenyekiti, Dorothy Semu, akiwa na Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu. **PICHA: SABATO KASIKA**

> "Chama chetu kinapendekeza kuwa na tume ya uchaguzi, mageuzi ya jeshi la polisi, katiba mpya na kuandikwa upya kwa sheria ya vyama vya siasa ni masuala makubwa ya kufanyiwa kazi, ili kutekeleza azma ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kufungua ukurasa mpya wa kisiasa nchini," anasema Semu.

**SWALI:** Kila mara serikali inapofanya uamuzi wa jambo fulani, nyie huwa mko mstari wa mbele kutoa tamko, tofauti na vyama vingine vya upinzani, matokeo ya matamko yenu yakoje?

**JIBU:** ACT Wazalendo ni chama cha siasa ambacho kinawajibika kutekeleza jukumu lake la msingi kama chama cha siasa makini kwenye kuisimamia serikali, kukosoa na kutoa masuluhisho mbadala kwa kuboresha sera, kutoa matamko na kuibua changamoto mbalimbali zinazikabili jamii ya Kitanzania. Tunajivunia kazi yetu kwa kuwa mara nyingi serikali imesikia na kujibu. Au kwa kukanusha suala, kuboresha na kutatua changamoto au kero husika. Tunaona hili ni muhimu kwetu, kwani tunatimiza jukumu letu la msingi na jamii yetu inanufaika. Tumechagua njia hii kwa sasa na tunaendelea kuboresha mbinu za kuibana kuikosoa na kutoa masuluhisho kwa serikali.

**SWALI:** Baadhi ya vyama vina migogoro ya ndani na ikumbukwe kuwa kuna msemo kwamba 'ukiona mwenzio ananyolewa na wewe tia maji'. Nyie mmejiandaaje kuepuka migogoro kama hiyo. Lakini pia uchaguzi unakuja mmejiandaaje?

**JIBU:** Ni kweli migogoro ilikuwepo na imekuwepo ndani ya baadhi vyama vya siasa. Changamoto hii imeshuhudiwa katika miaka 30 ya vyama vingi na imekuwa ikijirudua na hatujaweza kujiwekea mifumo rahisi ya kuielewa, kuitatua na kujikinga nayo. Kwa kweli ina madhara makubwa na inaharibu ukuaji na kushamiri kwa vyama vya siasa. Ni muhimu kama taifa na tulioamua kuwa na demokrasia ya vyama vingi kuja na namna bora ya kuviwezesha vyama vya siasa kuwa na mifumo imara ya kuizuia, kuigundua, kuitatua migogoro kwa wakati isiwe makaburi ya vyama vya siasa. Lakini kipekee, sisi ACT Wazalendo tunaendeleza utamaduni bora wa kufuata katiba yetu kama mwongozo wa uendeshaji wa chama.

Pia katiba yetu imeweka kamati ya maadili kutoka ngazi ya msingi, ambazo zina wajibu wa kupokea, kuchunguza mashtaka na kutoa masuluhisho ya migogoro ya ndani ya chama. Ni kazi endelevu ambayo inawezesha chama kuwa na jicho lake pale mipishano inapotokea kati yetu. Tunaendelea kujenga na kuboresha utamaduni wa kukaa na kutatua changamoto za migongano pale inapotokea kwa uwazi na haki. Kuhusu uchaguzi unaokuja, tumejianda kikamilifu kwa uchaguzi za serikali za mitaa na uchaguzi mkuu. Ninaamini tutafanya vizuri.

**SWALI**: Chama chenu kwa upande wa Zanzibar ndicho kimechukua nguvu za CUF. Nini dira ya kurejesha heshima na nguvu hasa Pemba?

**JIBU:** Pemba ni moja ya maeneo ambayo chama chetu kipo imara katika hali zote. Heshima ya ACT Wazalendo haijawahi na haitawahi kupungua katika siasa za Pemba. Tunaendelea kuwa imara.

**SWALI:** Nguzo kuu za kisiasa za chama ni vijana, wanawake na wazee. Kwa vile hivi karibuni Siku ya Wazee mlitoa kauli, je, mnaimarishaje makundi hayo? Je, mna matawi yao wapi, kwa kiasi gani, kuna changamoto?

JIBU: Makundi haya ya kinamama, vijana na wazee, sisi katika kueneza sera za chama, tuna tuna idara hizi na tunazoziita ngome ambazo zina uongozi kuanzia ngazi ya tawi hadi taifa. Hii ni mihimili muhimu katika ujenzi wa chama, ndizo zinazofanya kazi muhimu ya ushawishi wa wananchi kujiunga na chama. Ngome zetu zinaendelea kuimarika na kutimiza wajibu wake wa msingi kichama. Changamoto moja kuu ni hali ya kudumazwa kwa ushiriki wa kikamilifu wa wananchi katika siasa, hivyo kushuka ari ya wao kuwa sehemu ya vyama vya siasa.

**SWALI:** Siasa ni uwekezeji kifedha na hata magari, chama chenu kimejipangaje?

**JIBU:** Chama cha siasa kina-

**INAENDELEA UK. 17**

## MAMA ANNA HENGA, MKURUGENZI MTENDAJI LHRC;

# Mhamasishaji katiba anayejivunia kuwapo usawa kijinsia kazini kwake

**Na Elizabeth Zaya**

ANNA Henga ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu(LHRC), cha Dar es Salaam, anayesema kabla ya kuwa kiongozi katika nafasi hiyo ya juu, nyota yake ilianza kung`aa tangu akiwa mdogo na kwamba kabla ya kufikia ukurugenzi alianzia kuongoza wenzake msingi na sekondari.

Mbali na kuwa kiranja, ameongoza bendi ya shule na pia katika vikundi mbalimbali vidogo vya shule ya msingi na sekondari hata kanisani nako yumo akishika nyadhifa nyingi kama uongozi wa vijana.

"Kwa hiyo nilikuwa kiongozi kwenye vikundi hivyo vya chini kwenye nafasi ya katibu ambayo ilikuwa inanifanya kuwa mtendaji zaidi,"anasema Henga.

Anazungumzia kujiunga na LHRC, akisema alijiunga kituo hicho kwa ajili ya mafunzo baada ya kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alipohitimu shahada ya sheria, akifanya kazi ya ofisa wa chini wa masuala ya sheria.

Baadaye, anasema anajiriwa na kupewa nafasi ya kuratibu masuala ya katiba ndani ya kituo hicho na baadaye Mkurugenzi wa Utetezi na Maboresho, nafasi aliyoitumikia hadi alipoteuliwa kushika wadhifa alio nao sasa.

"Nafasi hizi siyo tu kwamba zimekuja kwa bahati au zimetokana na kupendelewa hapana, zote zilikuwa ni za juhudi. Mfano hiyo ya Mkurugenzi wa Idara, nilipata kwa sababu nilifanya kazi kubwa sana ya katiba mwaka 2012 hadi 2013 wakati mchakato wa Katiba ya Warioba unafanyiwa kazi. Nilizunguka Tanzania karibu yote na nilikuwa ni timu naiongoza peke yangu,"anakumbusha Anna.

"Nilifanya kazi kubwa sana ya kuwafundisha watu kuhusu katiba na walijitokeza kwa wingi kushiriki kwenye mchakato na katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 baada ya kuelewa umuhimu wa haki yao ya kuchagua na kuchaguliwa. Kwa hiyo kupitia jukumu hilo hata shirika lilipata sifa kubwa kwa hiyo ndiyo maana nikapata cheo hicho cha ukuu wa idara ambako sikukaa muda mrefu nikateuliwa Mkurugenzi Mtendaji."

"Na yenyewe siyo kwamba nilipandishwa cheo tu, hii ilikuwa na mahojiano magumu na watu ambao hawanijui, na tulikuwa na wengi tuliotuma maombi tulioshindanishwa na nikafanikiwa kupita. Anasema na kuongeza kuwa katika nafasi hizo amekuwa akikutana na changamoto mbalimbali lakini kama kiongozi anatafuta namna bora ya kuzitatua .

**CHANGAMOTO ZIPO**

"Uongozi ni jambo zuri lakini pia una changamoto na mafanikio mengi. Changamoto kubwa ambazo nilishawahi kukutana nazo ni namna ambavyo watu wanachukulia masuala ya kazi. Kwamba wewe unaona kitu kina umuhimu lakini wenzako hawaoni hivyo, kwa hiyo inabidi uwasaidie waone au uongoze kwa mfano, yaani utangulie mbele na wenzako wakufuate, kiongozi ni mtu ambaye wenzake wanamfuata nyuma, siyo anawaambia wenzake tunakwenda kule mbele halafu anabaki nyuma," anasema Anna.

"Kwa hiyo ukifanikiwa kuwashawishi nao watakwenda huko ambako inatakiwa waelekee, unatakiwa kuona maono ya mbali halafu uwasaidie na wao wayaone ikiwamo wewe mwenyewe kuanza safari na siyo kwa kuwalazimisha." Anaongeza.

Changamoto nyingine aliyokutana nayo katika nafasi yake hiyo ni namna ya kuweka uwiano sawa wa matakwa au manufaa binafsi ya unaowaongoza, serikali, asasi za kiraia, mitandao, familia, wazazi, watoa uamuzi, vyombo vya dola wadau na wanachama.

"Na kuna wakati maslahi ya wadau yanagongana, mwingine anataka hiki, wengine kile, kwa hiyo inabidi uunyoshe mstari useme hapa tunakwenda hivi bila kuangalia upande mmoja au kumfurahia mmoja,"anasisitiza Henga.

Mfumo dume ni changamoto inayomtesa Anna anayefafanua."Watu wengi hawamuangalii mwanamke kama binadamu bali kama mwanamke. Kwa hiyo kipimo unachopimwa ni mara mbili japo sijapata shida sana ndani ya LHRC kwa sababu tayari ni shirika la haki za binadamu linalojitahidi kuzingatia masuala ya jinsia lakini huko nje watu hawaamini masula haya ya jinsia."

Anaongeza: "Kuna wakati tulifanya mabadiliko makubwa ndani ya shirika, tukataka tupate nafasi mbalimbali ambazo zinaonekana ni za wanaume kwa kuwapa fursa wanawake na tuliwaajiri wengi sana, cha ajabu hata katika asasi za kiraia na baadhi ya wanachama, walianza kusema LHRC sasa imekuwa ya wanawake, kwa hiyo huo ni mfumo dume, kuna asasi nyingi wanawake wako kwenye uwiano wa asilimia 20 na wanaume 80 lakini haishangazi. Na suala siyo kuwa na wanawake wengi, bali ni kuwa na watu wanaofanya kazi, na hili ni shirika la haki za binadamu, je lingekuwa la kawaida,"anahoji Anna.

**SIKATI TAMAA**

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC anasema hata akikutana na changamoto kubwa kiasi gani, siyo mtu wa kukata tamaa. "Sikubali kusema nimeshindwa kitu, na nahisi siku nikisema nimeshindwa labda ndiyo ninaaga dunia. Kwa hiyo siyo mtu wa kusema siwezi ni lazima nijaribu kufanya na hiyo ndiyo inanisaidia nisikate tamaa. Nina msemo wangu kuwa 'washindi hata siku moja hawaghairi na wanaoghairi siyo washindi' japo changamoto ni nyingi."

Anazitaja sababu zinazochangia asikate tamaa kuwa ni kutokana na nguvu yake ya asili lakini pia kazi wanazofanya za kusaidia wanyonge kuhakikisha wanatabasamu, kufahamu haki zao, kutetea wananchi ni hamasa tosha ya kutokurudi nyuma.

"Ni furaha iliyoje unapotetea mtu na anapata furaha, hiyo pekee inakupa nguvu ya kesho yake kuamka asubuhi kwenda tena kazini na kuwatumikia wananchi ambao ndiyo walengwa wako wakuu" anasema Anna ambaye ni mama wa familia na kwamba pamoja na majukumu mengi anajitahidi kila nafasi kuiongoza kwa ufasaha mkubwa.

**NI MCHUNGAJI**

Pamoja na ukurugenzi anasema anashiriki katika bodi nyingi za Wakurugenzi ikiwamo Bodi ya Wadhamini ya Christian Catholic of Tanzania (CCT), International Fellows Program ya Marekani na Africa NGO`s, akishika nafasi mbalimbali kwenye bodi hizo.

Anasema mbali na nafasi hizo za kitaaluma, pia ni mchungaji anayechunga watu wasiopungua 200 chini ya huduma ambayo hakupenda kuitaja akisema ni kazi anayoifanya kwa muda maalumu

"Siyo Pasta wa muda wote lakini ni mchungaji, nina kwaya yangu kubwa sana na mimi ndiye mwenyekiti ina watu 130, kwa hiyo wote inabidi niwaongoze kila mmoja na namna alivyo,"anasema Anna akieleza mengi anayojivunia LHRC

**MAFANIKIO LHRC**

Ni pamoja na kuwafikia watu wengi sana kwa kipindi kifupi kuwasaidia kutatua kero zao na tangu ashike nafasi hiyo amekuwa akisisitiza sana watendaji wote katika taasisi hiyo kufika kwenye jamii kuhudumia wananchi wanaohitaji msaada wao.

"Siyo kwamba kukaa huku kwenye mikutano ni vibaya hapana , kama mnakutana na wenye maamuzi sawa, lakini mimi napendelea sana twende nje kuwahudumia wananchi moja kwa moja na wakurugenzi wangu wasaidizi wanajua hivyo,"anasema Anna.

Anajivunia kuleta usawa wa kijinsia kwenye ofisi mbalimbali, kuanzisha programu maalum ya masuala ya jinsia ambayo wanahakikisha wanazingatia usawa wa kijinsia kwenye taasisi yao na nje kwa kufanya utetezi.

Anasema wakati anashika nafasi hiyo aliyonayo LHRC wanaume waliokuwa wakifanya kazi hapo walikuwa kwa asilimia 70 na wanawake asilimia 30, lakini alivyoingia alifanya mapinduzi makubwa na magumu na kwamba mpaka sasa nafasi nyeti katika shirika hilo zinashikiliwa na wanawake.



DOROTHY SEMU

# Makamu Mwenyekiti ACT-Wazalendo aanika amelenga demokrasia imara ya vyama vingi

INATOKA UK. 15

hitaji rasilimali fedha,watu na nyenzo kuwezesha kifikia malengo. Chama hiki kinaendeshwa kwa ruzuku kidogo iliopatikana na michango ya wanachama. Kila tunapopata uwezo huo wa kiuchumi tumekuwa tukiwekeza kwa kutekeleza majukumu mbalimbali muhimu ya kichama. Ni gharama kubwa kuendesha chama cha siasa, hivyo kuwezeshwa kifedha na nyenzo na taasisi za mambo ya kisiasa, wadau na wapenzi ni muhimu. Bado pia tunaiona fursa ya serikali kuboresha uchangiaji wa kifedha katika kuboresha uendeshaji wa vyama vya siasa nchini. Sisi tulipendekeza maboresho makubwa kwenye utoaji wa ruzuku ya serikali kwa vyama ya siasa kupitia kikosi kazi cha Rais. Pendekezo la mapitio ya vigezo na asilimia za mgawanyo, ili angalau iwepo ruzuku ya msingi uendeshaji kwa vyama vyote. Asilimia kumi ya ruzuku iwe ni kwa vyama vyote. Na asilimia nyingine 90 ziwekewe kutegemea viti vya ubunge, kura za ubunge na udiwani.

**SWALI:** ACT Wazalendo bila Maalim Seif ikoje?

**JIBU:** Maalim Seif alikuwa ni muumini wa taasisi. Aliamini kwenye kujenga taasisi imara ya ACT Wazalendo na kuandaa viongozi wengine wengi wa kuindeleza, ndoto kuu ya ACT Wazalendo. Kibinadamu tunamkosa kama kiongozi wetu, lakini tunavuna alichoacha. Ni ACT Wazalendo iliyoimarika zaidi katika kufika maono yake, kiutendaji inayojiandaa kikamilifu kushika hatamu za uongozi wa nchi. Wakati huo huo ikitekeleza wajibu kama chama cha siasa makini kinachosemea Watanzania na kuisimamia serikali.

**SWALI:** Mwaka 1964, Nyerere alisema inawezekana timiza wajibu wako. Wewe unaelezaje nguvu yako katika Chama cha ACT Wazalendo?

**JIBU:** Nilijiunga na ACT Wazalendo Novemba mwaka 2014 baada ya kuvutiwa na maono yake makubwa kuhusu taifa hili. Niliona ni jahazi jema ambalo kwa kushirikiana na wenzangu niliowakuta tutafanya kazi kwa bidii kufanikisha ndoto hiyo na kufanya siasa za mabadiliko zenye tija nchini. Mchango wangu mkubwa katika chama hiki ni kukitumikia kwa juhudi kubwa na maarifa kufika malengo tuliyojiwekea. Naamini kwenye uongozi wa pamoja unaoleta matokeo makubwa chanya. Nguvu yangu ndani ya chama ni nguvu yetu sote.

**SWALI:** Tueleze kwa ufupi historia yake?

JIBU: Kitaaluma mimi ni 'mfiziotherapia'. Nina shahada za uzamili ya sayansi katika fani hii na nimebobea kwenye masuala ya utengemao (physical rehabilitation). Nilikuwa mtumishi wa umma kwa miaka 17. Nimesomea Chuo cha Fiziotherapia - KCMC Moshi na baadaye nilisoma Chuo Kikuu cha Western Cape - Afrika ya Kusini. Niliingia rasmi kwenye siasa Novemba 2014 kwa Chama cha ACT Wazalendo. Na




Makamu Mwenyekiti wa ACT Wazalendo, Dorothy Semu, katika picha mbili tofauti. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

nimeshika nafasi mbalimbali kuanzia Katibu wa Sera na Utafiti (2015-2017) na Katibu Mkuu(2017-2020), Makamu Mwenyekiti Bara kuanzia mwaka 2020 hadi sasa. Lakini pia mimi Waziri Mkuu Kivuli tangu Februari 2022. Chachu kuwa mwanasiasa iliniijia baada ya kuona utofauti mkubwa wa kitabaka katika shule za msingi nilizosoma nikiwa kati ya miaka sita hadi tisa.




Nikiwa darasa la kwanza hadi la tatu nilipata fursa adimu ya kusoma shule mbili kwa mwaka. Nilikuwa mwanafunzi wa shule ya kimataifa Arusha ambayo ilikuwa na likizo moja ya ziada ya mwezi mzima. Mama yangu alisema likizo hiyo niwe naitumia kuhudhuria shule nyingine ya msingi ya Sanawari-Arusha.

Shule hizi mbili zilikuwa na utofauti mkubwa katika kila hali majengo, viwanja vya michezo, walimu, vifaa vya kufundishia. Katika utoto ule nilitamani shule ile ya Sanawari iwe na hali bora zaidi iweze kufanania shule yangu ya kila siku. Niliona sisi sote kama watoto tunastahili shule bora.

Kwa hiyo nilijiwekea nia ya kuwa sehemu ya kubadilisha hali kama hizi. Kama sehemu ya kutimiza azma hii niliamua kuingia rasmi kwenye siasa nitakapotimiza miaka 40, ili niweze kutoa mchango wangu katika mabadiliko kwa kushirikiana na wenye nia kama yangu.

**SWALI:** Nipashe inakupa fursa ya kuelezea mambo ambayo unatamani kuyafikisha kwa wananchi, je ni yapi?

**JIBU:** Tuna ndoto ya kuwa na taifa bora lenye ustawi lililojengwa kwenye misingi ya demokrasia, haki na amani. Ni wajibu wetu kama Watanzania kushiriki kwenye ujenzi wa demokrasia hii kwa kuviunga mkono vyama vya siasa. ACT Wazalendo inaendelea kuwasemea wananchi kwa kuisimamia, kuikosoa serikali na kuja na Sera Bora mbadala kuleta hali bora ya maisha ya Watanzania. Ninaomba wananchi watuunge mkono.

> “Nikiwa darasa la kwanza hadi la tatu nilipata fursa adimu ya kusoma shule mbili kwa mwaka. Nilikuwa mwanafunzi wa shule ya kimataifa Arusha ambayo ilikuwa na likizo moja ya ziada ya mwezi mzima. Mama yangu alisema likizo hiyo niwe naitumia kuhudhuria shule nyingine ya msingi ya Sanawari- Arusha.

UNAIBU,KURITHI URAIS AFRIKA:

# Ni zama Wakenya kujifunza kilichotokea Afrika Kusini

**Na Ani Jozeni**

BAADA ya ushindi katika kinyang'anyiro cha urais nchini Kenya, Rais William Ruto ameunda serikali, na inaelekea hatakuwa na mapumziko ya awali serikalini kabla ya wananchi kutafakari mwenendo wake madakarani utakuwaje.

Tofauti na hilo Wakenya wataangalia ni kwa njia gani atakabiliana na hali inayojitokeza katika siku 100 za kwanza, kwani tayari kuna mawaziri aliowateua wenye kesi za jinai mahakamani.

Kilichotokea Kenya kinaendana na kilichotangulia ambacho kinafanana na kisa kingine cha kurithi kiti cha urais kilichotokea Afrika Kusini ambako Thabo Mbeki alipinga naibu wake Jacob Zuma kuwa mrithi wa urais , lakini akakwama ndani ya chama cha ANC, kama ilivyotokea Kenya.

Kwa lugha ya kawaida aliyeko madarakani kupinga naibu wake kuwa mrithi wake inaweza kuonekana kama 'roho mbaya,' yaani kumchongea mtu na kutokutaka mafanikio yake.

Zinaweza kutolewa sababu tofauti kwa hali hiyo, kwa mfano hisia za ukabila au migongano ya kiutendaji, mradi kila mtu aridhishwe na maelezo haya au yale. Ila kwa wakati huo ambao mzozo unafukuta kurithi nafasi hiyo, kitakachoonekana ni upungufu wa utii wa rais kwa naibu wake, na kufurahia ushindi wa naibu pindi kura ikienda upande wake. Ndivyo ilivyotokea Afrika Kusini na hivi karibuni ikawa ni Kenya.

Haijapita hata mwezi mmoja, wakati ambapo ndiyo Rais anaunda Baraza la Mawaziri baada ya kuapishwa, unakuja mlolongo wa maswali ambayo hayataweza kujibiwa ndani ya mfumo wa siasa uliopo. Itabidi maswali hayo yaishie katika makala za magazeti na ili kuyaeleza kwa ufasaha, yahamishiwe katika sanaa kama ambavyo inaanza kuonekana na siyo kujaribu kuyachukulia kisiasa au kisheria kwani 'maji yatazidi unga.'

Ni mabadiliko yanayotarajiwa kisiasa nchini Kenya yatakayoleta ukomavu, uvumilivu na uhimilivu halisi.

Kinachotofautisha Kenya na Afrika Kusini katika mazingira yaliyopo ni kuwa Afrika Kusini ina mfumo halisi wa mashindano hata ndani ya chama tawala.


Naibu rais wa zamani aliyeupata urais mwishowe aliondolewa madarakani na kufikishwa mahakamani, katika mapitio magumu ya kisiasa na kisheria ambayo Kenya haina uwezo huo.

Imefaulu kujenga ushindani na kutoa uhuru mpana kwa mhimili wa mahakama kusimamia katiba na sheria, ila haitakuwa rahisi kwa vyombo vya dola, taasisi hizo kuikabili hali hii.

Kilichotokea Afrika Kusini hakitazamiwi Kenya, na matokeo yake ni kuingia hatua nyingine



Rais William Ruto (kushoto) na Kiongozi Mkuu wa ANC Musalia Mudavad , aliyemteua na kumpa madaraka makubwa kuliko mawaziri wote.



Jacob Zuma, rais wa zamani wa Afrika Kusini anayetuhumiwa kwa kesi za jinai na kashfa nyingi. PICHA **ZOTE: MTANDAO**

> Licha ya kuwa moto utafukuta pembeni kama ilivyotokea awali, alipouawa Waziri wa Mipango Tom Mboya mnamo 1969, mbunge maarufu Josiah Mwangi Kairuki mwaka 1975 au Waziri wa Mambo ya Nje Dk. Robert Ouko 1990yalivyopotelea mbali .

ya demokrasia kwa njia mbili tofauti. Huko kwa Jacob Zuma ugomvi mkubwa ulizuka kutokana na mwenendo wake akiwa madarakani, kiasi kwamba wale ambao walimbeza Mbeki kwa madai kuwa ana 'roho mbaya' ya kutokumtakia mema naibu wake walianza 'kuuona mwanga,' kumbe alikuwa na sababu za msingi na siyo ushindani wa kisaikolojia ambao baadhi wanaita 'chuki binafsi.'

Ila wakati huo hapakuwa tena na jinsi, ikabidi wangoje hadi uchaguzi mkuu ukaribie ndipo wamwondoe, kulinda idadi ya kura siku za mbeleni.

Mvurugano huo ulikuwa kichocheo kimojawapo cha kuanza kupangua uungwaji mkono wa chama tawala cha African National Congress (ANC) ambacho ndiyo cha jadi kupigania uhuru (au usawa) nchini humo. Mwezi Novemba mwaka jana katika uchaguzi wa serikali za mitaa (manispaa na vitongoji) ANC ilipata asilimia 47.9 ya kura, mara ya kwanza imepata chini ya asilimia 50 ya uungwaji mkono.

Ni katika ugomvi kuhusu Zuma ambako nafasi ya ANC katika imani ya watu ilianza kushuka, ingawa bado ni chama kikongwe cha siasa.

Huko Kenya, baada ya tuhuma za kina kuinuliwa kuhusu kesi zilizozofunguliwa zinazowakabili au kuwagusa kwa karibu baadhi ya walioteuliwa uwaziri, na matukio yanayohitaji kuchunguzwa ambayo yanaweza kumgusa rais moja kwa moja, huenda kilichotokea Afrika Kusini hakitafuata.

Licha ya kuwa moto utafukuta pembeni kama ilivyotokea awali, alipouawa Waziri wa Mipango Tom Mboya mnamo 1969, mbunge maarufu Josiah Mwangi Kairuki mwaka 1975 au Waziri wa Mambo ya Nje Dk. Robert Ouko 1990yalivyopotelea mbali .

Ila raia wa Kenya watapata funzo kama Afrika Kusini kuwa rais aliyetangulia alikuwa na sababu za msingi kutomwamini naibu wake kikamilifu.

Jambo la kushangaza ni kuwa matokeo ya kisaikolojia ya hali hiyo jijini Nairobi tayari yameanza kuonekana hasa katika mitandao ya kijamii, kwa upande fulani, kama ilivyo Uganda.

Ni pale wachekeshaji wanapotangulia na kila aina ya vionjo kuhusu walio madarakani, na watu wanapakua vibonzo kama hivyo na kurushiana mitandaoni, ikiwa ni njia ya kujiliwaza kwani hawawezi kuongea hadharani wanachohisi, na hasa hawawezi kuandamana kudai yote hayo.

Ni mazingira ya kutoamini maonyo, na ikitokea kuwa kilichotabiriwa kinaonekana hakiwezi kuelekezwa kwa aliyelengwa wakati ule, kwani bado ana taswira halisi ya kiongozi wa fikra, hisia na mipango.

Kukosa raha na hali hiyo kutalenga kwingine, kutoiamini siasa kabisa, kukaa pembeni, kupisha mambo yaendelee.

Ni hali ambayo tayari ilishaanza kuonekana pale wagombea wawili walipobakia, yaani Ruto na Raila Odinga, waziri mkuu wa zamani akiungwa mkono na Rais Uhuru Kenyatta aliyemaliza muda wake. Hakuna jipya katika matukio ya hivi sasa kwani tangu awali vianzio vya utii kwa Ruto na mapana yake vilikuwa wazi; watu walitaka mabadiliko na siyo kuendelea na 'Timu Kenyatta' kwa kumweka tu Raila katika kiti chake.

Ni siri ya ushindi wa Ruto kwa maana kuwa Raila hakuwa na uwezo kubadilisha mfumo wa awali. Idadi ya waliojitokeza kupiga kura ilifikia wastani wa asilimia 60 hadi 62, wakati uchaguzi mkuu wa 2017 waliojitokeza kupiga kura walifikia asilimia 80.

Siyo ajabu hali hii ikasaidia kujenga misingi tofauti ya ushawishi wa kisiasa, kumaliza utii kwa makundi ya kikabila yenye harufu ya ufisadi ambayo yalitawala mwenendo wote wa uchaguzi mkuu mwaka huu. Haitakuwa rahisi kufika hapo lakini hata kama siasa kwa jumla itabaki ilivyo, watu hawatawapigania viongozi wa makundi ya kisaisa pale watakapodai wameonewa. Hivyo, hata siasa isipokuwa 'safi' bado kutakuwa na amani.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Burkina Faso hakukaliki mapinduzi kila kukicha

- Tangu 2015 marais watatu wametumbuliwa
- Aliyepinduliwa aondoka Ikulu kwa masharti
- Adai ulinzi wa uhakika kwake na maswahiba

**Na Gaudensia Mngumi**

MWAKA 2014, mamilioni ya Waburkinabe -raia wa Burkina Faso, waliumaliza utawala wa miaka 27 wa Rais king'ang'anizi ikulu, Blaise Campaore kwa kumlazimisha kuachia ngazi.

Mwaka 2015 Christian Kabore alichaguliwa kuwa rais. Katika uchaguzi wa watu wengi wenye matumaini waliokuwa wakiimba, 'hakuna kitakachokuwa kama hapo awali.' Wakimrejea Campaore.

Tangu wakati huo hali si shwari tena, kilichoanza kama uasi katika nchi jirani ya Mali na raia wa kabila la Watuareg waliotengwa mwaka 2012, kimeendelea kuteka eneo lote la Sahel hadi Burkina Faso.

Leo kuna mivutano ya kijamii maeneo yasiyotawalika na ukosefu wa usalama, makundi mbalimbali yenye silaha yanayohusishwa na Al-Qaeda na ISIS yanateka miji na majimbo, kudhibiti shughuli za kiuchumi na kusababisha ukosefu wa amani na utulivu wa kisiasa .

Burkina Faso imekuwa na sehemu yake ya mgogoro huo, kwa kiasi kikubwa ukisukumwa na kundi la Jama'at Nusrat al-Islam wal-Muslimin (JNIM) linalodaiwa kuwa na uhusiano na al-Qaeda.

Kuongezeka kwa mashambulizi ya makundi yenye siasa kali, kumesababisha mabadiliko ya serikali nchini Burkina Faso yanayofanywa kwa mapinduzi yasiyomwaga damu.

Yametokea mara mbili ndani ya mwaka 2022 katika nchi hiyo inayodaiwa kuwa ni miongoni mwa mataifa maskini zaidi Afrika.

Maandamano ya kitaifa yalimuondoa , Blaise Campaore kwa kumlazimisha kuondoka, akarithiwa na Roch Marc Kabore, katika uchaguzi wa kidemokrasia lakini naye akaondolewa na Paul-Henri Sandaogo Damiba.


Na hivi karibuni maofisa wa ngazi ya chini jeshini wanampindua Luteni Kanali Paul-Henri Sandaogo Damiba, wakidai ameshindwa kupambana na mashambulizi ya vikundi vyenye itikadi kali .

Wanajeshi hao wakamtangaza mwenzao Kapteni Ibrahim Traore (34) kuwa msimamizi wa serikali ya mpito.

Taarifa za Idhaa ya Kiswahili-DW, ikiripoti kuhusu mapinduzi hayo inasema, Januari mwaka huu Burkina Faso ilianza mwaka kwa kumpindua rais wa wakati huo, Roch Marc Christian Kabore, ambaye Damiba alimweka kando na jeshi likimshutumu kuwa ameshindwa kupambana na makundi ya wapiganaji wenye itikadi kali, kama ambavyo naye wanamwambia sasa.



Kapteni Ibrahim Traoré ndiye kiongozi mpya wa kijeshi wa Burkina Faso: **PICHA. ZOTE :MTANDAO.**



Paul-Henri Sandaogo Damiba, Kiongozi wa Kijeshi wa Burkina Faso, aliyeongoza kuanzia Januari 31 hadi Septemba 30, 2022.

Taifa hilo likiwa na watu milioni 16, likashuhudia tena mapinduzi mengine ndani ya siku mbili za mwanzo za mwezi huu yakimuondoa Damiba ikulu, aliyeondoshwa Ijumaa iliyopita.

Kabla ya kupinduliwa risasi zilirindima katika maeneo ya kuzunguuka makazi ya rais na makao makuu ya jeshi nchini Burkina Faso usiku wa kuamkia Ijumaa, serikali ikisema kuwa tukio hilo linahusishwa na mgogoro wa ndani katika jeshi hilo lakini pia, wanajeshi kadhaa wakiwa wamefunga barabara nyingi,kuu za mji mkuu Ouagadougou.

Serikali ya BurkinaFaso ikaeleza kuwa ni mgogoro wa ndani jeshini, jeshi ambalo lilifanya mapinduzi na kutwaa madaraka kwa nguvu nchini humo mnamo mwezi Januari, halijawa na amani wala kuleta utulivu.

DW inaeleza kuwa Burkina Faso imeandamwa na machafuko kwa muda mrefu ikiwa ni pamoja na mapinduzi yaliyomuweka madarakani kanali Damiba baada ya kumuondoa Kabore aliyechaguliwa na wananchi akiahidi kurudisha utawala wa kiraia ndani ya kipindi cha miaka miwili na kuyamaliza makundi ya wanamgambo nchini humo hasa wale wenye itikadi kali.

Aidha, inaelezwa kuwa mwanzoni mwa mwezi Septemba Damiba alimtimua Waziri wa Ulinzi na kujitwika mwenyewe jukumu hilo.Maelfu ya watu wamekufa na wengine 2,000,000 wameachwa bila makazi kufuatia mapigano tangu mwaka 2015 wakati uasi uliposambaa BurkinaFaso ambayo tangu wakati huo imegeuka kuwa kitovu cha machafuko katika eneo la Sahel, inaeleza DW.

Na mashambulizi katika taifa hilo yameongezeka tangu mwanzoni mwa mwaka huu licha ya utawala huo wa kijeshi kuahidi kulipa kipaumbele suala la usalama.

**KUKUBALI KUTUMBULIWA**

"Rais Paul-Henri Sandaogo Damiba alipendekeza kujiuzulu kwake ili kuepusha mizozo," anasema Hamidou Yameogo, msemaji wa juhudi za upatanishi. Inasema taarifa ya mtandao wa Al Jazeera

Licha ya Damiba kukubali kutumbuliwa anaweka "masharti saba" ya kuachia ngazi. Kwanza anataka wamhakikishie usalama kwa washirika wake katika jeshi, "anataka uhakika wa usalama na haki zake", na wanaochukua uongozi wataheshimu ahadi aliyotoa kwa Jumuiya ya Uchumi ya Afrika Magharibi ya kurejea kwa utawala wa kiraia ndani ya miaka miwili.

Traore anateuliwa rasmi kuwa mkuu wa nchi baada ya kukubali masharti yaliyotolewa na Damiba, akitoa wito kwa raia kuwa na utulivu, kujizuia kufanya fujo na kusali.

Jumapili iliyopita wanajeshi wanaomuunga mkono Traore wanasema ataendelea kutawala "hadi kuapishwa kwa rais wa Burkina Faso aliyeteuliwa na vikosi vya jeshi la taifa hilo" katika tarehe ambayo haijatajwa.

Mabadiliko ya pili ya uongozi katika mwaka mmoja yalianza mwishoni mwa wiki iliyopita wakati maofisa wa kijeshi walipotangaza kumuondoa madarakani Damiba, kuvunjwa kwa serikali ya mpito na kusimamishwa kwa katiba, inaongeza.

**NGUMU KUONDOKA**

Taarifa inayotolewa Jumapili na wanaomuunga mkono Damiba aliyeongoza mapinduzi Januari mwaka huu kumtoa Kabore, inasema hakuwa na nia ya kuachia madaraka na kuwataka maofisa hao "kurejea kwenye fahamu zao". Lakini kwa sasa amejiuzulu na kwa mujibu wa vyombo vya habari, ameikimbia nchi hiyo na kuelekea nchi jirani ya Togo Jumapili iliyopita.

AlJazeera inaongeza kuwa hali ya wasiwasi imezidi kuongezeka nchini Burkina Faso tangu Ijumaa iliyopita huku yakiripotiwa mapambano kati ya waandamanaji na vikosi vya usalama na Jumamosi iliyopita, waandamanaji wenye hasira waliushambulia ubalozi wa Ufaransa huko Ouagadougou mji mkuu wa nchi hiyo wakiamini kuwa Damiba alikuwa akipanga mashambulizi kutoka kwenye "kambi ya Ufaransa" - madai ambayo yeye na Ufaransa walikanusha. Burkina Faso ni koloni la zamani la Ufaransa.

**VIKUNDI VYA KIGAIDI**

Makundi ya siasa kali ni changmoto nchini humo, baada ya serikali ya Burkina Faso mwezi Septemba kutangaza kuwa takriban wanajeshi 11 wameuawa na raia 50 hawajulikani walipo baada ya wapiganaji waliokuwa na silaha kuushambulia msafara wa magari 150 uliokuwa na wanajeshi wakipeleka vifaa katika mji wa kaskazini, wakati wanapita jangwani Sahel.

Ikaelezwa kuwa shambulio hilo lilifanyika katika wilaya ya Gaskinde katika mkoa wa Soum, ambapo makundi yenye silaha yenye uhusiano na al-Qaeda na kundi la ISIS yamezidisha mashambulizi na kuyateka maeneo mengi tangu 2015.

Katika jimbo la kaskazini la Soum, makundi yenye silaha yameteka na kuzingira maeneo kadhaa, hivyo misafara ya serikali na ndege yamepeleka bidhaa muhimu kwa raia walionaswa. Shambulio la mwezi uliopita lilikuwa linalenga misafara ya ugavi wa huduma na bidhaa inayosindikizwa na jeshi.

***MITANDAO***

# Yafanyike mambo makubwa, tofauti kumuenzi Mwalimu

**INATOKA UK. 13**

na kustawi Lushoto kwenye Msitu wa Asili wa Amani.

Maua hayo maarufu kama 'African violets au Saintpaulia ionantha,' yanapatikana ndani ya misitu ya kitropiki yenye mvua nyingi na hapa ndipo nyumbani kwake , hivyo kutumia utaalamu na kupeleka maua hayo Butiama kwenye bustani ya Kambarage ni jambo linaloweza kumtangaza Mwalimu duniani kote na kuvutia utaliii kwa heshima yake.

Pamoja na hilo lipo ua jingine maarufu duniani likiuzwa kwa dola nyingi linalopatikana katika Misitu ya Magamba liitwalo Streptocarpus shumensis yote hayo yangeweza kuhifadhiwa katika bustani za Mwitongo kwa heshima ya kukuza, kutangaza utalii na juhudi za Mwalimu za kuitunza na kuihifadhi Tanzania.


Kuweka 'zoo' lenye wanyama kutoka Zanzibar mahsusu kwa Tanzania pekee jamii ya nyani au kima wekundu 'red colobus' , komba mbilikimo wanaoitwa Rondo dwarf galago (hapatikani sehemu nyingine ili kwenye misitu ya hifadhi ya Rondo mkoani Lindi ni kivutio cha kipekee.

Katika misitu ya Kilombero na Udzungwa mkoani Morogoro kuna ndege anayefanana na duma au chui kutokana na mabaka mabaka kwenye mbawa akipewa jina la 'Udzungwa forest partridge' Watanzania wanaweza kuwajengea makazi na hifadhi huko Butiama ili kuvutia utalii Mwitongo alikozaliwa Baba wa Taifa.

Viumbe kutoka misitu ya Mazumbai, Lushoto akiwamo chura mwenye ngozi yenye upele 'Mazumbai warty frog' wakitangazwa ndani ya zoo ya Butiama wataleta upekee na ubora wa utalii kwa jina la Nyerere mwana wa Mwitongo.

Ni jukumu la Wizara ya Mali Asili na Utalii. Mwalimu Nyerere Foundation, vyuo vikuu na wataalamu mbalimbali kuhamasisha uchangiaji na uwekezaji kijijini hapo wa kisasa na wa kipekee ili watu waone umuhimu wa kujenga vivutio vitakavyowezesha jamii na wageni kutoka fani na mataifa mbalimbali kufika Butiama kwa heshima ya Nyerere.









Ndege anayepatikana Tanzania pekee akiitwa 'udzungwa forest partridge', vito kama green tourmaline vitumike kumuenzi Nyerere: **PICHA MTANDAO.**

Lakini si hayo tu zinahitajika juhudi za kujengwa taasisi za kielimu kama Chuo Kikuu cha Madini na Geolojia Buhemba kwa ajili ya kumuenzi Mwalimu aliyehifadhi madini hadi Watanzania watapoyachima leo.

Ni vyema pia serikali ifikirie kufungua na kujenga migodi ya Buhemba na Kyabakari ili iwe vituo vikubwa vya kibiashara, kijamii na kielimu ili vichangie kwenye ajira na mapato ya Wilaya ya Butiama kwa heshima ya Mwalimu Nyerere.

Ni vyema kujenga kiwanda cha kukata na kuchonga dhahabu za migodi ya Knada ya Ziwa ili kijiji cha Nyerere kiwe kituo cha biashara ya dhahabu duniani kikipewa jina la Julius Nyerere Butiama Gold Centre.

Yote hayo yataifanya Butiama iendelee kuwa sehemu nyeti kwa kuuenzi mchango wa Nyerere wa kuikomboa Tanzania pamoja na Afrika.

Butiama au nyumbani kwa Nyerere palikuwa ni kimbilio la kusaidia Watanzania wenye shida yakiwemo mahitaji muhimu, fedha, ushauri na faraja kwa wajane, lakini viongozi wa Afrika wakiwamo wapigania uhuru wa Msumbiji, Afrika Kusini, Angola na Zimbabwe hivyo, jitihada za kuanzisha kituo cha Afrika Butiama ni muhimu ili kitumike kwa mikutano, makongamano na mikusanyiko ikiwamo ya kidini kumkumbuka Mwalimu.

Juhudi zianze sasa kuimarisha na kuendeleza Mfuko wa Mwalimu Nyerere Foundation kwa kuupa bajeti ili uwe kimbilio kwa wananchi wa kipato kidogo lakini pia utimize malengo ya kile Mwalimu alichokitamani alipouunda.

Wakala wa Barabara wa Taifa (TANRODS) na TARURA waone haja ya kujenga barabara, madaraja na miundombinu ya kipekee na ya mfano kuunganisha mkoa wa Mara, Manyara na Arusha ambazo umahiri, upekee na ubora wake utaendelea kuimarisha na kuzienzi kazi zisizosahaulika za Mwalimu Nyerere.

Aidha, kujenga na kuyaboresha zaidi Makumbusho ya Mwalimu Nyerere yaliyoko Butiama ili yawe kitovu cha kupata taarifa za kiuchumi, kitamaduni na elimu ya Siasa na Ujamaa na Kujitegemea, harakati za ukombozi wa Afrika , Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote (NAM) na Ushirikiano wa Mataifa ya Kusini (South South Corporation) ni suala lisilokwepeka ili kumuenzi Mwalimu.

Halikadhalika Makumbusho ya Mwalimu yawe ni kitivo cha kupata kumbukumbu na mafanikio, changamoto na athari ya Azimio la Arusha, Vijiji vya Ujamaa na yale yote yanayostahili kuenziwa na kudumishwa Tanzania na Zanzibar.

Pamoja na kuwa na taarifa hizo Makumbusho iwe na taarifa za kazi za viongozi wa kitaifa za Rais Ali Hassan Mwinyi, Waziri Mkuu Rashid Kawawa, Sheikh Abeid Amani Karume, Abdi Jumbe, Bibi Titi Mohamed, Edward Sokoine, Abdul Wakili, Benjamin Mkapa, Dk. Salmin Amour, Amani Karume Jakaya Kikwete, John Magufuli na Rais Samia Suluhu viongozi wote wakuu wa nchi.

Lakini pia makatibu wakuu kama Dk.Horace Kolimba, Lawrence Gama na viongozi wengine walioshirikia kujenga Tanzania na Zanzibar.

## CHEMSHABONGO NA -00 9 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. tupa kitu juu
7. mawe makubwa
8. safari ya kiongozi kikazi
9. mji mkuu wa Jordan
10.kifupi cha neno bibi
11.hali inayoleta matokeo mabaya 14.nafaka iliyosagwa
16.maoni 17.athari mbaya
18.ruhusa 20.ami 22.tunda la mnazi 23.mnyama kama chui mwenye mbio sana

Chini:
2. namna ya kumimina
3. mji mkuu wa zamani Thailand 4. upesi 5. utulivu
6. wingi wa neno mshindi
8. kitabu cha nyimbo katika Biblia 12.karo ya shule
13.fanya kama wengine
15.Gea 17.mzazi wa kike
19.vifaa vya kazi
21.badilisha kitu kwa fedha






## Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

ARGENTINA IGBO
MKALIMANI LALA
MADAFU UTII
ALAMSIKI SAA
MILANGO NNE
DHAHABU
MABAFU
UNUNUAJI
SHINDWANA
SKAFU
UNGUA
ULAYA
ILALA
LAHIKI

S A A

Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| K | U | N | G | U | I | A | | | | |
| A | | | A | | | L | | | | |
| Z | | | M | B | W | A | | | | |
| A | D | A | B | U | | M | | | | |
| K | | M | I | A | K | A | | T | | |
| I | N | U | A | | U | | K | O | M | A |
| S | | | | | N | | I | B | A | |
| T | | | | | J | O | G | O | O | |
| A | | | | | A | | A | | N | |
| N | | | | | | | L | | I | |
| I | N | D | O | N | E | S | I | A | | |





| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| D | A | R | A | S | A | | U | | M |
| A | M | U | | | D | U | N | I | A |
| R | A | D | I | | A | | G | | T |
| A | N | I | K | A | | S | U | M | U |
| J | A | W | A | B | U | | A | | N |
| A | | A | M | U | R | U | | | D |
| | | | A | | E | D | I | T | A |
| U | Z | I | | A | M | I | N | A | |
| T | | | | | B | | S | A | A |
| U | C | H | O | K | O | Z | I | | |

maoni: 0755429240



# Waonywa kufanya shughuli za kibinadamu hifadhini

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WANANCHI wa Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wametakiwa kuacha kufanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya hifadhi ili kuepuka kuharibu mazingira na kupunguza utalii kwenye maeneo hayo.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, aliyasema hayo juzi wakati maofisa wa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), walipokuwa wanatoa elimu ya utunzaji wa mazingira kwa wananchi wa Kijiji cha Ilundo kichoko pembezoni mwa Hifadhi ya Mlima Rungwe.

Alisema utalii ni miongoni mwa sekta ambazo zimekuwa zikichangia kwa kiwango kikubwa ukuaji wa pato la taifa na kwamba Hifadhi ya Mlima Rungwe ni miongoni mwa vivutio bora katika Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini.

Dk. Anney alisema baadhi ya wananchi wanafanya shughuli za maendeleo ndani ya hifadhi hiyo ikiwamo uwindaji haramu, ukataji wa miti kwa ajili ya shughuli mbalimbali hali ambayo ina hatarisha ikolojia ya hifadhi.

"Kuna baadhi ya watu wanalima humu pembezoni mwa mlima, lakini wapo wawindaji haramu pia ambao wanasababisha moto ndani ya hifadhi hii na kuharibu mazingira, nawaombeni sana muwe walinzi namba moja wa mlima huu," alisema Dk. Anney.

Alisema watalii wanapotembelea eneo hilo huwa wanawanufaisha moja kwa moja wananchi wanaozunguka hifadhi hiyo kutokana na kununua moja kwa moja bidhaa wanazozalisha.

**Baadhi ya wananchi wanafanya shughuli za maendeleo ndani ya hifadhi hiyo ikiwamo uwindaji haramu, ukataji wa miti kwa ajili ya shughuli mbalimbali hali ambayo ina hatarisha ikolojia ya hifadhi.**

# Misaada yaendelea kumiminika Mwakaleli

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MISAADA kutoka kwa wadau mbalimbali nchini inaendelea kumiminika katika Shule ya Sekondari Mwakaleli iliyoko katika Halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya kwa ajili ya kuwafariji wanafunzi wa shule hiyo waliopoteza vitu vyao kutokana na ajali ya moto iliyoteketeza bweni lao.

Bweni la wanafunzi hao wa kike liliteketea Septemba 19, mwaka huu saa 1:45 kwa kuchomwa na mmoja wa wanafunzi hao, Jacquiline Charles (14) wa kidato cha kwanza na wanafunzi hao walipoteza mali zao zote na kubaki na nguo walizokuwa wamezivaa.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Mkuu wa shule hiyo, Mwalimu Shaban Mwala, ajali hiyo haikumdhuru mwanafunzi yeyote zaidi ya kuteketeza mali na kuliharibu bweni hilo ambalo lilijengwa kabla ya uhuru.

Juzi msaada wa vifaa mbalimbali kutoka katika Ofisi ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa, uliwasilishwa katika shule hiyo kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi hao.

Mkuu wa shule hiyo Mwalimu Mwala, alisema moto huo ulisababisha hasara ya Sh. milioni 52 na kwamba wanafunzi walioathirika walikuwa 136 ambao ndiyo walikuwa wanakaa kwenye bweni hilo.

**Kwa sasa wanafunzi hao wanalala kwenye moja ya madarasa hali ambayo inawapa wakati mgumu kutokana na chumba hicho kuandaliwa kwa ajili ya darasa na sio bweni.**

Mwala aliitaja misaada waliyopokea kuwa ni pamoja na magodoro, mablanketi, sare za shule, nguo za ndani, viatu, mashuka na mataulo na baadhi ya vifaa hivyo vilipelekwa kulingana na idadi ya wanafunzi na kwamba vingine vilitolewa mara mbili ya idadi ya wanafunzi.

"Lakini tumepokea fedha taslimu Sh. milioni 2.02 na vifaa vingine vya shule kwa ajili ya wanafunzi kusomea na misaada hii tunaendelea kuipokea, kwa hiyo tunawashukuru sana wadau wote ambao wamejitoa," alisema Mwala.

Aliwataja baadhi ya wadau waliochangia michango hiyo kuwa ni Umoja wa Wakuu wa shule katika Halmashauri ya Busokelo, wadhibiti ubora wa shule, maofisa elimu kata na wananchi pamoja na ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Hata hivyo, alisema tathmini iliyofanyika imebaini kuwa bweni hilo haliwezi kukarabatiwa na badala yake linatakiwa kujengwa upya kwa gharama ya Sh. milioni 150.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Busokelo, Loema Peter, aliwashukuru wadau waliojitokeza kuwachangia watoto hao kwa maelezo kuwa serikali peke yake isingeweza kuwasaidia.

Aliwaomba wadau wengine kuendelea kujitokeza kusaidia michango mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa bweni jipya kwa maelezo kuwa vitahitajika vifaa mbalimbali vya ujenzi ikiwamo saruji, mawe, mchanga, mbao, mabati, nondo na misumari.

Alisema kwa sasa wanafunzi hao wanalala kwenye moja ya madarasa hali ambayo inawapa wakati mgumu kutokana na chumba hicho kuandaliwa kwa ajili ya darasa na sio bweni.

"Sisi kama serikali tunaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa bweni jipya, sasa tunawaomba wadau mtusaidie michango yenu kwa ajili ya ujenzi wa bweni hili jipya maana hili la zamani hatuwezi kulikarabati," alisema Loema.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Anyosisye Njobelo, aliwashauri wanafunzi hao kusahau yote yaliyotokea na badala yake waendelee kusoma kwa bidii ili wafanye vizuri mitihani yao ya mwisho wa mwaka na kwa wanaofanya mitihani ya kuhitimu wafanye vizuri.

Alisema ajali hiyo ni bahati mbaya na kuwasihi walimu kuendelea kuwafariji wanafunzi hao ili wasiwe na hofu.



Mchungaji wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG) Revival Temple, eneo la Kadege, jijini Mbeya, Aman Mwasote (kulia), akiwaombea wanafunzi wa darasa la saba wa Shule ya Paradise Mission juzi, katika ibada maalumu ili wafanye vizuri mitihani yao ya mwisho. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Madiwani watakiwa kushirikiana na watendaji ukusanyaji mapato

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MADIWANI wilayani Chunya, wametakiwa kushirikiana na watendaji wa halmashauri ya wilaya hiyo kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora.

Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Anakleti Michombero, aliyasema hayo juzi wakati wa Kikao Maalumu cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo kilichokuwa kimelenga kupitia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema halmashauri hiyo katika mwaka wa fedha uliopita ilikusanya fedha nyingi na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa mafanikio kutokana na ushirikiano mzuri uliokuwapo baina ya viongozi watendaji na madiwani.

Alisema madiwani wanatakiwa kusimamia mapato pamoja na kupanga na kupitisha matumizi ambayo yanaendana na uhalisia wa mahitaji ya wananchi wa wilaya hiyo.

"Mwaka wa fedha uliopita tulipata tulifanikiwa vizuri sana kwenye ukusanyaji kwa sababu ya ushirikiano mzuri, kwa hiyo nawaomba sana ushirikiano huu uendelee ili wananchi waendelee kufurahia matunda ya uwapo wenu," alisema Michombero.

Mweka Hazina wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Rajab Lingoni, alisema katika mwaka wa fedha uliopita halmashauri hiyo ilikusanya zaidi ya Sh. bilioni 27.9 sawa na asilimia 98 ya makisio ya ukusanyaji wa Sh. bilioni 28.5.

Alisema fedha hizo zinatokana na vyanzo mbalimbali ikiwamo makusanyo ya ndani, ruzuku ya Serikali Kuu na fedha za miradi na kwamba fedha hizo zilitumika kuboresha shughuli mbalimbali za maendeleo.

Alisema kati ya fedha hizo, makusanyo ya ndani walikusanya Sh. bilioni 5.2 ambazo ni sawa na asilimia 108 ya makisio ya halmashauri hiyo na kwamba matumizi mengine ya halmashauri walipokea Sh. milioni 800.

"Fedha za miradi tulipokea Sh. bilioni 9.4 ambazo ilikuwa ni kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, vituo vya afya, zahanati pamoja na maabara," alisema Lingoni.

Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya hiyo, Bosco Mwanginde, alisema watahakikisha wanafanya kazi kwa ushirikiano na kuhakiki wanasimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuepuka kutengeneza hoja za CAG.

Alisema mara nyingi hoja huwa zinaibuka kutokana na kupanga baadhi ya matumizi ambayo hayatekelezeki na kuwataka madiwani kuhakikisha wanakuwa makini wakati wa kujadili na kupitisha bajeti.





# RC atoa siku 14 miradi ya jiji kuanza kuingiza mapato

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, ametoa siku 14 kwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kukamilisha miradi ya maeneo ya biashara na kupata wawekezaji ili serikali ipate mapato.

Senyamule alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea na kujionea miradi mbalimbali inayosimamiwa na Halmashauri ya Jiji ikiwamo stendi kuu ya mabasi yaendayo mikoani, soko la Job Ndugai na City Hotel ambayo mengi hayana wawekezaji.

**Ujenzi wa miradi hiyo na mingine iliyopo inalenga kuwapatia wananchi huduma mbalimbali za kiuchumi.**

Alisema serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya miradi hiyo lakini maeneo hayo bado hayana wawekezaji hali inayoikosesha halmashauri hiyo mapato.

"Nimejionea kwenye hii ziara niliyoifanya ya kutembelea hili soko la Job Ndugai na stendi kuu ya mabasi yaendayo mikoani. Bado kuna nafasi nyingi za wazi hazina watu, zimekaa na haziingizi mapato yoyote," alisema.

Senyamule alisema ujenzi wa miradi hiyo na mingine iliyopo inalenga kuwapatia wananchi huduma mbalimbali za kiuchumi.

"Serikali imewekeza hapa Dodoma makao makuu ya nchi na miradi mbalimbali na mingi ipo ndani ya uwezo wa Halmashauri ya Jiji. Hakuna sababu ya kuwakwamisha watu wanaohitaji maeneo wakati mengi yako wazi," alisema.

Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Abeid Msangi, alisema ndani ya siku 14 halmashauri hiyo itatekeleza agizo hilo na kuhakikisha miradi inapata wawekezaji ili wasiendelee kukosa mapato.

"Mkuu ndani ya wiki mbili tutahakikisha tunajipanga na kuhakikisha wawekezaji wanaohitaji kuwekeza ndani ya mradi wa stendi kuu ya mabasi ya mikoani na soko la Job Ndugai inapata watu," alisema.




Wakazi wa Mtaa wa Majengo sokoni, jijini Dodoma, wakiangalia bajaj iliyoangukiwa na mti kwenye eneo la mzunguko wa barabara iendayo Hospitali ya Rufani ya mkoa wa Dodoma jana. Hakuna mtu aliyejeruhiwa katika tukio hilo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Taasisi kutembelea wanawake magerezani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Newface Creative imepanga kuwafikia wanawake 4,000 walioko magerezani mkoani Dodoma kwa ajili ya kuwapa misaada mbalimbali, zikiwamo taulo za kike.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Abdul Juma, alisema wamepanga kutembelea Gereza la Isanga lililoko Dodoma, Msalato na baadaye Wilaya ya Chamwino kwa ajili ya kutoa misaada kwa watu wenye ulemavu.

Juma alisema lengo la taasisi hiyo ni pamoja na kuwasaidia wanawake walioko gerezani na wengine kwenye vituo vya kulelea watoto yatima ili kuwapatia mahitaji kama walivyo watu kwenye makundi mengine.

"Taasisi yetu imelenga zaidi kuwasaidia wanawake kuanzia watoto, vijana na watu wazima, hivyo tunaomba serikali izidi kutupa ushirikiano ili tuwafikie walengwa tuliowakusudia," alisema Juma.

Alisema taasisi hiyo baada ya kumaliza mkoani Dodoma, imejipanga kwenda Morogoro na mikoa mingine kwa lengo hilo hilo la kusaidia wanawake wa makundi yote.

Pia alisema kupitia mradi wao wa Mwanamke Jasiri, wataendelea kutekeleza jukumu hilo la kutoa misaada kwa wanawake na kundi la watu wenye ulemavu.

"Tumeshawahi kufanya miradi mbalimbali kwa vijana ikiwamo kuwapa madaftari na vyakula katika kituo cha watoto yatima Miyuji, Bagamoyo na

Tuangoma. Tumejipanga kwenda sehemu mbalimbali," alisema Juma.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo, Alex Kapandila, aliziomba kampuni mbalimbali kusaidia ili kuwafikia watu wenye uhitaji.

"Kunahitajika msaada kutoka kwa watu wakubwa ili waje kuwasaidia watu wa chini na serikali haiwezi kufika kila kona. Lakini hizi taasisi ambazo zinaanzishwa kwa ajili ya kushirikiana na serikali zinaweza kuwafikia walengwa wote ambao imekusudia," alisema.

Alisema wanawake hususani walioko vijijini ndio wanahitaji zaidi kuinuliwa kiuchumi.

Katibu Tawala wa taasisi hiyo, Bariki Mwaisaka alisema lengo lao ni kuwakomboa wanawake kupitia mradi wa Mwanamke Jasiri ili kuhakikisha wanafikia na kutimiza ndoto zao.

Alisema wamejipanga kuwafikia wanawake wa vijijini ambao wengi wao wako nyuma kimaendeleo, hivyo watawasilisha misaada pamoja na kuwapa elimu ya namna ya kujikwamua.

Mwaisaka alisema wameanza na Dodoma lakini wanatarajia kwenda Morogoro, Dar es Salaam na mikoa mingine ambayo wamepanga kuitembelea.

# Tamisemi yataja sababu ongezeko watoto wa mitaani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema kushindwa kutoa malezi na makuzi vizuri ya awali kwa watoto, kunachangia kwa kiasi kikubwa taifa kuwa na kundi kubwa la watoto wa mitaani waliokosa malezi.

Mkurugenzi Msaidizi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI anayeshughulikia Serikali za Mitaa, Stephen Motambi, aliyasema hayo jana kwenye kikao cha wadau wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto jijini Dodoma, kilichoandaliwa na Mtandao wa Malezi na Makuzi ya Mtoto (TECDEN).

Motambi alisema kushindwa kufanya vizuri kwenye utoaji huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali kwa watoto, kunachangia kuwa na kundi kubwa la watoto waliokosa malezi bora ambao ni mzigo kwa familia na taifa siku zijazo.

Alisema hatua hiyo inasababisha kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kuhudumia watoto hao kuliko ambazo zingetumika katika malezi na makuzi yao.

"Sasa hivi tunahitaji kuajiri maofisa ustawi wengi ili wakashughulikie changamoto za watoto wa mitaani na fedha nyingi inatumika. Kama wangepata malezi mazuri, wasingekuwapo mitaani, hivyo fedha zinazotumika kuwahudumia hivi sasa zingefanya kazi nyingine kwenye taifa." alisema Motambi.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka maofisa maendeleo ya jamii kutoka sekretarieti za mikoa 10 iliyoanza kutekeleza mradi wa Mtoto Kwanza kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mradi huo ili kuhakikisha watoto wanakua na kufikia utimilifu wao na hatimaye kuwa na tija kwa taifa.

"Lazima muone kuwa hii ni fursa ya kuonyesha umahiri wenu katika kutekeleza afua zinazohusu malezi ya watoto. Mara nyingi mlikuwa mkilalamika kwamba hamna wadau au mradi wa kuwawezesha kuifikia jamii.

"Sasa mradi huu wa Mtoto Kwanza muutumie vizuri na mshiriki kikamilifu katika kutekeleza kwa faida ya jamii na taifa. Kushindwa kufanikiwa kwa mradi huu kutasababishwa na sisi wenyewe kushindwa kutimiza majukumu yetu sawasawa.

"Kwa hiyo nawaomba maofisa wote mshiriki na mtoe matokeo ambayo ni kufanikiwa kwa utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (MMMAM )," alisema Motambi.





# Waziri Maji ataka kasi uunganishaji umeme

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Shaibu Hassan Kaduara, ameutaka uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kufikisha haraka huduma sehemu ambazo wananchi wamewekeza katika kilimo ili kuzalisha kwa gharama na fuu.

Kaduara alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na uongozi wa ZECO pamoja na wafanyakazi wa shirika hilo huko Tibirizi, Chake Chake kisiwani Pemba.

Alisema mkulima akifikishiwa huduma ya umeme atazalisha mazao kwa gharama ndogo hali itakayosababisha bidhaa kuuzwa kwa bei ndogo kwa sababu atazalisha kwa gharama nafuu.

Waziri alisema Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi ameshatoa agizo nguzo za umeme zitolewe bure kwa wananchi, hivyo ZECO ihakikishe inawafikishia wananchi nguzo za umeme hasa wakulima ili wapate urahisi wa kuzalisha bidhaa zao.

"ZECO kwa nini mnachelewesha kufikisha nguzo za umeme kwa watu wanaozalisha bidhaa mbalimbali za chakula na matunda? Acheni kuzipigia hesabu gharama za nguzo, hizo peza si za mtu binafsi. Naagiza hizo nguzo kazifungeni haraka hata kama ziko tano zikafungwe maeneo ambayo watu wanazalisha bidhaa," alisema Kaduara.

Pia Waziri huyo aliwataka watendaji wa ZECO kuwajibika ipasavyo katika kuwahudumia wananchi wanaohitaji kufungiwa mita za umeme majumbani mwao wakati wameshalipa gharama zote za fedha zilizohitajika.

Alisema hali halisi ya ZECO ilivyo kwa sasa sio ya kusemwa vibaya lakini bado watendaji wa ZECO hawajawajibika ipasavyo hivyo endapo ataendelea kupata malalamiko ya wateja kwamba wameshalipa lakini ZECO hawajatimiza wajibu wao wa kuwafungia mita wateja watawajibika.

Pia alisema anafahamu wafanyakazi wa ZECO wanadai mishahara yao, hivyo ameagiza uongozi wa shirika hilo kuhakikisha kila mtu anapata haki yake anayodai pamoja na kupewa mwongozo wa majukumu yake ya kila siku kwa mujibu wa sheria na kanuni za utumishi.

Aliwataka watendaji wa ZECO kusimamia mapato ya huduma ya umeme na kujiepusha na vitendo vya kuhujumu uchumi na kuwasaka watu wanaojiungia umeme kinyume cha sheria.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Joseph Kilangi, aliwataka watendaji wa shirika hilo kutumia vizuri vifaa vya serikali, kufuata taratibu za ununuzi pamoja na kuongeza ushirikiano baina yao ili kuleta ufanisi katika majukumu yao.

Sambamba na hilo, aliwasisitiza wafanyakazi kujiepusha na utoro kazini na kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa katika kikao hicho kwa wakati ikiwamo kuwafungia wateja mita, nguzo za umeme kufikisha maeneo ya wakulima kwa wakati.

# Wakulima wa mwani wapigwa jeki vifaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu, imeikabidhi Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, vifaa kwa ajili ya wakulima wa mwani vyenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.58 vilivyonunuliwa kupitia fedha za Mfuko wa Uwezeshaji wa Ahuweni ya UVIKO-19.

**Makabidhiano hayo yanaipa nguvu zaidi kampuni ya uvuvi ya taifa ya mwani katika kusaidia kupeleka mbele gurudumu la uwezeshaji kwa wananchi wa Zanzibar.**

Akizungumza jana katika hafla ya makabidhiano ya vifaa hivyo iliyofanyika kwenye ofisi za Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Bluu Mjini Zanzibar, Waziri wa Wizara hiyo, Suleiman Masoud Makame, alisema vifaa hivyo vitasaidia kuongeza uzalishaji wa mwani.

Waziri huyo aliwataka wakulima wa mwani kutumia fursa ya mkopo wa ahueni ya UVIKO-19 ili kuimarisha hali zao za kipato kupitia ukulima huo.

Alisema licha ya wizara yake kutoa vifaa hivyo kwa wakulima wa mwani, pia inatarajia kutoa boti 400 kwa wakulima hao ili kulima kilimo hicho katika kina cha maji mengi baharini baada ya zao hilo kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

Naye Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shabani, alisema wizara yake imeanzisha kampuni ya mwani ambayo itasaidia kuongeza thamani ya zao hilo.

Alisema serikali inaendelea kujenga kiwanda cha kusarifu mwani huko Chamanangwe, kisiwani Pemba na kitakapokamilika, kitahitaji tani 30,000 za mwani, hivyo ni vyema wakulima kuongeza kasi ya uzalishaji kwa sababu mwani unaozalishwa kwa sasa ni tani 10,000 na wote unasafirishwa nje ya nchi.

Waziri huyo alisema pia kukamilika kwa kiwanda hicho kutawakomboa wakulima wa mwani ambao asilimia 90 wazalishaji ni wanawake kwa kuongeza thamani ya zao hilo.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Bluu, Aboud Suleiman Jumbe, alisema kupitia programu za utelelezaji wa kongamano la uchumi wa bluu chini ya fedha za UVIKO -19 ni pamoja na utengenezaji na utoaji wa boti 500 za mita tano za mwani na ununuzi wa vifaa vya mwani zikiwamo kamba na taitai kwa wakulima wa Unguja na Pemba.

Pia alisema wizara tayari imeshakamilisha ununuzi wa vifaa hivyo vyenye thamani ya Sh. 1,587,600,000 ambavyo vitawezesha uwekezaji na uwezeshaji katika kilimo hicho.

Alisema makabidhiano hayo yanaipa nguvu zaidi kampuni ya uvuvi ya taifa ya mwani katika kusaidia kupeleka mbele gurudumu la uwezeshaji kwa wananchi wa Zanzibar.

Jumbe alimpongeza Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kusimamia mchakato wa uwezeshaji wa kinamama katika uchumi wa bluu kupitia kilimo cha mwani.



Waziri wa Uchumi na Buluu na Uvuvi Zanzibar, Suleiman Masoud Makame (kulia) akikabidhi hati ya makubaliano ya utoaji wa vifaa vya mwani kwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shabani, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wizara yatoa agizo mitaala shule binafsi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa shule binafsi wameshauriwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na mafunzo ya Amali kufuata mitaala ya elimu itakayokidhi mahitaji ya elimu wanayoitoa.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Zanzibar, Abdallah Mohammed Mussa, aliyasema hayo jana katika sherehe za wanafunzi wa Shule ya Maandalizi ya Iqra Intergrated Academy zilizofanyika katika viwanja vya Kisonge mjini Unguja.

Alisema Wizara iko katika hatua ya kukamilisha upitiaji wa mtaala wa masomo ambao unashajihisha kujifunza kwa vitendo. Alisema hatua hiyo inakusudia kukuza na kuboresha huduma za kielimu kulingana na wakati uliopo sasa.

Mkurugenzi huyo alisema ili kuwa na usawa katika masuala ya elimu, wizara imeona umuhimu wa kuwa na mitaala inayokwenda na wakati ili masomo yanayotolewa yawe kwa vitendo na nadharia.

Alisema hatua hiyo pia itasaidia kutambua vipaji walivyo navyo watoto katika hatua za awali.

Pia aliipongeza Shule ya Iqra kwa kuwawezesha wanafunzi kusoma vizuri na kuwajenga katika kujiamini na kushiriki masuala mbalimbali yakiwamo ya michezo. Alisema kuwekeza katika elimu kwa watoto ni hatua nzuri kwa sababu samaki mkunje akiwa mbichi.

Naye Mkurugenzi wa Shule hiyo, Khadija Sadik Said, alisema masuala ya michezo kwa watoto ni muhimu hasa katika kumjenga kiakili kwa kufanya vizuri katika masomo.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Henry Natai, alisema wataendelea kufundisha wanafunzi kuwa wabunifu na kuwaandaa katika kujenga kielimu katika mafunzo ya nadharia na vitendo.



# Watu wenye VVU waahidi ushirikiano utafiti UKIMWI

**Na Richard Makore,** MWANZA

BARAZA la Taifa la Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (NACOPHA), limeahidi kushirikiana na wadau mbalimbali katika utafiti wa viashiria vya matokeo ya ugonjwa huo nchini.

Msimamo huo ulitolewa hivi karibuni jijini Mwanza na Ofisa Mtendaji Mkuu wa NACOPHA, Deogratius Rutatwa, katika uzinduzi wa mpango wa utafiti huo.

"Sisi tunaoishi na VVU tunaamini uwapo wa faida za papo kwa papo na za kimkakati zitokanazo na matokeo ya utafiti. Tunatarajia kuwa wakati utafiti ukiendelea washiriki wote watafaidika moja kwa moja kwa kupata huduma za ushauri na upimaji, matokeo ya haraka ya vipimo, huduma za rufaa za VVU pamoja na huduma nyingine zinazohitajika kutokana na matokeo ya kipimo," alisema Rutatwa.

**NACOPHA ipo tayari kushiriki kikamilifu katika hatua zote za kufanya utafiti na kuyafanyia kazi mapendekezo yatakayotokana na utafiti huo.**

Alisema, manufaa mengine ya utafiti huo ni pamoja na kuwashirikisha watu wanaoishi na VVU na Watanzania wote, hivyo kuwawezesha kutoa taarifa zao kuhusu shida mbalimbali wanazokutana nazo zikiwamo za unyanyapaa, ukatili wa kijinsia, kutofikiwa, kutopatikana na kushindwa kutumia huduma za UKIMWI zinazotolewa na serikali.

Pia, alizitaja faida zingine za utafiti huo ni pamoja na kuweka mazingira wezeshi na motisha kwa Watanzania na wanachama wa baraza hilo kushiriki katika kutoa michango yao inayolenga kuboresha mwitikio wa kitaifa wa UKIMWI.

Alisema manufaa mengine ya utafiti huo kwa wanaoishi na VVU ni pamoja na kuelewa uhusiano uliopo kati ya kuishi na VVU na magonjwa mengine kama vile kifua kikuu, homa ya ini, magonjwa yasiyoambukiza na athari zake kwao.

Rutatwa alisema, utafiti huo utawasaidia wao pamoja na wadau wengine wanaofanya kazi nao kupata taswira ya hali halisi ya viashiria vya kimkakati kwa makundi mbalimbali.

Alisema, hatua hiyo itasaidia kubuni na kutekeleza mikakati na afua zinazoongozwa na takwimu sahihi, kuwa na ufuatiliaji makini na kutoa mapendekezo muhimu kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma za mwitikio wa UKIMWI nchini.

Kupitia utafiti huo pia, alisema utakuwa ni fursa endelevu kwao katika jukumu lao la kutetea utoaji endelevu wa huduma bora za afya, utu na huduma za kinga kwa mujibu wa sera, mipango, mikakati, miongozo na mifumo ya sheria nchini.

Katika utafiti huo watapata fursa ya kupaza sauti zao kwa waandaaji wa programu, watoa maamuzi, watunga sera na wadau wa maendeleo katika utekelezaji wa afua za UKIMWI nchini, na wataongezewa uwezo wa kujiamini, kutetea na kuchangia katika utekelezaji wa maamuzi mbalimbali ya viongozi wa serikali yanayolenga kuboresha huduma ya afya na VVU.

Alisema, NACOPHA ipo tayari kushiriki kikamilifu katika hatua zote za kufanya utafiti na kuyafanyia kazi mapendekezo yatakayotokana na utafiti huo.

Aliishukuru wizara, wakala na idara za serikali kwa kujitoa kikamilifu katika kuwahudumia, kuwapa msaada wa kitaalamu, kuwashirikisha katika utafiti mbalimbali wa kundaa sera, miongozo na mikakati ya utoaji wa huduma katika ngazi ya jamii na vituo vya afya.



Baadhi ya wafanyakazi wa kampuni ya Tigo Tanzania, wakiwa kwenye matembezi kama sehemu ya uzinduzi wa wiki ya huduma kwa wateja 2022, jijini Mwanza juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walia na polisi kifo cha mtoto

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WAZAZI wa marehemu Hamis Mayunga (19), mkazi wa Dulisi wilayani Kishapu, anayedaiwa kuuawa kwa kupigwa risasi na mlinzi wa kampuni ya Samu Security, Emmanuel Chacha, katika mgodi wa almas wa El-Hilali alipoingia na wenzake wanne kuvua samaki katika bwawa la mgodi huo, wamedai polisi kumlinda mtuhumiwa.

Baba mzazi wa kijana huyo, Mayunga Inegele, akizungumza na Nipashe juzi nyumbani kwake wilayani Kishapu, alisema tangu tukio hilo la mauaji ya mtoto wake litokee, Mei 20, mwaka huu, mtuhumiwa hajakamatwa.



Aliomba serikali kumsaidia ili mtuhumiwa afikishwe katika vyombo vya sheria kwa kuwa kila anapofuatilia kwa jeshi la polisi mkoani Shinyanga kujua hatima ya kukamatwa kwa mtu huyo, hajawahi kupewa majibu yoyote.

"Mauaji ya mtoto wangu yalitokea Mei 20, mwaka huu, lakini cha kushangaza hadi leo eti mlinzi aliyehusika na mauaji haya bado hajakamatwa nina wasiwasi na utendaji kazi wa polisi na kila ninapofuatilia napigwa chenga tu, naomba haki itendeke," alisema.

Mama mzazi wa marehemu, Shinje Ntemanya, alisema kifo cha mwanaye kilimuuma na kuiomba serikali itende haki juu ya kifo hicho.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Sinyanga, Janeth Magomi (pichani), alikiri kutokea mauaji ya kijana huyo na kubainisha kuwa mlinzi anayetuhumiwa kusababisha mauaji hayo alikimbia kusikojulikana na mpaka sasa wanamtafuta.

Alisema, jeshi hilo halijalala bado linaendelea kumsaka na siku likimkamata atafunguliwa kesi na kisha kupelekwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

# Waziri abaini mbinu chafu wizi wa dhahabu

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

SERIKALI imebaini mbinu mpya ya wizi inayotumiwa na wafanyabiashara ya kushusha thamani madini ya dhahabu katika soko la ndani na kuyauza kwa bei kubwa nje ya nchi huku wakikwepa kulipa kodi stahiki.

Waziri wa madini, Dotto Biteko aliyasema hayo jana kwenye ufunguzi wa maonyesho ya tano ya teknolojia na uwekezaji kwenye sekta ya madini yanayoendelea kwenye uwanja wa Bombambili mjini Geita.

Biteko alisema, wanaoshusha thamani ya madini yakiwa sokoni na kuyauza kwa bei ya juu nje ya nchi huo ni uhujumu uchumi na kwamba serikali imeshabaini mbinu hizo.

"Utoroshaji wa madini huko tulishatoka kwa sababu serikali ilishapunguza kodi dhambi ya wizi ni dhambi tu niwaambie serikali inafuatilia kila mahali kuna mbinu siku hizi wachimbaji wanaitumia ya kushusha thamani ya madini tutawakamata na kuwachukulia hatua na sasa tukikukamata hatutangazi.

"Kama wewe unaona hakuna hatua..nenda kwenye soko la dhahabu lolote jaribu tu kutorosha hautashuka hata ngazi ya kwanza tayari tulishakukamata na tukikukamata tunakupiga faini mara tatu ya thamani ya madini uliyokamatwa nayo na chombo kilichotumika kutoroshea kinataifishwa na serikali," alisema.

Dk. Biteko, aliongeza kuwa serikali imepunguza kodi kwenye sekta ya madini hivyo hakuna sababu ya kujihusisha na utoroshaji unaweza kusababisha umaskini kwa wachimbaji kwa kupigwa faini na kutaifisha mali zao.

Waziri alisema hayo baada ya Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini mkoani Geita, Christopher Kadeo, kusema mkoa huo unakabiliwa na wimbi la utoroshaji wa madini, hivyo kuomba msaada kwa serikali kuthibiti utoroshaji huo.

"Kuna baadhi ya wachimbaji wadogo, mheshimiwa waziri wameanza kutorosha madini tunaomba msaada wa haraka kuthibiti hali hiyo ambayo inashika kasi sana ili kuwa na maendeleo ya nchi yetu," alisema.

# Utata kifo aliyekutwa na kanga shingoni

**Na Romana Mallya**

UTATA umeibuka kuhusu kifo cha mkazi wa Tabata Segerea jijini Dar es Salaam, Piariz Hiza (31) ambaye mwili wake unadaiwa kukutwa sakafuni chumbani kwake ukiwa hauna nguo, huku ukiwa na kipande cha kanga shingoni na kingine kikining'inia kwenye feni.

Akizungumza na Nipashe juzi, mdogo wa marehemu, Focus Hiza alidai taarifa za kifo cha dada yake alizipata Jumapili akiwa safarini akitokea Lushoto mkoani Tanga kwenda Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa jeshi hilo linaendelea na uchunguzi ili kubaini sababu za kifo hicho.

"Tunachunguza tukio hili, tunamhoji mume wake, maana kushikiliwa ni jambo lingine na kukamatwa ni jambo lingine. Mtu akipoteza maisha huwa tunahoji kujua sababu ya kifo ni nini, ukisema amenyongwa halafu taarifa ya daktari zikakuta kitu kingine, tunachunguza.

"Au ni sawa sawa unikute nimekufa, nina jeraha shingoni halafu ukasema kwa vyovyote nimeuawa. Hakuna mtu anajikata kisu anakufa, ni kupeleleza. Hii ndiyo njia nzuri ya kutenda haki, jambo hili linachunguzwa," alisisitiza.

Akisimulia kuhusu tukio hilo, mdogo wa marehemu, Hiza, alidai kuwa akiwa kwenye basi, alipigiwa simu na ndugu yake aliyeko Lushoto, akimjulisha kuhusu kifo cha dada yake ambaye alikuwa akiishi Tabata Segerea eneo la Kwa Bibi na hatua ya kwanza aliyochukua ni kupiga simu kwa msaidizi wa kazi za ndani wa dada yake aliyedai anaitwa Janeth.

"Janeth alipopokea akawa analia, nikamuuliza 'Janeth kuna shida gani?', akasema, 'dada kajiua', nikamuuliza 'kajiuaje?', akaniambia 'shemeji ametoka ndani analia, anasema 'dada yenu amejinyonga'. Nikamuuliza Janeth kama ameingia chumbani na kuuona mwili, akanijibu 'ndiyo, nimekuta dada amelala sakafuni' na alipofika nyumbani kwa dada yake, aliingia chumbani na kushuhudia alichokuwa amedokezwa.

"Niliwakuta askari polisi wameshafika nyumbani kwa shemeji lakini wakati ninafika walikuwa hata hawajaugusa (mwili), hawajafanya chochote.

"Nilimkuta dada kalala sakafuni, hana hata nguo, walikuwa hata hawajamfunika, tukamfunika, nimemkuta dada sehemu ya shingoni kuna kipande cha kanga kimefungwa na kingine kikiwa kinaning'inia kwenye feni," alidai.

Aliendelea kudai kuwa mwili wa dada yake aliuona ukiwa na majeraha ya kuviria damu maeneo ya kifuani na shingoni, akibainisha kuwa baada ya uchunguzi wa polisi nyumbani kwa dada yake, mwili ulichukuliwa kwa ajili ya uchunguzi zaidi.



Kaimu Mwenyekiti wa Chama cha TLP Taifa, Alhaji Omary Mkadam (wa pili kulia), akizungumza katika mkutano wa kupanga mikakati ya kuimarisha chama uliohusisha viongozi wa TLP Mkoa wa Dar es Salaam juzi. Wengine ni Katibu Mkuu wa chama hicho, Richard Lyimo (wa pili kushoto), Katibu wa Kitengo cha Wanawake Taifa, Maryam Kassim na Mwenyekiti wa chama Mkoa wa Dar es Salaam, Yustus Rwamugira. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Polisi yasema katibu hakuwa na uhusiano na mke wa Masanja

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limesema uchunguzi wa awali walioufanya kuhusu kifo cha Katibu wa Kanisa la Feel Free, Joas Steven anayedaiwa kujiua kwa kujinyonga, umeonyesha hakuwa na uhusiano wa kimapenzi na mke wa Emmanuel Mgaya, maarufu Masanja Mkandamizaji.

Joas alikuwa katibu wa kanisa hilo ambalo kiongozi wake ni Masanja.

Hivi karibuni katika mitandao ya kijamii kulisambaa taarifa za kifo cha Joas ambaye kabla ya kuchukua uamuzi huo anadaiwa kuandika ujumbe unaotaja sababu za kujiua ni uhusiano wa kimapenzi uliodaiwa kuwapo kati yake na mke wa Masanja aitwaye Monica.

Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, akizungumzia tukio hilo jana, alisema: "Ni kweli huyo mtu amepoteza maisha lakini ni kweli pia mazingira ya kupoteza maisha yanaonyesha amejiua kwa kujinyonga.

"Uchunguzi wa awali unaonyesha mawasiliano kwa njia ya simu kati ya aliyepoteza maisha na anayedaiwa ni mke wa Masanja, yanaonyesha huyo marehemu (Steven) akiwa anaomba, akiwa anataka uhusiano wa kimapenzi na huyu mtu ambaye inadaiwa ni mke wa Masanja.

"Pia ni kweli kabla ya tukio mke wa Masanja akiwa na mama mwingine ambao walikwenda nyumbani kwa marehemu kumweleza kwamba yule mke hataki message (ujumbe) za namna ile na hataki uhusiano naye, suala ambalo wao walilitimiza wakaondoka zao.

"Ni kweli pia yule mtu alifadhaika baada ya kuelezwa waziwazi kwamba yule ni mke wa mtu na hataki uhusiano naye."

Kamanda Muliro alisema mtitiriko wa visa hivyo unatoa nafasi ya kutokuwa na shaka na mazingira ya kifo chake.

Kamanda Muliro aliendelea: "Kwa mtu huyo bila shaka atakuwa amejinyonga kwa sababu mbalimbali za fikra zake au sababu nyingine yoyote lakini hata hivyo, bado pamoja na mazingira hayo Jeshi la Polisi haliwezi likaishia kwenye ushahidi wa awali ambao umeonekana.

"Mwisho huwa ni kufanya uchunguzi wa kitaalamu, wataalamu wa mwili kujua chanzo cha kifo ni nini."

Baada ya tukio hilo kusambaa mtandaoni Masanja kupitia ukurasa wake wamtandao wa kijamii wa Instagram aliandika: "Kila kazi ina gharama yake, acha tulipe gharama ya tulichoitiwa, ninakupenda mpaka pumzi yangu ya mwisho mke wangu, hili nalo litapita, tuombeeni nasi tunaomba, mtetezi wetu yu hai."

# Zumaridi, wenzake wana kesi ya kujibu

**Na Pelusy Yohana (SAUT)**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza, imemkuta na kesi ya kujibu Diana Bundala, maarufu kwa jina la Mfalme Zumaridi na wenzake wanane katika mashtaka matatu yanayowakabili, likiwamo la kumshambulia askari polisi na kumzuia ofisa wa serikali kufanya kazi.

Washtakiwa hao walikutwa na kesi ya kujibu jana mahakamani huko katika shtaka lao namba 10 la mwaka 2022.

Mahakama hiyo ilitoa uamuzi kuhusu washtakiwa hao baada ya kesi kuunguruma tangu Februari mwaka huu, upande wa mashtaka ukikamilisha ushahidi kwa kupeleka mashahidi 12 na vielelezo 11.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka matatu ambayo ni kusababisha majeraha ya mwili, kuzuia askari kutekeleza majukumu yao na kumzuia ofisa wa serikali kutekeleza majukumu yake.

Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Monica Ndyekobora, baada ya kutoa uamuzi huo, aliwapa nafasi upande wa utetezi kueleza namna watakavyowasilisha utetezi wao.

Upande wa utetezi katika kesi hiyo ukiongozwa na wakili, Erick Mutta, uliahidi kuwasilisha vielelezo 12 zikiwamo picha za video pamoja na mashahidi 30.

Ushahidi huo utasikilizwa kwa siku tano mfululizo kuanzia Oktoba 17 hadi Oktoba 21, 2022.

Akiwa mahakamani huko, Mchungaji Diana alisomewa shauri lingine linalomkabili katika mahakama hiyo linalohusu utumikishaji na kusafirisha binadamu.

Baada ya shauri hilo kusomwa, wakili wa upande wa mashtaka, Dorcas Akyoo, aliiomba mahakama hiyo ipange tarehe nyingine kwa ajili ya kesi hiyo kutajwa kwa kuwa upelelezi haujakamilika.

Wakili wa Utetezi, Erick Mutta aliuomba upande wa mashtaka kueleza hatua walizochukua ili kukamilisha upelelezi kwa kesi hiyo ambayo imekaa muda mrefu pasi na kusikilizwa.

Wakili Mutta, alidai kitendo cha kuchelewesha haki ya mtu ni sawa na kumnyima haki yake, kwamba mpaka sasa ni zaidi ya miezi saba imepita bila ushahidi kukamilika, akirejea kauli ya Rais Samia Suluhu Hasani ya kuzuia uendeshwaji wa kesi za jinai ambazo ushahidi wake haujakamilika.

Akijibu hoja hiyo Wakili wa Serikali, Dorcas Akyoo alidai serikali haiwezi kuweka wazi mwenendo wa upelelezi huo kwa kuwa ni kinyume cha sheria na kusisitiza kwamba kwa sasa upelelezi huo umefikia hatua nzuri.

Hakimu Monica Ndyekobora, aliueleza upande wa utetezi kuwa hakuna kifungu kinachomwelekeza kuwa anaweza kupeleka jalada la kesi ambayo haijakamilika kwa Hakimu Mfawidhi.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARTIN LYIMU IBOMA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HILUX** yenye usajili namba **T662 DGP.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**DSM/PHQ/RB/338063/2022**

## KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJI

**ISSA SUDI SALEHE** anatangaza kupotelewa kwa kadi za Bajaji aina ya **TVS KING** zenye; usajili namba **MC 531 ALB ,** CHASSIS NAMBA **MD6M14PK1D4L24779** NA ENGINE NAMBA **OK4LD1029286,** ya pili ina usajili namba **MC 390 AHH**, CHASSIS NAMBA: **MD614PK1C4A30873** na ENGINE NAMBA **OK4GB1051221** na ya tatu ina usajili namba **MC 574 BBR ,** CHASSIS NAMBA: **MD6M14PKD4A74394** NA ENGINE NAMBA: **OK4ADL103645**. Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**DSM/PHQ/RB/392846/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**SOSTHENES ALON MFUGALE,** Anatangaza kupotelewa kwa vyeti vya kidato cha nne (1) Dunda secondary school index **No.S.1969-0072** mwaka 2014, (2) alfagames Secondary school index **No.P.2517-0952** mwaka 2016,kitambulisho cha chuo(Tanzania Institute of Accountancy ) Reg **No.SGD/BHRM/19/67828,** result slip ya kidato cha sita ,kitambulisho cha ukarani wa sensa na cheti cha kuzaliwa C **No.10001700474,** vyote vimepotea pamoja na vyeti vya vifo vya marehemu Aron mfugale na Yosepha Kalinga ,pamoja na fomu ya **NIDA no.19960513671200000121. DSM/PHQ/RB/386484/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA.**
**Kituo cha NYALIKUNGU mkoa wa SIMIYU**
**Shauri la Madai/Ndoa Na.45/2022**
**Jina la Mdai: MICHAEL DAUD**
**Jina la Mdaiwa:JULIETH MAKOYE.**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa JULIETH MAKOYE WA MWATULOLE-GEITA**
**KK :MWENYEKITI WA MTAA, MWATULOLE-GEITA**
**KK:HAKIMU MFAWIDHI,MAHAKAMA YA MWANZO, GEITA-MJINI.**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao(Eleza hapa habari za Madai)Mdai talaka kwa Mdaiwa ambaye ni Mke wangu hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 07 Mwezi 10 Mwaka 2022 saa 8:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hatohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini ,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 03 Mwezi 10 Mwaka 2022.

HAKIMU

**Hakimu**
**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU**

**MAHAKAMA YA WILAYA YA SINGIDA**
**MKOA WA SINGIDA**
**HATI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI Na 32/2022**
**OMBI LA ANNA REUBENI KIOGHO KUTEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU CHRISTINA JINGU TUNDUU**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote wa mirathi ya marehemu **CHRISTINA JINGU TUNDUU** wanaalikwa kuja mahakamani kuhudhuria kesi mnamo Tarehe 19 mwezi 10 mwaka 2022, kabla ya mwombaji huyo hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

**Tarehe 04/10/2022**

Tarehe 04/10/2022
Hakimu Mkazi
Mahakama ya Wilaya Singida

## KUPOTEA KWA CHETI



**GODLISTEN DICSKON LEMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0919-0074** kilichotolewa na baraza la mitihni la taifa kupitia **NDURUMA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DSM/PHQ/RB/393275/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**HADIJA SAIDI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1778-0028** kilichotolewa na Baraza La Mitihani La Taifa kupitia **KIRONGWE SECONDARY SCHOOL** mwaka **2009.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/MBA/RB/185586/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo KAWE wilaya ya KINONDONI**
**Kituo cha KAWE Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la madai/Ndoa Na. 340 ....2022**
**Jina la mdai ELIZABETH TITUS MUNTHALI**
**Jina La Mdaiwa KASSIM WILLIAM MLAY**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za Taratibu Madai katika Mahakama za mwanzo)**

**Kwa kuwa mdai/wadaiwa ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za madai)**

**KUJIBU KESI YA MADAI Tsh 2,800,000/=**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 25 mwezi 10 mwaka 2022 saa 2:30 Asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta/shahidi mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.

**Angalizo:** kama hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hai ya kuitwa shaurini. Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo. Hati hii imetolewa kwa Amri na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 04 mwezi 10 mwaka 2022

HAKIMU

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KAWE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RICHARD DANIEL NDOSSI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T933 CWY, CHASSIS NAMBA: DA62T-320271** na **ENGINE NAMBA: K6A-5304895.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/393573/2022**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**MASIGE DEUS MASIGE**
Anatangaza kupotelewa kwa kadi za pikipiki zenye namba za usajili **L7GPCKLY0M1051021/L7GPCKLY8L1032134/L7GPCKLY1L1028975/L7GPCKLY9M1051003/LZL15P901KHM56542,** yeyote atakae ziona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0772970974.**
**DSM/PHQ/RB/292929/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KUSIRIE ROBERT LEMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 652 DEL – NISSAN CARAVAN.** Chassis namba **VWGE24001477.** Engine namba **QD32014237.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/320740/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**

**WILAYA YA MJINI MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......68/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: CHRISTOPHER. M. MWALITAGETE WA MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA MAGNET ANANGISYE**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 06 Mwezi 10 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 03 mwezi 10 mwaka 2022

**HAKIMU MFAWIDHI**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# PUMU KALI CHANZO KIFO CHA COOLIO

**LOS ANGELES, Marekani**

MARAFIKI wa rapa wa Marekani, Coolio wanafikiri "pumu kali" (asthma), inaweza kuwa imechangia kifo chake, kwa mujibu wa TMZ.com, kwani ilikuwa ikimsumbua kwa miaka mingi.

Vyanzo vya habari vililiambia gazeti la Page Six Jumatatu kwamba, rapa huyo wa kibao cha "Gangsta's Paradise" "alipambana" na puku kali kwa miaka mingi na kwamba wachunguzi wa kifo chake wamearifiwa kuhusu hilo.

Coolio alifariki duniani Septemba 28, mwaka huu baada ya kukutwa akiwa amepoteza fahamu kwenye sakafu ya bafuni ya nyumbani kwa rafiki yake huko Los Angeles, Marekani. Alifariki akiwa na umri wa miaka 59.

Sababu rasmi ya kifo bado haijatolewa, lakini ripoti za awali zinashuku kuwa alikuwa amepatwa na mshtuko wa moyo.

Utafiti uliochapishwa na Chama cha Utafiti wa ugonjwa wa Moyo cha Marekani unaonyesha kwamba, watu wenye pumu ya kudumu wanaweza kuwa katika hatari kubwa ya kupata mshituko wa moyo na kufariki dunia.

Licha ya hali yake ya kiafya, Coolio alionekana akiendelea kufanya maonyesha ya muziki mara kadhaa siku chache kabla ya kifo chake, kwa kuweza kuimba mfululizo kwa dakika 30 hadi 40.

Coolio aliendelea kutumbuiza siku chache kabla ya kifo chake. Katika picha za video kutoka kwenye ziara yake aliyoipa jina la "I Love the '90s", "West Up!" rapa huyo alionekana mwenye nguvu huku akicheza jukwaani kwa furaha.

Mashabiki pia walibainisha hapo awali kwamba Coolio alionekana mwenye "furaha sana" huku akipiga picha na kucheza na mashabiki wake walipokutana naye chini ya wiki moja kabla ya kifo chake.

Montell Jordan, ambaye alikuwa kwenye ziara na rapa huyo siku chache kabla ya kifo chake, pia aliliambia gazeti la Page Six kwamba hangeweza kutarajia kwamba kifo cha rafiki yake wa muda mrefu kilikuwa karibu.

Coolio ameacha jumla ya watoto 10, sita akiwa amezaa na mke wake wa zamani, Josefa Salina, ambaye alimuoa mwaka 1996 kabla ya kuachana.

## HARMONIZE AWAKATAA 'MACHAWA'

**Na Mwandishi Wetu**



NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva, Harmonize ameonekana kutupa kijembe cha kuwakataa 'machawa'.

Kupitia kibao chake kipya alichokiachia juzi, amesema kuwa hawahitaji machawa kwenye maisha yake.

Ngoma hiyo mpya ameipa jina la 'LeaveMeAlone' akimshirikisha mwanadada, Abby Chams.

Harmonize ameonekana kufikisha ujumbe wake huo akiwataka watu wamuachie maisha yake peke yake. Katika kibao hicho, amesema hawataki Mwijaku, H Baba wala Baba Levo, kwani akimpenda Mungu inatosha.

Harmonize kwa nyakati tofauti amekuwa karibu na mtangazaji Mwijaku huku msanii wa Bongo Fleva, H Baba akijiondoa kwake na kwenda kuungana na Baba Levo kumsapoti Diamond Platinum.

## ZUCHU ANOGESHA BIRTHDAY YA DIAMOND



**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Jumapili ya Oktoba 2, mwaka huu nyota wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz aliadhimisha siku yake ya kuzaliwa ambapo bosi huyo wa WCB alisherehekea kutimiza miaka 32, Zuchu alionyesha hisia kali kwa ujumbe mzito.

Watu wengi wakiwamo mashabiki, familia, marafiki wa karibu na wasanii wenzake walitumia siku hiyo kumsherehekea.

Zuchu, ambaye anadaiwa kuwa kwenye mapenzi na Diamond, alisema kuwa kila siku angependa kumkumbuka bosi wake huyo kama Mcha Mungu sana.

"Biggy, ishi kwa muda mrefu. Chapisho la pili ni jinsi ninavyotaka kukukumbuka kila siku," aliandika kwenye Instagram.'

Zuchu aliambatanisha ujumbe wake na video iliyomuonyesha Diamond akifanya sala ndani ya chumba chake.

Pia Zuchu ambaye ni mtoto wa Malkia wa Mipasho, Khadija Kopa aliwaaomba mashabiki wake wamwimbie Diamond wimbo wa 'Happy Birthday' wakati akitumbuiza usiku wa kuamkia siku yake ya kuzaliwa.

"Yeye ni mtu maalum sana kwangu. Nitamtumia video hii. Nataka mnisaidie kumuimbia shujaa wangu 'Happy Birthday'. Yeye ni shujaa wangu. Yeye ndiye shujaa wangu pekee," alisema kabla ya kuongoza umati kuimba wimbo 'Happy Birthday.

# AZAM SASA YAANZA TAMBO, KUWAFUATA WALIBYA KESHO

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Singida Big Stars juzi, Azam FC imeanza tambo ikidai mechi hiyo ndiyo ilikuwa bora zaidi kuliko zote kwenye raundi ya sita ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Afisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia 'Zaka Zakazi', amesema kasi ya mchezo huo, ubora wa vikosi vyote viwili pamoja na ufundi wa wachezaji, umeifanya mechi hiyo kuwa ndiyo bora zaidi kwenye raundi ya sita, huku akifurahia ushindi pamoja na kuwafunika Wabrazil.

"Tunafurahi tumeshinda na kwenye mechi hii waamuzi wamejitahidi, si kwa sababu tumeshinda, kuna watu wanadhani kuwa mimi nalalamika tu nikishinda, lakini ukitazama hata mechi dhidi ya Kagera Sugar na Mbeya City tulishinda, lakini tulilalamikia maamuzi.

"Mechi dhidi ya Yanga tulitoka sare, nayo pia tulilalamika kwa hiyo siyo mpaka tufungwe, tunalalamika pale tunapoona tumeonewa bila kujali matokeo," alisema Zaka Zakazi.

Zaka aliendelea na vijembe vyake kwa viongozi wa Singida Big Stars kuwa wachezaji wa Kibrazil walionekana kufurahi sana walipofika Uwanja wa Azam Complex kiasi cha kupiga picha.

"Kwanza kabisa niseme kuwa kwenye hii raundi ya sita, hii ndiyo ilikuwa mechi bora sana, ufundi wa hali ya juu kwa wachezaji wa timu zote mbili, kasi, mbinu na ufundi, niliwaona wale Wabrazil walifurukuta, lakini tuliwadhibiti, na mechi ilipokwisha walionekana kufurahi sana kuona uwanja mzuri wa Azam Complex, wakawa wanapiga picha, hapa ndipo inafaa pawe kwao, ila nilivyosema tunawahitaji viongozi wa Singida Big Stars walinijibu kuwa watawauza pale watakapopewa Uwanja wa Azam Complex, tunasubiri dirisha dogo, wale ni wa kucheza Kombe la Shirikisho hatua ya makundi," alisema.

Wakati huo huo, kikosi cha timu hiyo kinatarajia kuondoka nchini kesho kwenda nchini Libya kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho dhidi ya Al Akhdar SC unaotarajiwa kuchezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Martyrs of Februari nchini humo. Zaka alisema wanakwenda huko wakiwa na lengo la kufanya vema kwenye mechi hiyo ugenini ili kujiweka kwenye mazingira mazuri katika mchezo wa marudiano.

**WAWA KAZINI...**



Beki wa kati wa Singida Big Stars, Pascal Wawa, akifanya mazoezi katika Uwanja wa Uhuru huku wachezaji wenzake, Amissi Tambwe (kushoto) akijiandaa kwa kuvaa viatu na beki Mghana Biemes Carno akiendelea kufuatilia kinachoendelea uwanjani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwamnyeto: Bao limenipa morali Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

NAHODHA wa Klabu ya Yanga, Bakari Mwamnyeto, amesema amefarijika kuwa miongoni mwa wafungaji walioipa timu hiyo ushindi wakati ikiichapa Ruvu Shooting mabao 2-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi.

Bao lingine la Yanga katika mchezo huo, lilifungwa na Feisal Salum 'Fei Toto', hivyo kuifanya timu hiyo iendelee kushika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 13 sawa na Simba iliyopo kileleni kutokana na tofauti kubwa ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mwamnyeto alisema msimu huu ukipata nafasi ya kufunga unapata matumaini kikosini kutokana na ushindani wa namba uliopo.

"Nimepata faraja kufunga goli langu la pili msimu huu, tunafahamu ugumu wa ligi yetu, hivyo ukipata nafasi kama hiyo inazidi kukupa hamasa ya kuipambania timu," alisema Mwamnyeto.

Alisema baada ya kuiwezesha timu yake kupata pointi tatu dhidi ya Ruvu Shooting, sasa anaelekeza nguvu kwenye mchezo wao wa kimataifa dhidi ya Al Hilal ya Sudan, utakaopigwa Oktoba 8, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Kwa sasa akili yangu ninaielekeza kwenye mchezo wetu wa Ligi ya Mabingwa Afrika, lengo ni kuipa mafanikio timu yangu kwenye uwanja wa nyumbani," alisema nahodha huyo ambaye katika nafasi ya beki wa kati amekuwa akipata wakati mgumu wa kuanza kikosi cha kwanza dhidi ya Dickson Job na Yannick Bangala.

Alisema atashirikiana na wachezaji wenzake kufuata maelekezo wanayopewa na benchi lao la ufundi ili wapate matokeo mazuri Jumamosi dhidi ya Al Hilal.

Mwamnyeto alisema mchezo huo unatarajiwa kuwa mgumu na wenye ushindani na kudai wataingia uwanjani kwa tahadhari kubwa.

Endapo Yanga itapata matokeo ya jumla katika mchezo huo na ule wa ugenini Oktoba 16, mwaka huu, itafuzu hatua ya makundi na timu itakayotolewa itaangukia mechi za mchujo za Kombe la Shirikisho ili kuwania kufuzu hatua ya makundi ya kinyang'anyiro hicho cha pili kwa ubora na utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

# Mil. 300/- walizopigwa wasanii zarejeshwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KAMATI maalum ya kutetea haki za wasanii imefanikisha kurejeshwa kwa Sh. milioni 300 ambazo wasanii walikuwa wamedhulumiwa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania, Dk. Kiagho Kilonzo, alisema kamati hiyo iliyoundwa na waziri mwenye dhamana na mambo ya sanaa nchini, hadi sasa imeshapokea malalamiko 30 na kuyashughulikia.

"Takriban Sh. milioni 300 zilizokuwa zimedhulumiwa zimesharejeshwa kwa wasanii. Malalamiko 22 yamesuluhishwa, na nane yapo katika hatua mbalimbali za kushughulikiwa,"alisema.

Alibainisha kuwa baadhi ya malalamiko yaliyopokelewa na kushughulikiwa ni yale ya marehemu Amri Athumani (King Majuto), marehemu Steven Kanumba, msanii David Ganzi (Young Dee) na Mzalishaji wa Tamthiliya ya Samwel Isike.

# Coastal yajipa mechi 8 Ligi Kuu

**Na Hadija Mngwai**

TIMU ya Coastal Union ya jijini Tanga, imejipa mechi nane kuweza kupata tathimini yao juu ya hatma yao katika mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Bara.

Coastal Union ambayo ipo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara imecheza mechi sita hadi sasa ikishinda michezo miwili na kutoa sare moja huku ikipoteza mitatu hivyo kujikusanyia pointi saba.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa Coastal Union, Jonathan Tito, alisema wanahitaji muda kuweza kukaa sawa na kuona mwelekeo katika mzunguuko wa kwanza wa ligi hiyo.

"Kikosi chetu kipo vizuri, kwa sasa bado ni mapema mno kuweza kufanya tathimini ya timu kwa kuwa ndio kwanza mechi ya sita sasa tumecheza.

"Kwa bahati mbaya timu haikupata muda wa kupumzika, tumemaliza ligi kisha tukakaa kidogo na kurudi kuandaa timu kwa ajili ya msimu mpya, hivyo ni mapema mno kusema kama timu yetu ipo vibaya ama ipo vizuri. Tunahitaji kuona angalau mechi nane au tisa kupata mwelekeo wa timu yetu katika mzunguuko wa pili," alisema Tito.

## ZISIKUPITE

### RONALDO KUONDOKA JANUARI
MSHAMBULIAJI wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, ataruhusiwa kuondoka Manchester United Januari. ***(Telegraph)***

### MARTINELLI ATAKIWA CHELSEA
CHELSEA wanaaminika kumfuatilia mshambuliaji wa Arsenal na Brazil, Gabriel Martinelli mwenye umri wa miaka 21. ***(Mail)***

### SAKA MSHAHARA MNONO
ARSENAL wamempa ofa mshambuliaji wa England, Bukayo Saka ya mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki, ili nyota huyo mwenye umri wa miaka 21, aongeze muda wa kubakia katika klabu hiyo. ***(Football.london)***

### CHELSEA YATAKA WA2 LEIPZIG
MBALI na mazungumzo na RB Leipzig kuhusu kumsajili fowadi wa Ufaransa, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 24, Chelsea pia wanajadili kumsajili beki wa kati wa Croatia, Josko Gvardiol mwenye umri wa miaka 20 kutoka klabu hiyo ya Ujerumani. ***(90 Min)***

### MENDY ATATHIMINIWA CHELSEA
CHELSEA pia watatathmini hali ya walinda lango katika klabu hiyo miezi ijayo, huku nyota wa kimataifa wa Senegal, Edouard Mendy mwenye umri wa miaka 30 akiwa bado hajasaini mkataba mpya. ***(Telegraph)***

### HAG ACHIMBA BITI UNITED
KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag ameuambia uongozi wa klabu hiyo kutompa mchezaji yeyote mkataba mpya hadi atakapofanya uamuzi wa nani anastahili. ***(Telegraph)***

### SALIBA MKATABA MPYA
MLINZI wa Ufaransa, William Saliba amethibitisha kuwa wawakilishi wake wamezungumza na Arsenal kuhusu kusaini mkataba mpya. ***(90 Min)***

### XAVI AFUNGUKA YA MESSI
KOCHA wa Barcelona, Xavi amesema "si wakati" wa kumzungumzia fowadi wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 35, kurejea katika klabu hiyo na "nataka atulie kwa amani" ili kufurahia muda wake kule Paris St-Germain. ***(ESPN)***

### EDWARDS, O'NEIL WATAJWA
ALIYEKUWA kocha wa Watford, Rob Edwards na bosi wa muda wa Bournemouth, Gary O'Neil wako katika harakati za kuchukua nafasi ya Chris Wilder aliyetimuliwa kama kocha Middlesbrough. ***(Football Insider)***

### RHYS ANAWANIWA PALACE
KLABU za Bournemouth, Crystal Palace na Leicester City zinamfuatilia mchezaji wa Sheffield United mwenye umri wa miaka 23, Wales Rhys. ***(Football Insider)***

### WILSON AONGEZEWA NEWCASTLE
NEWCASTLE wamekubali kuongeza mkataba wa miaka miwili na mshambuliaji wa England, Callum Wilson mwenye umri wa miaka 30. ***(90min)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DIJK AKIRI MAMBO MAGUMU KWA LIVERPOOL

Tunacheza katika ligi bora zaidi duniani, ambapo timu zote ni bora na zinaweza...

**LIVERPOOL, England**

MLINZI wa Liverpool, Virgil van Dijk amekiri kwamba, timu hiyo lazima ikumbuke jinsi ya kucheza kwa furaha na uhuru baada ya kuanza vibaya msimu huu.

Liverpool mwishoni mwa wiki haikuwa na matokeo mazuri baada ya kulazimishwa sare ya mabao 3-3 na Brighton nyumbani.

Vijana hao wa kocha Jurgen Klopp kwa sasa wapo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu wakiwa na pointi 10 pekee katika michezo saba - pointi 11 nyuma ya vinara wa ligi hiyo, Arsenal ambao wamecheza mchezo mmoja zaidi.

Wachezaji wengi wa Liverpool wamekabiliwa na ukosoaji kwa uchezaji wao mbaya msimu huu, akiwamo Van Dijk, na Mholanzi huyo amekiri kwamba wamepata ugumu wa kuwa na mwanzo mbaya.

"Kiwango bora mfululizo ndio sehemu ngumu zaidi ya soka," alisema Van Dijk.

"Lazima mfanye hivyo pamoja, na kukabiliana na vikwazo pamoja, na kuendelea kufanya mambo yale yale mnayotaka kufanya. Ni wazi kwamba tumekuwa na vikwazo, na ni vigumu kuitikia kwa njia sahihi ikiwa hauko katika umbo bora zaidi.

"Lakini nina imani kuwa tutakua. Ni nini? Miezi minne iliyopita tulikuwa tunachezea mataji yote, sasa hatuko kwenye wakati mzuri...lakini tutafika."

Alipoulizwa kama Liverpool bado walikuwa na wasiwasi kutokana na kushindwa katika harakati zao za kutaka mataji manne msimu uliopita, Van Dijk alisisitiza kwamba hakuna uhusiano wowote na kile kinachoendelea msimu huu.

"Halihusiana na hilo," alisisitiza.

"Na timu ni dhahiri zinakuwa bora, tunacheza katika ligi bora zaidi duniani, ambapo timu zote zinaweza kushindana na lazima turudi kwenye msimamo huo, na kucheza kwa furaha na uhuru. Lakini yote huanza kwa kuifanya pamoja na kufanya kazi kwa bidii."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,037,3

MECHI KALI

BENFICA
VERSUS
PARIS ST GERMAIN

1 | 3.87
X | 3.97
2 | 1.75

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SALIBA AANZA MAZUNGUMZO YA MKATABA MPYA ARSENAL

**LONDON, England**

WILLIAM Saliba amethibitisha kuwa wawakilishi wake wamezungumza na Arsenal kuhusu kusaini mkataba mpya, kwa mujibu wa 90min.

Mfaransa huyo amekuwa bora msimu huu na amevutia watu wengi kutoka Ulaya kwani amebakiza zaidi ya miezi 18 katika mkataba aliosaini alipojiunga na 'Washikabunduki' hao mwaka 2019.

Mtandao wa 90min ulifichua mapema msimu huu wa majira ya joto kwamba Arsenal walikuwa wakitayarisha mazungumzo na Saliba juu ya kuongeza muda, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, sasa amethibitisha kuwa mazungumzo yamefanyika.

Alipoulizwa kuhusu hali ya mkataba wake, Saliba alijibu: "Ndio, tutaona. Wanazungumza kidogo. Tutaona."

Moja ya matokeo bora ya msimu huu ya Saliba kufikia sasa ni katika mchezo wa Jumamosi iliyopita, ambapo aliisaidia Arsenal kupata ushindi mnono wa mabao 3-1 dhidi ya Tottenham Hotspur kwenye dabi ya timu za London Kaskazini.

Baada ya mchezo huo, Saliba alifichua jinsi kocha Mikel Arteta alivyomsaidia kumshawishi kurejea Arsenal msimu huu wa majira ya joto baada ya muda wake mzuri wa mkopo akiwa kule Marseille.

"Alizungumza kuhusu msimu wangu wa mwisho na alielezea mradi wa msimu huu," alisema Saliba kuhusu mazungumzo yake na kocha huyo.

"Tunaposhinda, ndivyo tunavyojiamini. Tunataka kila wiki kushinda, kushinda, kushinda - na ndio hivyo.

"Ilinibidi kusubiri kwa muda mrefu kwa dabi yangu ya kwanza ya Kaskazini mwa London. Lakini nilifurahia tangu dakika ya kwanza hadi mwisho, na sasa nina furaha sana. Sasa tunacheza dhidi ya wachezaji bora zaidi duniani. Ni nzuri kwa wachezaji wachanga kama mimi na ninajifunza mengi."




# Chelsea yakomaa na Nkunku

**LONDON, England**

CHELSEA wapo kwenye mazungumzo na RB Leipzig juu ya makubaliano mawili ya kuwanunua Christopher Nkunku na Josko Gvardiol, kwa mujibu wa 90min.

'The Blues' hao walishuhudia uhamisho wa beki wa kati Gvardiol ukirudishwa nyuma hadi mwishoni mwa dirisha la usajili la majira ya joto, ambapo Nkunku alifanyiwa uchunguzi wa kimatibabu chini ya uangalizi wa Chelsea kwa lengo la kumsajili mwaka 2023.

Vyanzo vimeithibitishia 90min kwamba, njia za mawasiliano za Chelsea zimebaki wazi na Leipzig tangu msimu wa majira ya joto na mmiliki mwenza, Todd Boehly anatazamia



kumaliza usajili wa wachezaji wote wawili haraka iwezekanavyo.

Baada ya kuona Chelsea ikikosa kumsajili Aurelien Tchouameni mwaka 2021 na kujikuta ikiingia kwenye sakata ndefu la kumnunua Wesley Fofana msimu huu wa majira ya joto, inafahamika kwamba Boehly ana nia ya kufanya biashara yake ya uhamisho mapema iwezekanavyo.

Masharti kibinafsi yamekaribia kuafikiwa kikamilifu kati ya Chelsea na Gvardiol na Nkunku, na sasa kipaumbele cha Boehly ni kujaribu kuwashawishi Leipzig kukubali mauzo mara moja.

Chelsea inatumaini kuwa usajili wa wachezaji wote wawili utakamilika kabla ya Kombe la Dunia, ingawa Leipzig wanaweza kusita kuwaachia kuondoka wachezaji wawili.

'The Blues' wanatafuta kuzuia kipengele cha kuachiwa kwa mchezaji mmoja mmoja, ambacho kinapaswa kulipwa kikamilifu, na badala yake wanafuata makubaliano na Leipzig juu ya usajili wote wawili, jambo ambalo linaongeza utata katika mazungumzo.

HABARI MICHEZO

361,877/-

# VIPIGO LIGI KUU VYAMUONDOA KOCHA MKUU TAIFA JANG'OMBE

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Taifa Jang'ombe imeachana na Kocha wake Mkuu, Muhammed Seif 'Kocha King' baada ya timu hiyo kuendelea kupata matokeo mabaya kwenye Ligi Kuu Zanzibar.

Taifa Jang'ombe imecheza michezo mitano na kutoka sare miwili na kufungwa mitatu hadi sasa msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Afisa Habari wa timu hiyo, Haji Kiduka, alisema sababu kubwa ya kuondoka kocha huyo ni timu hiyo kuendelea kupata matokeo mabaya tangu kuanza kwa Ligi Kuu msimu huu.

Alisema, kocha huyo hajaipa mafanikio timu kwa kipindi kifupi tangu alipoanza kuinoa Taifa Jang'ombe mapema msimu huu.

Kiduka alisema, lengo la kila uongozi wa klabu ni kuona katika michezo ya awali timu inafanya vizuri ili kujiweka nafasi nzuri kwenye mzunguko huo wa kwanza kabla ya kwenda dirisha dogo ambapo timu nyingi zinafanya usajili wa kuziba mapengo waliyoyaona mzunguko wa kwanza. Pia, alisema kumekuwa na makelele mengi kutoka kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo ya kutofurahishwa na mwenendo wa timu hiyo kwa kuambulia vipigo kila wanaposhuka uwanjani.

"Timu yetu haijawahi kupata matokeo mazuri tangu kuanza msimu huu wa ligi, na malengo yetu yalikuwa mengi mno hasa mzunguko wa kwanza kuhakikisha tunafanya vizuri, lakini imekuwa tofauti hatujawahi kushinda, tumeendelea kupata matokeo mabaya hii ndio sababu mwalimu akaondoka," alisema.

Aidha, alisema timu hiyo hivi sasa ipo chini ya kocha msaidizi na ipo mbioni kutafuta kocha mkuu wa kuinoa ili ipate mafanikio.

Taifa Jang'ombe inashika nafasi ya pili kutoka mkiani ikiwa na alama mbili wakati huu ikitarajiwa kushuka tena dimbani Jumapili wiki hii kuvaana na Malindi, mchezo utakaopigwa Uwanja wa Amaan.

## CHUMA HICHO...




Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto', akiifungia timu yake bao la kwanza wakati ikishinda 2-1 dhidi ya Ruvu Shooting kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Simba SC yakwepa figisu za Waangola

INATOKA UK. 32

mazuri.

Alisema wanakumbukumbu yaliyowatokea Namungo FC wakati walipokwenda kuchezo nchini Angola na wapinzani wanaokutana nao Jumapili.

"Hatutaki kukutana na kile kilichowapata Namungo FC, kabla ya timu kwenda Angola Jumamosi, tayari watu wetu maalum wametangulia nchini humo kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya kufikia timu, sehemu ya mazoezi na usafiri kutika uwanja wa ndege hadi hoteli tutakayofikia," alisema mjumbe huyo.

# Nabi atetea Mayele kushindwa kutetema

INATOKA UK. 32

dhidi ya Al Hilal ya Sudan.

Naye Kocha wa Ruvu Shooting, Boniface Mkwassa, alisema wachezaji wake wamepambana na kuwapongeza Yanga kwa uzoefu mkubwa waliotumia kuweza kupata matokeo hayo.

Alisema mchezo una matokeo matatu, hivyo wamekubaliana na kilichotokea na hana wa kumlaumu kwa sababu walifanya makosa mapema katika kipindi cha pili na Yanga kufanikiwa kupata ushindi huo.

"Makosa machache ya safu yangu ya ulinzi ndiyo yametukwamisha, mipango yetu ilikuwa kuwazuia Yanga na kutowaruhusu kupanda, hata hivyo, licha ya kupoteza wachezaji wangu wamepamba na tulifanikiwa katika mbinu zetu za kutoruhusu bao katika kipindi cha kwanza na kuhitaji kuzuia hadi wale waliosubiri kutetema hawakutetema," alisema Mkwassa.

Alisema baada ya mchezo huo wameona mapungufu yao na sasa wanaenda kujipanga kwa mchezo ujao kuhakikisha wanapata matokeo mazuri kama ilivyo kwa michezo yao miwili iliyopita kabla ya kukutana na Yanga.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 08/10/22 | 17:00 | Millwall vs Middlesbrough | 2.63 | 3.13 | 2.73 |
| 02. 08/10/22 | 17:00 | Swansea vs Sunderland | 2.33 | 3.28 | 3.03 |
| 03. 08/10/22 | 17:00 | Wigan vs Cardiff | 2.35 | 3.18 | 3.08 |
| 04. 08/10/22 | 17:00 | Birmingham vs Bristol City | 2.59 | 3.24 | 2.69 |
| 05. 08/10/22 | 19:30 | Brighton vs Tottenham | 2.90 | 3.35 | 2.37 |
| 06. 08/10/22 | 19:30 | Sevilla FC vs Athletic Bilbao | 2.69 | 3.19 | 2.64 |
| 07. 08/10/22 | 22:30 | Pacos Ferreira vs Vitoria Guimaraes | 3.00 | 3.10 | 2.48 |
| 08. 09/10/22 | 14:00 | Huddersfield vs Hull City | 2.36 | 3.33 | 2.93 |
| 09. 09/10/22 | 15:00 | Valladolid vs Betis | 3.03 | 3.33 | 2.30 |
| 10. 09/10/22 | 16:00 | Salernitana vs Verona | 2.53 | 3.37 | 2.68 |
| 11. 09/10/22 | 16:00 | Udinese vs Atalanta | 2.63 | 3.37 | 2.58 |
| 12. 09/10/22 | 16:00 | Angers vs Strasbourg | 2.44 | 3.33 | 2.78 |
| 13. 09/10/22 | 17:15 | Cadiz CF vs Espanyol | 2.88 | 3.18 | 2.48 |
| 14. 09/10/22 | 18:30 | Arsenal vs Liverpool | 2.64 | 3.45 | 2.53 |
| 15. 09/10/22 | 18:30 | Hertha BSC vs SC Freiburg | 3.02 | 3.41 | 2.25 |
| 16. 09/10/22 | 19:30 | Real Sociedad vs Villarreal | 2.53 | 3.23 | 2.78 |
| 17. 09/10/22 | 20:30 | Stuttgart vs Union Berlin | 2.61 | 3.15 | 2.71 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 05/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1509 | Omiya Ardija vs Montedio Yamagata | 3.48 | 3.28 | 1.97 |
| 13:00 | 2878 | Bahir Dar Kenema FC vs Wolkite City FC | 1.57 | 3.49 | 5.63 |
| 13:00 | 3323 | Daegu vs FC Seoul | 2.42 | 3.20 | 2.67 |
| 13:00 | 3418 | Akzhaiyk Uralsk vs FK Arys | 2.14 | 2.97 | 3.36 |
| 13:00 | 3928 | Ulsan Hyundai vs Jeonbuk Hyundai | 2.03 | 3.24 | 3.34 |
| 13:00 | 5429 | Daejeon Citizen vs Jeonnam Dragons | 1.74 | 3.55 | 4.09 |
| 13:30 | 2430 | Kyoto Sanga vs Sanfrecce Hiroshima | 4.49 | 3.56 | 1.68 |
| 13:30 | 3046 | Chungnam Asan vs Seoul E Land | 2.12 | 3.21 | 3.16 |
| 14:00 | 4005 | Lech II Pozna vs Pogon Siedlce | 1.97 | 3.50 | 3.26 |
| 14:30 | 1167 | Shanghai SIPG vs Beijing Guoan | 1.81 | 3.54 | 3.79 |
| 14:30 | 1853 | Wuhan Zall vs Chengdu Qianbao | 5.25 | 3.64 | 1.57 |
| 14:30 | 3754 | Meizhou Kejia vs Shandong Luneng | 4.46 | 3.49 | 1.70 |
| 15:00 | 5218 | Real Madrid Youth vs Shakhtar D U19 | 1.39 | 4.87 | 5.65 |
| 15:00 | 5540 | Osmanlispor vs Bursaspor | 2.18 | 3.12 | 3.12 |
| 16:00 | 2393 | Csakvari TK vs Szentlorinc SE | 2.00 | 3.31 | 3.35 |
| 16:00 | 2737 | Soroksar vs FC Ajka | 2.21 | 3.21 | 2.97 |
| 16:00 | 3441 | FK Humenne vs FK Slavoj Trebisov | 1.76 | 3.63 | 3.88 |
| 16:00 | 4460 | Red Arrows vs Buildcon | 1.76 | 3.30 | 5.00 |
| 16:00 | 5405 | Mosonmagyarovar vs Budafoki Mte | 2.19 | 3.21 | 3.02 |
| 16:30 | 1883 | NK Dob vs Krka | 3.06 | 3.36 | 2.10 |
| 16:45 | 5567 | Al Shabbab vs Bahrain Club | 2.12 | 3.26 | 3.11 |
| 17:00 | 1108 | Slovan Velvary vs Banik Sous | 1.26 | 5.43 | 8.15 |
| 18:00 | 3049 | FC Gyori Eto vs Gyirmot FC | 2.52 | 3.20 | 2.57 |
| 18:00 | 5365 | KuPS Kuopio vs Haka | 1.60 | 3.76 | 4.77 |
| 18:30 | 2500 | Vestmannaeyjar vs Hafnarfjordur | 2.38 | 3.39 | 2.60 |
| 18:30 | 2754 | Sitra Club vs AL Khalidiyah | 4.90 | 3.60 | 1.70 |
| 19:00 | 2857 | Haladas vs Kazincbaricika SC | 2.27 | 3.11 | 2.97 |
| 19:00 | 4538 | Diosgyori Vtk vs Dorogi FC | 1.34 | 4.77 | 6.82 |
| 19:00 | 4896 | Bgsz Siofok vs Pecs MFC | 2.92 | 3.12 | 2.29 |
| 19:45 | 3014 | RB Salzburg vs Dinamo Zagreb | 1.66 | 3.87 | 4.57 |
| 19:45 | 3828 | RB Leipzig vs Celtic | 1.51 | 4.34 | 5.33 |
| 19:45 | 4757 | Zrinjski Mostar vs Siroki Brijeg | 1.86 | 3.30 | 3.84 |
| 20:00 | 1750 | Vikingur Reykjavik vs Valur | 1.67 | 3.93 | 4.03 |
| 20:30 | 3433 | Moroka Swallows FC vs Kaizer Chiefs | 3.68 | 2.68 | 2.30 |
| 21:45 | 1176 | Hull City vs Wigan | 2.55 | 3.21 | 2.65 |
| 21:45 | 1473 | Corinthian Casuals vs Cray Wanderers | 2.42 | 3.64 | 2.43 |
| 21:45 | 1717 | Burnley vs Stoke City | 1.74 | 3.60 | 4.40 |
| 21:45 | 1785 | Rotherham vs Millwall | 2.55 | 3.15 | 2.70 |
| 21:45 | 2083 | Middlesbrough vs Birmingham | 1.64 | 3.70 | 5.00 |
| 21:45 | 3125 | Watford vs Swansea | 1.93 | 3.40 | 3.75 |
| 21:45 | 5575 | Edinburgh City vs Peterhead | 1.54 | 4.13 | 5.12 |
| 22:00 | 1068 | Real Madrid vs Shakhtar Donetsk | 1.16 | 7.14 | 12.89 |
| 22:00 | 1449 | Preston vs West Bromwich | 2.98 | 3.17 | 2.33 |
| 22:00 | 4059 | Chelsea vs AC Milan | 1.67 | 3.77 | 4.66 |
| 22:00 | 4984 | Benfica vs Paris St Germain | 3.87 | 3.97 | 1.75 |
| 22:00 | 5061 | Sevilla FC vs Borussia Dortmund | 2.77 | 3.37 | 2.37 |
| 22:00 | 5563 | Manchester City vs Copenhagen | 1.07 | 9.30 | 27.13 |
| 22:00 | 5626 | Juventus vs Maccabi Haifa | 1.31 | 5.06 | 8.31 |
| 22:30 | 2933 | Colon Santa Fe vs Patronato Parana | 2.47 | 3.05 | 2.72 |
| 23:30 | 3700 | Ayacucho vs Sporting Cristal | 4.39 | 3.66 | 1.67 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Oktoba 5, 2022
Nipashe




UKURASA 29

## Van Dijk akiri mambo magumu Liverpool

FENERBEHCHE...



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa (mwenye mpira), akiwa na viongozi mbalimbali wa Klabu ya Fenerbehche ya Uturuki, alipozuru katika uwanja wao jana. Katika ziara hiyo wamekubaliana kushirikiana kwenye maeneo ya mafunzo, kambi na ujenzi wa shule za michezo. **MPIGAPICHA WETU**

# NABI AMTETEA MAYELE KUSHINDWA KUTETEMA

## ●●●Awataja mabeki, huku akieleza sasa anageukia rasmi mechi dhidi ya Al Hilal...

**Na Saada Akida**

HUKU akikiri kuzidiwa kiufundi na timu ya Ruvu Shooting katika kipindi cha kwanza juzi, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi ameeleza pia sababu ya mshambuliaji wake nguli, Fiston Mayele kushindwa 'kutetema' (kufumania nyavu) katika mchezo huo wa Ligi Kuu Bara.

Licha ya Yanga juzi kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Ruvu Shooting katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, ililazimika kusubiri hadi dakika ya 52 na 71 kuweza kuziona nyavu kupitia kwa Feisal Salum 'Fei Toto' na Bakari Mwamnyeto kabla ya Rolland Msonjo kuipatia Ruvu Shooting bao la kufutia machozi dakika ya 85.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mchezo huo, Nabi alisema wanakutana na wakati mgumu sana wanapocheza dhidi ya Ruvu Shooting tangu msimu uliopita, ambao walipata ushindi baada ya nyota wao kupewa kadi nyekundu na mechi ya marudiano kutoka sare.

Alisema hali hiyo imejitokeza tena katika mchezo huo wa juzi kwa Ruvu Shooting kuingia uwanjani na mfumo tofauti wa kutumia mabeki watatu, viungo watano na washambuliaji wawili kipindi cha kwanza hivyo kuwapa tabu ya kupata ushindi mapema.

"Leo (juzi) wamekuja na mfumo tofauti kabisa wanavyocheza, wachezaji wangu walishindwa kujua ni aina gani ya mchezo na kipindi cha kwanza kupata wakati mgumu, ukiangalia zaidi Mayele (Fiston) kacheza na mabeki watatu ambao hawakumpa nafasi kabisa wa kufunga.

"Tulipokwenda mapumziko tuliongea na wachezaji, kipindi cha pili tuliwaambia wapambane na kutumia mbinu ili kupata matokeo chanya, wamefanikiwa na kutoka na ushindi huo.

"Hata hivyo, baadhi ya wachezaji wangu walikwenda katika majukumu ya timu ya taifa katika Kalenda ya Fifa, hawako katika kiwango kizuri ikiwamo Stephen Aziz Ki, hajarudi katika timu," alisema Nabi.

Kuhusu Tuisila Kisinda, alisema anahitaji kupata muda kwa sababu bado hajawa na ubora wake hiyo ikitokana na kutocheza kwa muda mrefu.

Nabi alisema baada ya mchezo huo, sasa wanaenda kujiandaa kwa ajili ya mechi ijayo ya Ligi ya Mabingwa Afrika

INAENDELEA UK. 31

## Simba SC yakwepa figisu za Waangola

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KIKOSI cha Simba kinatarajiwa kuondoka Jumamosi alfajiri kwa ndege ya kukodi kuelekea nchini Angola kwa ajili ya mechi ya mkondo wa kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Primeiro de Agosto ya huko utakaogwa Jumapili wiki hii kwenye Uwanja wa Estadio 11 de Novembro.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, akizungumza na waandishi wetu jana, alisema kikosi kitaondoka siku hiyo kwenda kucheza moja kati ya mechi ngumu kwa ajili ya kazi moja tu, kuhakikisha wanaingia kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Kikosi kinatarajia kuondoka tarehe 8 (Jumamosi) kama mipango ya tiketi itakamilika kama ilivyopangwa kwa sababu utawala unashughulikia hilo, tarehe 9 (Jumapili) tunacheza mechi yetu, halafu tunarejea kesho yake kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya marudiano.

"Tunachoshukuru ni kwamba mechi yetu dhidi ya Dodoma Jiji haikuzalisha majeruhi, ni wale wale tu, Shomari Kapombe, Peter Banda, na Jimsony Mwanuke, Pape Shakho yeye aliondoka nchini kwenda kwao kwa sababu alifiwa, lakini amerejea, Augustine Okrah hakucheza mechi iliyopita kwa sababu hakuwa vizuri siku hiyo kiafya, na Henock Inonga alipatwa na mchafuko wa tumbo, ilibidi tumwondoe kwenye kikosi na kumweka Kennedy Juma," alisema Meneja Habari huyo.

Alisema baada ya kushinda dhidi ya Dodoma Jiji juzi, tayari kikosi kimerejea mazoezini kujiandaa na mchezo huo wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Timu imeingia kambini na kocha wetu wa muda Juma (Mgunda), anaendelea na maandalizi ya dhidi ya de Agosto kwenda kupambana kutafuta matokeo mazuri katika mechi zetu mbili za ugenini na nyumbani.

Kwa mujibu wa kigogo mmoja ndani ya Bodi ya Wakurugezi ya Simba, ambaye hakutaka kutajwa jina lake, alisema maamuzi ya kwenda huko Jumamosi ni kwa sababu kila kitu kipo tayari baada ya baadhi ya viongozi kutangulia mapema nchini humo kwa ajili ya kufanya maandalizi

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >